# Nipashe

Alhamisi Agosti 15, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579997

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



ST.JOSEPH UNIVERSITY
In Tanzania
"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on 24th August, 2019, "Entrance is free". For details www.alumni.sjuit.ac.tz

For more information contact:
+255 676 504 147
+255 745 281 505

215359802




## Bageni ashindwa rufani, sasa kunyongwa hadi kufa

UKURASA 3

# Kesi Lissu, Ndugai kunguruma Kisutu

• **Ni** ya kupinga kuvuliwa ubunge, Spika atakiwa kufika na vielelezo... *Uk.2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 7

**MHADHIRI KORTINI MADAI YA RUSHWA YA NGONO**

MHADHIRI wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Samson Mahimbo (68), amefikishwa...

UKURASA WA 24

**NEEMA YAJA WANAOVAA MIWANI KWA UONI HAFIFU**

WATANZANIA ambao wanalazimika kuvaa miwani kutokana na uoni hafifu hii ni...

UKURASA WA 26

**WATUMISHI WAPEWA SIKU 7 KULIPA 'ULTRA SOUND'**

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, ametoa siku saba kwa watumishi wote wa...




LISSU NDUGAI

## Daktari feki anaswa kanisani

UKURASA 5



## Majeruhi sita zaidi ajali lori la mafuta wafariki

UKURASA 2


MICHEZO AUSSEMS: SIMBA HII SI YAKUPIGWA TENA 5 UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Lissu, Ndugai kuwasha moto mahakamani leo

**Na Mary Geofrey**

MAOMBI ya kesi namba 18 ya mwaka 2019 yaliyofunguliwa na Mwanasheria Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, kupitia kwa mawakili wake dhidi ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, yanatarajiwa kuanza kusikilizwa leo katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Masjala Kuu ya Dar es Salaam.

Katika kesi hiyo, Lissu anapinga uamuzi wa Spika Ndugai wa Juni 28, mwaka huu wa kumvua ubunge wa Jimbo la Singida Mashariki.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Chadema, Tumaini Makene, ilieleza kuwa maombi hayo yatasikilizwa mbele ya Jaji Mtupa.

Katika taarifa yake hiyo, Makene alisema hati ya wito wa mahakama inabainisha kuwa mlalamikiwa ambaye ni Spika Ndugai, atatakiwa kufika mahakamani bila kukosa akiwa na nyaraka zote anazotakiwa kuwa nazo kwenye shauri hilo.

"Tunatoa wito kwa viongozi, wanachama, wafuasi wa Chadema na Watanzania wote wapenda haki, demokrasia na utawala bora unaoheshimu sheria, mahali popote walipo kufuatilia kwa karibu mwenendo wa shauri hilo kuanzia hatua ya sasa na kipekee kupata muda wa kufika mahakamani kuungana pamoja na kusikiliza mapambano hayo ya kuitafuta haki ya Tundu Lissu," Makene alieleza katika taarifa yake hiyo.

Alisema wameamua kutafuta haki mahakamani baada ya Spika Ndugai kutangaza kukoma kwa ubunge wa Lissu Juni 28, mwaka huu, alipokuwa akiahirisha mkutano wa Bunge la Bajeti jijini Dodoma.

Lissu ambaye pia alikuwa Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, yuko Ubelgiji akiendelea na matibabu ya kibingwa baada ya kushambuliwa kwa risasi na

INAENDELEA UK.8



Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakari Zuberi (wa nne kulia), akifanya dua fupi ya kuwaombea majeruhi waliolazwa wodini katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam juzi, kutokana na majeraha waliyopata katika ajali ya moto iliyotokea mkoani Morogoro. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Uuguzi wa Muhimbili, Yassin Munguatosha. **PICHA: JOHN STEPHEN**

# Majeruhi wengine 6 wafariki

**Na Waandishi Wetu**

MAJERUHI 14 kati ya 46 waliopokelewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) baada ya kujeruhiwa katika ajali ya lori la mafuta eneo la Msamvu Itigi mkoani Morogoro, wamefariki dunia.

Vilevile, imeelezwa kuwa majeruhi wengine 17 akiwamo mtoto, wako katika hali mbaya na wanaendelea kupatiwa matibabu kwenye chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) na wengine 15 wako wodi za kawaida za hospitali hiyo kubwa zaidi nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Huduma kwa Wateja, Aminiel Aligaesha, alisema kati ya watu sita waliofariki dunia juzi, watano walikuwa ICU.

Aligaesha alisema wagonjwa wengine tisa waliokuwa katika wodi za kawaida hali zao zilibadilika juzi, hivyo kulazimika kuwekwa ICU.

"Kati ya majeruhi 46 waliofikishwa Muhimbili, 14 wamefariki dunia, hivyo waliobaki ni 32. Wagonjwa sita walifariki dunia jana (juzi) wakati wakiendelea kupatiwa matibabu," Aligaesha alisema.

Alibainisha kuwa majeruhi 17 walio katika hali mbaya zaidi, mtoto mmoja amelazwa ICU ya jengo la watoto, mama mmoja yuko ICU ya jengo la wanawake na wengine 15 wako ICU ya jengo la Mwaisela.

Alisema majeruhi wengine 15 ambao hali zao zinaendelea vizuri, wamelazwa wodi namba 22 ya jengo la Sewahaji.

Aligaesha aliwataja waliopoteza maisha juzi kuwa ni Joseph Lewanga (48), mkazi wa Mafisa, Jafari Kilombero (30), mkazi wa Mafisa, Margreth Mtunguja (44), mkazi wa Kichangani, Ramadhani Ally (26), Mussa Athumani (28), mkazi wa Mtawala na Garadia Mbaruka (26), mkazi wa Morogoro.

Alisema miili yote imehifadhiwa katika chumba maalum cha kuhifadhia maiti katika hospitali hiyo na kwamba wanaendelea na taratibu nyingine wakitarajia kutoa taarifa zaidi leo.

Alisema hospitali hiyo inaendelea kuchukua sampuli za wagonjwa walio mahututi ili kuoanisha na watu wanaojitokeza kutambua ndugu zao.

Aligaesha alisema kutokana na kuwapo kwa changamoto ya ndugu zaidi ya wawili kumgombania mgonjwa mmoja, waliamua kuishirikisha Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kuchukua sampuli kwa ajili ya utambuzi wa kisayansi.

Aligaeshi pia alisema vijana na makundi mbalimbali yamekuwa yakijitokeza kwa kuchangia damu kwa ajili ya majeruhi hao.

"Mwitikio ni mzuri, watu wanaendelea kujitokeza kuchangia damu na sisi tunaendelea kuhimiza wananchi kujitokeza kuchangia damu kwa sababu damu inahitajika kwa wingi," Aligaesha alisema.

Alisema walishachukua vinasaba vya wagonjwa wote waliokuwa chumba cha uangalizi maalum (ICU) na kwamba wanasubiri ndugu zao wajitokeze kuwatambua.

**ILIVYOKUWA MUHIMBILI**

Nipashe ilishuhudia kundi kubwa la watu karibu na eneo la jengo la kuhifadhia maiti katika hospitali hiyo wakitaka kutambua ndugu zao waliopoteza maisha.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya watu waliofika eneo hilo, wakieleza kuwa walikuwa wakisubiri kupata taarifa za

INAENDELEA UK.8

## Wamiliki wa malori wachangia mil. 20/- kwa majeruhi

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Wamiliki wa Malori nchini (Tatoa), kimetoa msaada wa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya majeruhi wa moto wa ajali ya lori la tangi la mafuta, Msamvu mkoani Morogoro.

Akizungumza jana Dar es Salaam wakati akikabidhi msaada huo, Makamu Mwenyekiti Tatoa, Elias Lukumay, alisema, wamiliki wa malori wameguswa na tukio hilo ambalo limeleta maafa ndani ya jamii.

Alisema tukio hilo hakuna wa kulaumiwa kwa kuwa linaweza kumpata mtu yeyote hivyo cha msingi ni kuhakikisha majeruhi hao wanasaidiwa kwa hali na mali.

"Tukio hili limegusa watu wengi hivyo kama wamiliki wa malori tumeona ni jambo letu sote hivyo tumeamua kuungana na wenzetu kutoa vifaa tiba na vitendanishi ili kuweza kuwasaidia majeruhi hawa," alisema Lukumay.

Lukumay alisema walipokea ushauri kutoka hospitalini hapo aina ya msaada uliokuwa unahitajika na hatimaye wamefanikiwa kutoa ili uweze kuwasaidia wagonjwa hao.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Idara ya Utasishaji Hospitali ya Taifa Muhimbili, Batusaje John, alisema, vifaa hivyo ni muhimu kwa majeruhi wa moto ambao wamekuwa wakihitaji joto kwenye vidonda na usafi.

Alisema vifaa walivyopokea ni pamoja na gozi, pamba, mafuta ambavyo vitasaidia wagonjwa hao wasipate bakteria na kutunza ngozi zao.

Batusaje alisema wamejipanga kuhakikisha wanafanyakazi usiku na mchana ili kuweza kuokoa maisha ya majeruhi.

"Msaada huu utawafikia walengwa moja kwa moja kwani tuna imani wanahitaji zaidi vifaa tiba kuliko fedha," alisema Batusaje.

Wakati huohuo, jumla ya uniti za damu 170 zimepatikana tangu kuanzishwa kwa uchangiaji wa damu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ili kuokoa maisha ya majeruhi wa moto waliolazwa hospitalini hapo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Muhimbili, Aminiel Eligaesha, alisema, damu hiyo imepatikana baada ya wachangiaji wengi kuhamasika kuja kujitolea kuokoa maisha ya majeruhi.

Alisema katika uchangiaji huo Naibu Waziri wa Kilimo na Mifugo, Abdallah Ulega na timu yake ya vijana kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), walichangia jumla ya uniti 100.

Alisema pia taasisi ya kamanda mstaafu, Suleiman Kova ya SUKOS, walichangia kiasi cha uniti 70.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Ama Kasangala, alisema, jana walipokea wasanii wa kikundi cha Pilipili tisa waliochangia damu.

Alisema waendelea kuhamasisha watu wengi kuendelea kujitokeza kwa wingi kuchangia damu.

"Tunahamasisha Benki ya Damu iwe na damu ya kutosha pia wananchi nao wajenge mazoea ya kuchangia damu kila wakati," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Mahakama yatupa rufani ya Bageni, ahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imesema hukumu dhidi ya Mkuu wa zamani wa Upelelezi Wilaya ya Kinondoni, (kwa sasa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni), Mrakibu wa Polisi (SP) Christopher Bageni, aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa ilikuwa sahihi na kwamba inatupilia mbali maombi yake ya mapitio.

Kadhalika, imesema imeangalia mwenendo mzima wa kesi, lakini haijaona kitu kipya katika hoja za mapitio zilizowasilishwa na mlalamikaji na kwamba ilitimiza majukumu yake kama Mahakama ya Kwanza ya Rufani.

Uamuzi huo ulisomwa jana na Naibu Msajili Mwandamizi, Elizabeth Mkwizu baada ya maombi hayo kusikilizwa na jopo la majaji watatu likiongozwa na Jaji Stella Mugasha, Ferdinand Wambari na Rehema Kerefu.

Hukumu hiyo inatokana na kesi ya msingi ya wafanyabiashara wanne wa madini kutoka Mahenge, Morogoro waliodaiwa kuuawa na polisi ambao ni Sabinus Chigumbi, maarufu Jongo na ndugu yake, Ephrahim Chigumbi, Mathias Lunkombe na dereva teksi, mkazi wa Manzese Dar es Salaam, Juma Ndugu.

Msajili alisema Mahakama ya Kwanza ya Rufani ina wajibu wa kuangalia kilichotokea katika ushahidi ili iweze kutimiza majukumu yake ya utoaji haki.

Alisema wakati hukumu iliyotolewa dhidi ya mshtakiwa, mahakama hiyo haikufanya kosa la kuathiri haki ya mshtakiwa kwa kuzingatia mambo mawili.

Moja, mahakama ilipomtia hatiani ilizingatia ushahidi uliotolewa na mshtakiwa mwenzake Rajabu Bakari, ambaye alishuhudia tukio la mauaji hayo.

Pili, katika msitu wa Pande mshtakiwa ndiye alikuwa ofisa wa juu kuliko wote ingawa Rajabu hakusikia akitoa amri ya kufanyika mauaji, lakini kwa mujibu wa Jeshi la Polisi ofisa wa juu ndiye mwenye mamlaka ya kutoa amri.

Jopo limeridhika na ushahidi huo na kwamba uliungwa mkono kwa namna nyingi na Bageni ikiwamo mwenendo wake baada ya tukio hilo.

Msajili aliendelea kusoma kuwa, Bageni alidanganya kwa viongozi wake kwamba kulikuwa na majibishano ya risasi kati ya wafanyabiashara na polisi eneo la Sinza, jijini Dar es Salaam huku akijua si kweli.

Hata hivyo, ushahidi wa Jamhuri unaeleza hapakuwa na majibishano ya risasi siku ya tukio.

Pia, Bageni aliamuru askari kwenda kupiga risasi baharini na kuonyesha maganda tisa kwa viongozi wake huku akijua si kweli.

"Mahakama hii imeona kwamba Bageni ameshindwa kuishawishi mahakama kwamba ilikosea kumtia hatiani, hatuna namna zaidi ya kutupilia mbali maombi yake," alisema Msajili Mkwizu, akinukuu jopo lililosikiliza maombi hayo.

Mapema mahakamani hapo, Bageni alifungua maombi ya mapitio akitaka imwachie huru kwa sababu uamuzi wa Mahakama ya Rufani Tanzania, uliomtia hatiani hakupata nafasi ya kujitetea.

Kadhalika, alidai kuwa uamuzi wa rufani iliyomtia hatiani iliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), ilikuwa na hoja za kisheria na kwamba mlalamikaji Bageni hakupata nafasi ya kujibu na kujitetea.

INAENDELEA UK. 8

# Waziri Mkuu azindua mwongozo uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amezindua Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkoa wa Kagera wenye lengo la kutangaza fursa za uwekezaji, hivyo kukuza maendeleo ya mkoa huo na ameziagiza halmashauri zote za wilaya nchini ziondoe urasimu na kupunguza vikwazo kwa wawekezaji.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana wakati akizindua Kongamano la Wiki ya Kagera na Mwongozo wa Uwekezaji mkoani humo, mjini Bukoba, na kuwataka Watanzania wahakikishe wanachangamkia fursa za biashara zilizopo.

Alisema Watanzania wanao uwezo wa kutumia fursa za uwekezaji na biashara zilizopo nchini kwa kushirikiana na taasisi za kifedha na kuwekeza katika miradi mbalimbali nchini, badala ya kuachia fursa hizo kuchukuliwa na wageni.

Alisema azma ya Serikali ya kukuza uchumi kupitia sekta na kufikia wa kati ifikapo mwaka 2025 itaendelea kutekelezwa, hivyo, alikaribisha wawekezaji wa nje nao waje kuwekeza.

"Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda Awamu ya Tatu (2010/2020) na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/2016 2020/2021) ambao lengo lake ni kuendeleza uchumi wa viwanda".

Akizungumzia kuhusu maadhimisho ya Wiki ya Uwekezaji Kagera, Waziri Mkuu alisema yamelenga kuwakutanisha wadau wa uwekezaji, ambao ni pamoja na Wafanya

INAENDELEA UK. 8


**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA ANDAN GROUP COMPANY LIMITED,**

Kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali lifuatalo:

| NAMBA | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MMILIKI DHAMANA | AINA YA DHAMANA | AUCTION COMPANY | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1` | PAMBA | KATARAMA/SIMON,STRATON | SAMWEL/S,NEEMA | NYUMBA | BOSTON AUCTION MARTS | BWIRU | 30/08/2019 | SAA 4:00 NAKUENDELEA |
| 2. | PAMBA | NGAWIZAKUMBUGA/G,FABIAN | NGAWIZAKUMBUGA/G,FABIAN | TITILE 29235 TITLE NO 44463 | BOSTON AUCTION MARTS | MWANZA | 30/08/2019 | SAA 4:00 NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

**Dhamana zitauzwa mahali zilipo**

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (nyundo itakaposhushwa), salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.

i. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

ii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**Kwa mawasiliano:**

**Mratibu wa MIKOPO AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu**
**Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340**
**Barua pepe: info@accessbank.co.tz**
**Simu ya Dalali husika: +255766547732 BOSTON AUCTION MARTS**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215373601



fcs

**TAARIFA KWA UMMA**



**Menejimenti ya Foundation for Civil Society (FCS)** inapenda kuutaarifu Umma kuwa **Ndg. Amos Mwakabambo** hajawahi kuwa wakala, mwakilishi au mfanyakazi wa taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS).

Tunatoa rai kwa wananchi na wadau wote wa Asasi za Kiraia nchini kwamba Taasisi yetu haitahusika kwa namna yoyote ile na taarifa au uwakilishi unaofanywa na **Ndg. Amos Mwakabambo.**

**Imetolewa na,**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Foundation for Civil Society**
**S.L.P 7192 Dar es Salaam**
**Simu: +255 22 266 4890-2, +255 754 005708**
**Barua pepe: information@thefoundation-tz.org**
**15/08/2019**

215374302

HABARI KITAIFA

# Wanasaikolojia watua Moro kusaidia waathirika wa ajali lori la mafuta

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

TIMU kutoka Wizara ya Afya na wataalamu wa kisaikolojia, imewasili Morogoro kutoa tiba ya kisaikolojia kwa waathirika wa ajali ya lori la mafuta lililopinduka na kuwaka moto eneo la Msamvu Itigi katika Manispaa ya Morogoro Jumamosi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alitangaza kuwasili kwa timu hiyo alipozungumza na waandishi wa habari mjini Morogoro.

Alisema licha ya utambuzi, mazishi na tiba, huduma nyingine itakayoanza kutolewa ni tiba ya kisaikolojia kwa walioathiriwa na ajali hiyo na ndiyo maana timu hiyo ya wataalamu imewasili Morogoro.

Alitoa rai kwa vyombo vya habari, hasa vinavyoendesha

INAENDELEA UK.7



Daktari Bingwa wa macho wa Hospitali ya Kimataifa ya Macho (International Eye Hosptal), Aydin Yildirim akimfanyia tiba mtu mwenye uoni hafifu, ili kumwezesha kuona mbali au karibu bila kutegemea kuvaa miwani, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana, ambapo huduma hiyo imeanzishwa hapa nchini kwa mara ya kwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Pinda atoa ushauri kuipanga Dodoma

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameushauri uongozi wa Jiji la Dodoma kwenda China kujifunza namna ya kuupanga mji huo ili uendane na hadhi ya makao makuu ya nchi.

Pinda alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuonyesha vyakula vyenye asili ya China ambayo iliandaliwa na Ubalozi wa Watu wa China.

"Nilipokuwa katika jimbo moja la China, nilipata bahati ya kwenda katika maonyesho ambayo dhamira yake ilikuwa ni kutaka watu wajue wamepiga hatua katika mipango miji.

"Na ni kweli wamepiga hatua kubwa sana na miji yao ni mikubwa na imepangwa vizuri na maeneo mengine ukiambiwa ni makao makuu ya mkoa huamini.

"Ndiyo maana nimemwomba sana Balozi wa China nchini, atusaidie kutuunganisha katika miji iliyojengeka vizuri nchini kwake ili kile tulichokiona kule cha mipango miji na sisi tupeleke vijana wetu kwenda kuona na kujifunza na wakirudi wanakuwa wamepanuka vizuri uelewa juu ya mipangomiji.

Pinda pia aliwashauri Watanzania kuanza kutengeneza vyakula vya asili ya China katika hoteli wanakofikia watalii kutoka nchi hiyo.

"Dhamira kubwa ni kwamba wameona Tanzania ina mwelekeo wa mvuto wa watalii kutoka China. Kwa hiyo, wanaona ni vema wanapokuja kufanya utalii, wanapata kabisa na vyakula vya kwao.

"Hata mazao yetu tunayolima wenyewe wamesema wanaweza kuyatumia hayo katika kupika chakula cha kichina," Pinda alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema tayari wamekamilisha mapitio ya mpango kabambe wa makao makuu ya nchi ambao utaendana na mabadiliko yaliyofanyika ya ujenzi wa

INAENDELEA UK. 8

## UDART yafafanua msongamano vituoni

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI inayotoa huduma katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), imesema msongamano wa abiria kwenye kituo cha Mbezi Mwisho uliotokea jana asubuhi ulisababishwa na foleni.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano UDART, Deus Bugaywa, aliliambia Nipashe kuwa msongamano wa abiria katika kituo hicho ulisababishwa na foleni ya magari ambayo hutumia njia moja na mwendokasi.

"Hatuna upungufu wa magari, msongamano unaouzungumzia wa leo (jana) haujasababishwa na upungufu wa mabasi, umetokana na foleni barabarani kwasababu mwendokasi unapita kwenye njia ya kawaida Kimara mwisho hadi Mbezi, ambayo magari mengine hutumia," alisema.

Alisema foleni husababisha magari hayo kuchelewa vituoni na kwa sababu hayafiki kwa muda uliopangwa idadi ya abiria huwa kubwa.

Mradi huo ulianza Mei, 2016 ukiwa na mabasi 140 na kati ya hayo, 39 ni makubwa yenye urefu wa mita 18 na uwezo wa kubeba abiria 155 na mengine 101 ni ya urefu wa mita 12 yenye uwezo wa kubeba abiria 90.


Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku

215227501



## HABARI KITAIFA



Mafundi wa Kampuni ya Estim, wakiendelea na kazi ya kuweka lami ikiwa awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, katika eneo la Kimara Temboni, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha, mkoani Pwani yenye urefu wa kilomita 19.
**PICHA: JOHN BADI**

# Daktari feki anaswa akitibu kanisani

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKAZI wa Visiga, Kibaha mkoani Pwani, Moses Masoud (34), anashikiliwa na polisi mkoani Ruvuma kwa tuhuma za kukutwa akitoa huduma za kidaktari, kwa madai kuwa ni daktari wa magonjwa ya binadamu.

Mtuhumiwa huyo, kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, Masoud alikamatwa juzi akitoa huduma hizo katika kanisa la Jesus Miracle (JMC), eneo la Msamala kwa Gasa, Manispaa ya Songea wakati hana sifa hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kamanda Maigwa alisema polisi walipata taarifa kutoka kwa raia wema kuwa kuna mtu mmoja anafanya kazi ya kutibu magonjwa mbalimbali ya binadamu.

Kamanda alisema baada ya kupata taarifa hizo, walikwenda kwenye eneo la tukio wakiwa wameongozana na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dk. Jairy Khanga, na kumkamata akiwa anatoa huduma kwa wagonjwa, huku akiwa na vifaa tiba na dawa mbalimbali ambazo zilikuwa zinatolewa kwa wagonjwa.

Alisema katika mahojiano ya awali yaliyofanywa na polisi mkoani hapa kwa kushirikiana na Dk. Khanga, mtuhumiwa huyo alikiri kuwa amekuwa akifanya kazi hiyo, lakini hana taaluma za kidaktari na hajawahi kuhitimu mafunzo ya aina yoyote katika vyuo vya udaktari ndani na nje ya nchi.

Kamanda alisema taarifa za awali zilizopokelewa na polisi kutoka kwa wananchi ambao ni raia wema, zilidai kwamba mtuhumiwa kwa zaidi ya wiki mbili tangu

INAENDELEA UK. 26

# Wataalamu dawa SADC wanolewa

**Na Devota Mwachang'a**

WATAALAMU wa dawa nchini na wengine kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi wa dawa ili kupata timu ya wataalamu wenye uelewa wa pamoja wataoweza kukagua dawa kwa kufuata taratibu, sheria na kanuni zinazofanana kwa nchi zote.

Mafunzo hayo ya siku 14 yaliyoanza jijini Dar es Salaam yamefadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na kusimamiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA), yamekutanisha wakaguzi 30 kutoka nchi 14 wanachama wa SADC.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainab Chaula, amesema wakati nchi inasimamia mkutano mkuu wa SADC, ni fursa ya kuitambua hatua ambayo nchi imefikia katika masuala mbalimbali kimataifa.

"Tunawashukuru WB kwa kutengeneza programu inayofanya mifumo ya dawa kuuwianishwa na kuwawezesha wataalamu wa nchi mbalimbali kufahamu, kuwawezesha wawe na uelewa wa pamoja katika ukaguzi wa dawa...tunafaidika na uwapo wa wataalamu hawa nchini pia sisi tunawapa elimu wenzetu," alisema.

Dk. Chaula aliwaeleza wataalamu kuwa Tanzania kupitia TMDA imepiga hatua kubwa hadi kutunukiwa cheti cha mifumo bora ya usimamiaji wa dawa na vifaa vya dawa, na inaongoza katika nchi za Afrika kwa kuwa na ukomavu wa hadhi ya ngazi ya Tatu (maturity level III), na kuwa hii ni kutokana na kujituma na kuwa na jitihada endelevu.

Vilevile, Katibu Mkuu alisema vita ya udhibiti wa dawa na uwapo wa dawa bora nchini unategemea zaidi umoja na kuwa na lugha moja kati ya Tanzania na nchi jirani.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, alifafanua kuwa ukaguzi unaofanywa na wataalamu ni katika kuhakiki ubora wa dawa kwenye viwanda.

"Hivyo mafunzo yatazalisha timu ya wataalamu watakaotumika katika ukaguzi wa pamoja utakaofanywa kwenye nchi wanachama wa SADC," alisema.

Mratibu wa Uwianishwaji wa Mradi kwa nchi za SADC kutoka Zimbabwe, Sakhile Mwedzi, alisema mafunzo yanalenga kuwawezesha wataalamu kutatua masuala yanayoathiri afya za watu kwenye nchi wanakotoka.

# Shahidi akana mawasiliano na Zitto

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Kijiji cha Mpeta Uvinza, Petro Salum (50), amedai mahakamani kwamba hajawahi kuwasiliana na Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, kuhusu idadi ya watu waliokufa katika operesheni ya kuwaondoa wananchi waliokuwa wakiishi maeneo ya hifadhi ya wanyama Uvinza.

Salum ambaye ni shahidi wa Jamhuri katika kesi ya uchochezi inayomkabili Zitto, alitoa ushahidi wake jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, shahidi alidai Mkuu wa Wilaya ya Uvinza alimfahamisha kwamba wananchi wanatakiwa kuhamishwa katika hifadhi hiyo, hivyo alikuwa akiomba eneo la kuwahamishia.

Shahidi alidai alikaa na halmashauri ya kijiji, eneo lilipatikana

INAENDELEA UK. 26


**SUMAJKT AUCTION MART**

**MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYO PEWA NA TUJIJENGE TANZANIA LIMITED TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA/ VIWANJA KAMA JEDWALI LINAVYOONESHA HAPA CHINI.MUDA WA MNADA NI KUANZIA SAA NNE ASUBUHI

| s/no | JINA | MAHALIZILIPO | DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | REGINALD MIKE KIBULA/ SAID KHAMIS NASSORO | MTONIKIJICHI | NYUMBA | 17/08/2019 |
| 2 | NAKUNDWA JOHN MIYOMBO | MLANDIZIMSEDUKWA | KIWANJA | 21/08/2019 |
| 3 | ABDUL HASHIM SAID | MBONDOLE KIVULE | NYUMBA | 24/08/2019 |
| 4 | NAOMI JOSEPH WAMBURA | MBONDOLEKIVULE | NYUMBA | 24/08/2019 |
| 5 | DANIEL ELIAS NYAMBEHO | PUGU BOMBANI | NYUMBA | 28/08/2019 |
| 6 | ABDALLAH HUSSEIN LAKUMO | BUYUNI MGEULE CHANIKA | KIWANJA | 28/08/2019 |
| 7 | DONATH M. MALLYA | VIKONGORO CHANIKA | NYUMBA/ KIWANJA | 31/08/2019 |
| 8 | CLARA MATHIAS KWILASA | CHANIKA MTAA WA ZAVARA | KIWANJA | 31/08/2019 |
| 9 | CHARLES MWITA KIBANDERA | VIWEGE MAJOHE | NYUMBA | 04/09/2019 |
| 10 | EMMANUEL NDULU | CHANIKA KIGEZI CHINI | NYUMBA | 04/09/2019 |

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mteja anatakiwa kulipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14
2) Endapo Mteja atashindwa kumalizia 75% ya salio lililobaki ndani ya siku 14 hatarudishiwa kiasi alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
3) Gharama zote za kubadili **HATI MILIKI ni JUU YA MNUNUZI.**

215374502

**Kwa mawasiliano zaidi piga namba:- 0716004554 NA 0753063481**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

August 15, 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya jumapili Tarehe 15/08/2019 kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **NGAKA COAL MINING** kuelekea NAMANGA gari hilo lenye namba za usajili:

**T875CZT/T901 CZT**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19.5 |
| Upana | - | mita | 2.70 |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika**: NGAKA COAL MINING hadi NAMANGA Kupitia LINDI, g**ari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215374002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kazi sasa kwenu mabalozi wetu kwa majukumu SADC

**MABALOZI** 42 wa Tanzania katika nchi mbalimbali wamewasili kwa ajili ya kumshuhudia Rais John Magufuli anavyokabidhiwa Uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Rais Magufuli anayerajia kupokea kijiti cha uenyekiti wa jumuiya hiyo kubwa katika eneo la Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka viongozi wakuu wa nchi na serikali za nchi wanachama zipatazo 16 mwishoni mwa wiki hii jijini Dar es Salaam.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alisema juzi kuwa mabalozi hao wamepewa wito rasmi kushiriki mikutano ya SADC inayoendelea nchini kabla ya mkutano wa kilele wa wakuu wa nchi na serikali Jumamosi na Jumapili.

Alisema leo watatembelea mradi wa ufuaji umeme wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) uliopo Rufiji mkoani Pwani, ambao unatarajiwa kuzalisha umeme wa megawati 2,100, ambao utaiwezesha Tanzania kuondokana na changamoto za nishati ya umeme.

Wakiwa nchini, wawakilishi watu nje ya nchi, pia watatembelea miradi kadhaa mikubwa inayotekelezwa nchini.

Kwa mujibu wa Msemaji Mkuu wa Serikali, ni muda tangu wameondoka nchini, hivyo watakwenda huko kujionea mradi huo unaotekelezwa na serikali kwa fedha za ndani, ili watumie fursa ya kuwahamasisha wawekezaji kuja nchini kuwekeza.

Kwa kuwapa jukumu hilo mabalozi wetu ni kuuongezea nguvu mkakati wa serikali wa kitangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini, hususan ambazo zimeongezwa na utekelezaji wa miradi mikubwa. Kwa mfano, mradi wa Rufiji ambao utazalisha umeme wa kutosha, utawezesha kuanzishwa kwa viwanda vingi.

Hali hiyo itakuwa ni kivutio kikubwa kwa kutilia maanani kuwa kukosekana kwa nishati (umeme) wa uhakika kwa miaka mingi nchini, kulikuwa kikwazo kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda. Baada ya mabalozi wetu kutembelea mradi huo, bila shaka kila mmoja akirejea katika nchi anayowakilisha, atafanya kila jitihada za kuitangaza fursa hiyo kushawishi na kuvutia wawekezaji wa huko.

Pia mabalozi waliopo kwenye nchi za SADC nao watakabidhiwa uenyeviti kama ilivyofanyika juzi kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, kupokea uenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa SADC.

Kualikwa kwa mabalozi wetu walioko ughaibuni kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa SADC, pamoja na mambo mengine, lengo ni kuhakikisha Tanzania inatimiza kikamilifu majukumu yake katika kusukuma mbele masuala mbalimbali yanayohusu jumuiya hiyo kwa mwaka mzima ambao itakuwa mwenyekiti.

Kwa kuwashirikisha mabalozi wetu wote walioko ughaibuni, kutawezesha kila mmoja kwa nafasi yake popote aliko kuitangaza fursa zilizomo katika SADC.

Kwa kuwa mabalozi waliopo kwenye nchi za SADC nao watakabidhiwa uenyeviti wa jumuiya hiyo, lazima watambue kuwa huo ni mtihani mkubwa sana kwao.

Tunasena hivyo kwa kuwa watakuwa na majukumu mengi na makubwa ya kufanya kuhakikisha kuwa Tanzania kama mwenyekiti inawezesha shughuli za Sadc zisonge mbele kwa kasi badala ya kukwazwa.

Watakaoshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, watakuwa wanamkwamisha Rais Magufuli katika kuiongoza jumuiya hiyo katika mwelekeo mpya wa kujibadili kutoka katika historia ya ukombozi kuelekea katika mtangamano wa uchumi mkubwa kupitia ushirikiano wa biashara, viwanda na uwekezaji.

Tunatarajia kuanza kuwaona mabalozi wetu wakiipaisha Tanzania katika hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tohara muhimu kupindukia katika zama hizi za Ukimwi

**KATIKA** vita ya kupambana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU), kumekuwa na mikakati mbalimbali kwa ajili ya kufanikisha vita hiyo, mojawapo ikiwa ni kuhamasisha tohara kwa wanaume.

Tohara inahamasishwa, kwa vile inaelezwa kitaalamu kwamba mtu asiyetahiriwa ana asilimia 60 zaidi ya kupata VVU, kulinganishwa na aliyetahiriwa.

Hiyo ni kwa mujibu wa wataalamu wa afya ambao wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa wanaume kufanyiwa tohara, ili angalau kupata unafuu wa kinga kutoka ugonjwa huo, ingawa bado kuna ukweli naye aliyetahiriwa naye yuko katika uwezekano wa kuambukizwa VVU.

Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo bado ziko katika mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa, kwa kubuni mbinu mbalimbali za kukabiliana nao ikiwamo hiyo ya kuhimiza tohara.

Kumekuwapo na matangazo redioni na kwenye mabango yanayoweka wazi ukweli, mwanamume asiyetahiriwa ana asilimia kubwa ya kuambukizwa virusi vya Ukimwi, anapokutana na mwenzi mwenye virusi, pasipo kutumia kinga .

Kwa kutambua hilo, sasa ni muda mrefu tangu Tanzania iingie katika kampeni za 'dondosha mkono wa sweta', lengo likiwa ni kuzuia maambukizi ya virusi vya Ukimwi na baadhi ya watu wameitikia kwa kufanyiwa tohara.

Mfano mmojawapo ni mkoani Shinyanga ambako katika kipindi cha mwezi Oktoba 2016 hadi Machi 2017, zaidi ya wanaume 47,500 walinufaika na huduma ya tohara, kupitia kampeni ya tohara kinga ya maambukizi ya VVU.

Ni kampeni inayoendeshwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Intrahealth International.

Siyo Shinyanga tu, serikali imeandaa mpango wa kitaifa wa kutekeleza huduma za tohara ili kufikia lengo la kitaifa la asilimia 80 kutoka asilimia 72, kipaumbele kikielekezwa kwenye mikoa yenye viwango vya chini vya huduma za tohara na maambukizi ya VVU.

Mikoa hiyo ni Iringa, Njombe, Mbeya, Rukwa, Katavi, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera, Ruvuma na Mara, hususan wilaya ya Rorya. Wataalamu wa afya wanasema, tohara ya mwanaume imethibitika kuwa salama na yenye mafanikio inapofanywa katika mazingira rasmi ya utoaji tiba, hivyo ni muhimu kuichangamkia.

Ni vyema wanawake nao wakahusika kuhamasisha waume zao kufanikisha mpango huo wa tohara kama ambavyo wenzao wa mkoa wa Geita, wamewahi kufanya kwa lengo la kuhakikisha wanaume wote wanatahiriwa.

Ushiriki wa wanawake katika kampeni hizo mkoani Geita ulisaidia kuwafanyia tohara wanaume 119,000 ambao wengi wao walikuwa ni vijana kati ya miaka 20 na 29 kwa vile ndilo kundi linalodaiwa kufanya ngono zisizo salama.

Wataalamu wanasema pia kwamba tohara inaelezwa kuwa ni kinga yenye uwezekano wa kupunguza kupata saratani ya kichwa cha uume na magonjwa mengine ya zinaa.

Hiyo inatokana na kwamba kitaalamu, magonjwa mengi hujificha kirahisi katika ngozi ile inayotakiwa kukatwa na pia kubaki bila kutahiriwa ni uchafu kwa mwanaume.

Kwa maana hiyo kuna umuhimu mkubwa kwa kila mwanaume kufanyiwa tohara kwa vile inaweza kusaidia mtu kuwa salama dhidi ya magonjwa hayo, lakini si kwamba hawezi kuambukizwa virusi vya Ukimwi.

Inawezekana wapo baadhi ya wanaume ambao wanaona aibu kwenda kutahiriwa, aibu hiyo inaweza kuzaa matatizo, hivyo jambo la msingi ni kuachana nayo na kuchukua hatua sahihi za kufanyiwa tohara. Kwa wale ambao wamekuwa wakiendekeza mila na desturi, wakidai kwamba ni makosa kutahiriwa, wajue kuwa huu siyo wakati wa kuendekeza mila zilizopitwa na wakati kwani zinaweza kuwa majanga kwao.

Jambo la kuzingatia ni kwamba kutahiriwa hakumpunguzii mwanaume chochote kwenye maumbile yake zaidi ya kukatwa ngozi tu ambayo inasemekana kutunza uchafu.

Uchafu huo unaotajwa kuwa chanzo cha kuleta maambukizi ya magonjwa mbalimbali, hivyo njia rahisi na salama ni wanaume wote kukubali kufanyiwa tohara bila kujali umri wao.

HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, akimkabidhi hati ya ardhi Jenita Mapunda katika eneo la Uledi Kata ya Mpera Manispaa ya Tabora, wakati wa ziara yake mkoani Tabora. **PICHA: WANMM**

# Wakurugenzi kikaangoni makusanyo kiduchu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza wakurugenzi wa halmashauri ambazo zimefanya vibaya kwenye makusanyo, utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo na asilimia 10 kwa makundi maalum kujitathmini na kuandika barua ya kujieleza ndani ya siku 14.

Pia amasema halmashauri na mikoa iliyofanya vibaya kwenye makusanyo, itapewa zawadi maalum ya kinyago cha uzembe chenye sura mbaya ambacho kitawekwa kwenye ofisi za wakurugenzi na wakuu wa mikoa.

Agizo hilo alilitoa jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya makusanyo kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2018/19. Katika makusanyo hayo, Jafo alisema wakurugenzi wa halmashauri 12 wamekusanya mapato kutoka vyanzo vya ndani chini ya asilimia 50 na kwamba ziko halmashauri 80 zimekusanya chini ya asilimia 80, kiwango ambacho ni cha chini kilichowekwa na ofisi hiyo. Kutokana na hali hiyo, alisema wakurugenzi wa halmashauri hizo wanatakiwa kujieleza kwa kushindwa kukusanya kwa kiwango kilichowekwa.

Sambamba na hilo, alisema wakurugenzi wa halmashauri 102 wameshindwa kuchangia katika miradi ya maendeleo kwa asilimia 20, huku akibainisha kuwa zaidi ya halmashauri 40 zimeshindwa kuchangia katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. "Hawa nao watoe maelezo na sababu za kushindwa kusimamia Kanuni za Usimamizi wa Fedha za michango ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu," alisema.

Jafo alifafanua kuwa katika mwaka wa fedha 2018/19, halmashauri zilipanga kukusanya Sh. bilioni 723.7 kutoka kwenye vyanzo ya ndani na ndicho kilikuwa kipimo kwa wakurugenzi.

"Mapato halisi yaliyokusanywa katika kipindi hiki ni Sh. bilioni 661.4 ambayo ni takribani asilimia 90 ya malengo ya mwaka huo na ni ongezeko la asilimia tisa kwa kulinganisha na makusanyo ya asilimia 81 ya mwaka 2017/18," alisema.

**WALIO KIKAANGONI**

Waziri Jafo alisema miongoni mwa halmashauri za mwisho kwa kigezo cha wingi wa mapato yaliyokusanywa (pato ghafi) ni za wilaya za Kakonko (Sh. milioni 408.2), Buhigwe (Sh. milioni 403.8), Kigoma (Sh. milioni 397.1), Gairo (Sh. milioni 396.2) na Mji Nanyamba (Sh. milioni 257.6).

Halmashauri za mwisho kwa kigezo cha asilimia ya mapato ya ndani, kwa mujibu wa Jafo ni za wilaya ya Newala (27), Masasi (26), Msalala (19), Tandahimba (19) na Mji Nanyamba asilimia 11.

Kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Jafo alizitaja halmashauri hizo kuwa ni za wilaya za Kalambo (mbili), Korogwe (tatu), Momba (tatu), Same (nne), Gairo (nne), Manyoni (nne); na Mji Kondoa pia asilimia 4.

Pia alisema halmashauri tano za mwisho kwa kigezo cha asilimia ya fedha zilizotengwa kuwezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni za wilaya za Morogoro (18), Momba (16), Bariadi (16), Ileje (13) na Kyela (11) na Manispaa ya Kigoma (15).

**MIKOA YA MWISHO**

Jafo aliitaja mikoa ya mwisho kwa kigezo cha asilimia ya mapato ya ndani yaliyokusanywa kulinganisha na jumla ya makisio ya halmashauri kuwa ni Mara (80), Kigoma (74), Shinyanga (62), Simiyu (59) na Mtwara (42).

Alitaja mikoa mitano ya mwisho kwa kigezo cha wingi wa mapato yaliyokusanywa (pato ghafi) ni Njombe (Sh. bilioni 11.5), Simiyu (Sh. bilioni 8.8), Rukwa (Sh. bilioni 8.2), Kigoma (Sh. bilioni 7.8) na Katavi (Sh. bilioni 7.4).

**DODOMA KINARA**

Wakati halmashauri zikishika nafasi za mwisho, Jafo alitaja halmashauri tano zilizoongoza kwa kigezo cha wingi wa mapato yaliyokusanywa (pato ghafi) na kiasi kwenye mabano kuwa ni Jiji Dodoma (Sh. bilioni 71.7), Manispaa za Ilala (Sh. bilioni 58.2), Kinondoni (Sh. bilioni 34.0), Temeke (Sh. bilioni 33.3) na Ubungo (Sh. bilioni 18.6). Kwa upande wa halmashauri tano zilizoongoza kwa kigezo cha asilimia ya mapato ya ndani yaliyokusanywa kulinganisha na makisio ya halmashauri ni wilaya za Mbozi (198), Wanging'ombe (165), Kilolo (150), Misenyi (142) na Mji Geita.

**MIKOA ILIYOONGOZA**

Jafo alisema mikoa mitano iliyoongoza kwa kigezo cha wingi wa mapato yaliyokusanywa (pato ghafi) ni Dar es Salaam (Sh. bilioni 163.6), Dodoma (Sh. bilioni 82.7), Mwanza (Sh. bilioni 32.7), Arusha (Sh. bilioni 31.9) na Mbeya (Sh. bilioni 31.4).

Pia alisema mikoa mitano iliyoongoza kwa kigezo cha asilimia ya mapato ya ndani yaliyokusanywa kulinganisha na jumla ya makisio ya halmashauri ni Geita (119), Iringa (117), Songwe (112), Kagera (105) na Njombe asilimia 104.

# Wanasaikolojia watua Moro kusaidia waathirika wa ajali lori la mafuta

**INATOKA UK. 4**

shughuli zake kupitia mitandao ya kijamii, kuacha kupotosha taarifa za tukio hilo, husussan idadi ya majeruhi na vifo.

Alisema baadhi ya mitandao ya kijamii imekuwa ikitumika kupotosha umma kuhusu tukio hilo kwa kusingizia vifo kwa baadhi ya watu, na kwamba wenye jukumu la kutoa taarifa zozote ni Kamati ya Maafa ya Kitaifa iliyo chini ya ofisi yake au ile ya mkoa iliyo chini ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro.

"Mtu anasema majeruhi Hospitali ya Morogoro amehesabu wamebaki 14 wakati ukweli hadi sasa wamebaki majeruhi 16, ni vyema taarifa hizi zikatolewa na mamlaka husika badala ya kila mtu kutaja au kujiandikia vile anavyofikiri," Mhagama alisema.

Kuhusu maendeleo ya tume ya kuchunguza tukio hilo la ajali iliyoundwa na Waziri Mkuu, Waziri Mhagama alikataa kuizungumzia akidai kuripoti shughuli zozote za tume ya aina hiyo ambayo ipo kwa mujibu wa sheria, ni lazima taarifa zake zitolewe rasmi kwa kuwa tayari kuna mfumo wa kujiratibu na utoaji wa taarifa.

Hata hivyo, waziri huyo alisema tayari tume hiyo imeshaundwa na imeanza kazi na kutakuwa na utaratibu rasmi wa utoaji wa taarifa zake bila kuharibu uchunguzi, hivyo Watanzania waendelee kusubiri kitakachobainika baada ya uchunguzi wa tume hiyo.

Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ng'ondi, aliyeongoza timu ya wataalamu wanaoshiriki kutoa tiba hiyo wakiwamo maofisa ustawi wa jamii na maofisa maendeleo ya jamii, Chama cha Wanataaluma wa Ustawi wa Jamii, Chuo cha Ustawi wa Jamii Kijitonyama na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema watazitambua familia zilizopoteza ndugu na walioopata majeruhi ili kuzipa huduma hiyo.

"Msaada huu ni muhimu sana kwa binadamu yeyote, inapotokea jambo la kushtusha kama hili huwa inaleta msongo wa mawazo na kuchanganyikiwa. Kwa hiyo, hii inasaidia kurejesha walioathirika kurudi katika hali zao za kawaida na kufanya kazi," alisema.

Nipashe ilitembelea Mtaa wa Sume, Kata ya Mwembesongo katika Manispaa ya Morogoro na kuzungumza na uongozi wa mtaa huo, ambao ulibainisha kuwa kupoteza watu 19 katika tukio hilo, wengi wao wakiwa ni vijana.

Meneja wa CRDB Mkoa wa Morogoro, Steven Mapunda, alisema benki hiyo iliguswa na tukio hilo na kutoa misaada mbalimbali tangu ajali hiyo ilipotokea.

## Mhadhiri NIT kortini madai ya kuomba rushwa ya ngono

**Na Hellen Mwango**

MHADHIRI wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Samson Mahimbo (68), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na tuhuma za kuomba rushwa ya ngono kwa mwanafunzi wa chuo hicho.

Mhadhiri huyo ambaye alikuwa akifundisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza 2015/16, anadaiwa kuomba rushwa hiyo kutoka kwa mwanafunzi Victoria Faustine.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Vera Ndeoya, alidai kuwa Januari 12, 2017 katika nyumba ya kulala wageni, iliyopo Mwenge jijini Dar es Salaam, mshtakiwa aliomba rushwa ya ngono.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo akiwa mwajiriwa wa NIT katika kozi ya Usimamizi wa Barabara na Usafirishaji namba LTU 07101 kwa kutumia mamlaka yake, alimlazimisha mwanafunzi huyo kutoa rushwa ya ngono.

Ilidaiwa kuwa aliomba rushwa hiyo ili aweze kumfaulisha katika mtihani wake wa marudio katika kozi ya Usimamizi wa Barabara na Usafirishaji anayosomea ya Januari 5, 2017.

Mshtakiwa alikana mashtaka hayo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe ya kuanza kusikilizwa.

Hakimu alimtaka mshtakiwa kuwa na mdhamini mmoja atakayesaini hati ya dhamana ya Sh. milioni nne na alitimiza masharti hayo.

Alisema kwa kuwa mshtakiwa ametimiza masharti ya dhamana atakuwa nje mpaka Septemba 17, mwaka huu, kesi hiyo itakapoanza kusikilizwa.

# Mahakama yatupa rufani ya Bageni

INATOKA UK. 3

Wakili wa upande wa mlalamikaji, Gaudiosis Ishengoma, wakati akiwasilisha hoja za mapitio mbele ya jopo la majaji watatu, likiongozwa na Jaji Mugasha, Wambari na Kerefu.

Ishengoma alidai kuwa maombi ya mlalamikaji dhidi ya DPP ni kuiomba mahakama kufanya mapitio ya uamuzi wake wa Septemba 16, 2016, uliomtia hatiani kigogo huyo wa zamani wa polisi.

Vile vile, alidai kuwa uamuzi huo ulikuwa unalenga kutengua hukumu ya Mahakama Kuu iliyowaachia huru baada ya ushahidi wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha tuhuma za mauaji ya wafanyabiashara watatu na dereva taksi mmoja.

Alidai kuwa pamoja na mambo mengine mamlaka ya mahakama hiyo ni kufanya mapitio uamuzi wake pale inapotokea ukiukwaji wa haki haiwezi kuachwa ikawa hivyo.

"Kwa uhalisia wa kesi hii rufani iliyoletwa na DPP, mlalamikaji hakupata nafasi ya kusikilizwa wakati Mahakama ya Rufani ilipotengua uamuzi wa kumtia hatiani, uamuzi huo wa Mahakama Kuu katika kutafsiri kifungu cha kanuni ya 22 na cha 23 ya adhabu kwamba huwezi kumtia hatiani mtu aliyesaidia kuua ukamwacha aliyeua," alidai Ishengoma.

Upande wa mlalamikiwa DPP ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislais Komanya, ulidai kuwa mlalamikaji hana sababu za msingi za kutengua uamuzi uliomtia hatiani.

Komanya alidai kuwa rufani ya kesi hiyo ilishasikilizwa kwamba sasa si wakati wake kusikilizwa kwa mgongo wa mapitio.

Alidai kuwa SP Bageni alipata nafasi ya kusikilizwa na kwamba mahakama itupilie mbali mapitio hayo.

"Mahakama hii ilitoa uamuzi wake kupitia hukumu ya Mahakama Kuu ikionyesha kuwa ilitolewaje, jopo la majaji lilijadili kwa kina hukumu ya mahakama ya chini na uamuzi wake ulikuwa sahihi," alidai na kuongeza:

"Mahakama hii ina uwezo wa kusikiliza jambo na kulifanyia uamuzi kwa hiyo mambo yatakayoletwa yazingatie kifungu cha 66 kidogo cha (1) (b) cha kanuni ya adhabu, maombi ya mlalamikaji tunaona hayajakidhi vigezo vinavyotakiwa, kwa kuruhusu maombi kama haya ambayo hayafiki mwisho, tunafungua mwanya kwa wengine yatupiliwe mbali," alidai Komanya.

Katika maombi yake SP Bageni, alipinga hukumu iliyotolewa katika mahakama hiyo chini ya jopo la majaji watatu likiongozwa na Jaji Bernard Luanda, Sauda Mjasiri na Senistocles Kaijage, kwamba lilifanya makosa ya dhahiri.

Pia, alidai kuwa jopo hilo lilifanya makosa katika mwenekano na kusababisha haki kutokuzingatiwa mahakama hiyo itengue hukumu hiyo.

Septemba 16, 2016, 3:45 asubuhi, Msajili wa mahakama hiyo (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu), John Kahyoza, alisoma hukumu hiyo baada ya kusikilizwa rufani iliyokatwa na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

DPP alipinga hukumu ya Mahakama Kuu iliyowaachia huru aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Dar es Salaam (RCO) Kamishna Msaidizi wa Polisi wa zamani, Abdallah Zombe na maofisa wenzake watatu akiwamo Bageni, mwaka 2009.

Akisoma hukumu hiyo Msajili Kahyoza, aliwataja walalamikiwa kuwa ni ACP Zombe, SP Bageni, aliyekuwa Mkuu wa Upelelezi wa Kituo cha Polisi Urafiki, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Ahmed Makelle na Rajabu Bakari.

Alisema Mahakama ya Rufani ilipitia ushahidi uliotolewa Mahakama Kuu na kuona kwamba ilishindwa kuwatia hatiani washtakiwa kwa mauaji na kwa kosa la kusaidia mauaji kufanyika.

"Kosa la kuua na kosa la kusaidia kuua ni makosa mawili tofauti, si sahihi kwa mtu aliyeshtakiwa kwa mauaji kutiwa hatiani kwa kosa jingine, tangu mwanzo mshtakiwa alitakiwa kulijua ili aweze kujitetea," alisema na kuongeza:

"Washtakiwa wote katika utetezi wao walipinga kuhusika katika mauaji hayo, lakini mlalamikiwa wa nne Rajabu alisema ukweli katika ushahidi wake kwa kueleza tukio la mauaji lilivyofanyika katika msitu wa Pande, lakini ushahidi wake ulitakiwa kupokelewa kwa makini na ulitakiwa kuwapo na ushahidi mwingine wa kuunga mkono," alisema Msajili Kahyoza.

Akifafanua msajili alisema, "mlalamikiwa wa kwanza Zombe, mahakama haioni kama kuna ushahidi wa kumtia hatiani kwa mauaji wala kwa kusaidia kuua japo kuna jambo kichwani mwake ninalolifahamu kuhusu mauaji hayo, ushahidi mwingine unaonyesha wajibu rufani watatu walishuhudia mauaji, lakini hawakuua," linasema jopo. Jopo lilisema wamekubaliana kwamba watu wanne waliuawa kwa bunduki na mauaji yalikuwa ya kinyama katika msitu wa Pande. "Mahakama hiyo ilijiuliza maswali kwamba je, wajibu rufani walikuwapo Pande? Jibu ni kwamba walalamikiwa wa pili, wa tatu na wa nne walikuwapo katika msitu huo na kwamba mlalamikiwa wa nne alisema ukweli mahakamani kuhusiana na tukio hilo."

Ilidaiwa kwamba mauaji hayo yalifanywa na askari polisi Sadi, lakini mshtakiwa huyo hajawahi kushtakiwa, mahakama inajiuliza marehemu walipelekwa Pande kwa amri ya nani.

Kwa mujibu wa ushahidi mahakama inajiuliza nini nia ya kuwapeleka marehemu Pande sehemu ambayo haina hata nyumba, mlalamikiwa wa pili, Bageni ndiye alitoa amri ya kuua, ushahidi unaonyesha washtakiwa waliwapeleka wakiwa hai Pande na waliwarejesha wakiwa marehemu.

"Marehemu walipelekwa huko ili tukio la mauaji lifanyike bila kipingamizi kwa kibali cha Bageni, ushahidi wa mlalamikiwa wa nne uliungwa mkono na tabia ya Bageni kwamba alikuwa akificha ukweli kuhusu mauaji hayo," alisema.

Hata hivyo, ushahidi wa maofisa watatu wa Jeshi la Polisi, wote walidanganya kwamba mauaji yalitokea Sinza katika majibizano kati ya Polisi na marehemu wakati wengine wa Sinza walisema hawakusikia tukio la aina hiyo kutokea.

"Mahakama hii imeona walalamikiwa wa kwanza, wa tatu na wa nne, rufani dhidi yao inatupwa hakuna ushahidi wa kuwatia hatiani, mlalamikiwa mahakama inatengua kuachiwa kwake kutiwa hatiani na Mahakama Kuu, inamuhukumu kunyongwa hadi kufa kwa mauaji ya watu wanne," alisema Msajili Kahyoza na kusababisha mahakama hiyo kulipuka kwa vilio.

Katika kesi ya msingi, wafanyabiashara wa madini kutoka Mahenge, Morogoro waliouawa ni Sabinus Chigumbi, maarufu Jongo na ndugu yake, Ephrahim Chigumbi, Mathias Lunkombe na dereva teksi, mkazi wa Manzese Dar es Salaam, Juma Ndugu.

Walidaiwa kutenda makosa hayo Januari 14, 2006, katika msitu wa Pande, uliopo wilayani Kinondoni baada ya kuwakamata wafanyabiashara hao Sinza, walipokuja Dar es Salaam kuuza madini.

# Waziri Mkuu azindua mwongozo uwekezaji

INATOKA UK. 3

biashara kutoka ndani ya mkoa na nchi jirani zinazozunguka Mkoa wa Kagera.

"Ni ukweli usiofichika kwamba tunahitaji wawekezaji watakaosaidia uchumi wa mkoa huu kukua kwa kasi kupitia fursa zilizopo kwenye nyanja za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, maliasili na utalii."

Waziri Mkuu alisema ukuaji mzuri wa uchumi wa mkoa utakuwa na manufaa katika kuongezeka kwa pato la mwananchi wa Kagera, pato la mkoa na hata pato la taifa nalo litakuwa kwa kasi ndani ya kipindi cha muda mfupi.

Amesema Mkoa wa Kagera ndiyo unaoongoza kwa uzalishaji wa kahawa nchini, ambapo zaidi ya nusu ya kahawa yote huzalishwa katika mkoa huo. Wastani wa uzalishaji wa kahawa kwa mwaka ni kati ya tani 50,000 hadi tani 65,000 kutegemea na hali ya hewa ya mwaka husika.

Hivyo, mkoa huo una fursa kubwa ya uwekezaji kwenye viwanda vya kukoboa na kusindika kahawa.Pia mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa michache Tanzania yenye fursa nyingi za uwekezaji.

"Kagera imepakana na Uganda, Rwanda, Burundi na Kenya. Kupakana na nchi hizo zenye idadi kubwa ya watu katika ukanda huu wanaokadiriwa kufikia takriban milioni 190 ambapo kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2018 ni fursa ya uwepo wa soko kubwa la bidhaa zinazozalishwa au zinazoweza kuzalishwa katika mkoa wa Kagera," alisema.

Kadhalika, Waziri Mkuu alisema Serikali imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ya usafiri ukiwamo wa anga na wa barabara ili kurahisisha usafiri kutoka Bukoba makao makuu ya mkoa wa Kagera kufika katika nchi hizo.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema dhamira ya kuandaliwa kwa wiki ya uwekezaji mkoani Kagera ina lengo la kuhakikisha kwamba mkoa huo unafanya vizuri katika sekta ya uwezekezaji na biashara, hivyo kuchangia katika ukuaji wa pato la Taifa.

Alisema mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa 10 ambayo inamchango mdogo katika pato la Taifa, hivyo wanataka watoke kwenye kuchangia asilimia 3.9 hadi wafikie asilimia 10.

Kwa upande wao, viongozi mbalimbali wakiwamo Magavana kutoka nchi za Rwanda na Burundi waliahidi kutumia fursa zilizopo nchini, pamoja na kuwakaribisha wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania kwenda kuwekeza katika nchi zao.

## Majeruhi wengine 6 wafariki

INATOKA UK. 2

namna ya kuhifadhi miili ya ndugu zao baada ya kupokea taarifa za vifo.

"Tuko hapa tangu asubuhi, tuliambiwa ndugu yetu ameshafariki, ilipofika saa sita mchana, alikuja kiongozi wao akatusomea majina ya waliofariki na akatuambia anahitajika ndugu wa damu wa marehemu kama mama mzazi kwa ajili ya kwenda kupewa maelekezo mengine," alisema Jumanne Mnyenyelwa, mkazi wa Morogoro.

Kwa majeruhi wengine sita kufariki dunia juzi, idadi ya watu waliopoteza maisha katika ajali hiyo sasa imefika 82. Lori hilo lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli, lilianguka na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.

***Imeandikwa na Mary Geofrey, Philip Nyiti na Mariam Magili**

## Lissu, Ndugai kuwasha moto

INATOKA UK. 2

watu wasiojulikana wakati akijiandaa kushuka kwenye gari lake nyumbani kwake mjini Dodoma Septemba 7, 2017.

Baada ya kunusurika kifo katika shambulio hilo, Lissu alipatiwa matibabu ya awali katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na baadaye kusafirishwa kwenda Hospitali ya Nairobi, Kenya kwa matitabu ya dharura kisha kuhamishiwa Ubelgiji ambako amekuwa akipata matibabu tangu Januari 2018.

Mwanzoni mwa mwaka huu, afya ya Lissu ilionekana kuimarika alipofanya ziara katika nchi kadhaa za Ulaya na Amerika na kuzungumza na vyombo vikubwa vya habari, akiilaumu Serikali ya Tanzania kwa kushindwa kuwapata waliomshambulia.

Mtalaamu huyo wa sheria pia aliweka wazi kuwa atawania nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu ujao ikiwa chama chake kitaamua hivyo huku akitangaza kuwa amepanga kurejea nchini Septemba 7, mwaka huu, tarehe aliyoshambuliwa mwaka juzi.

## Pinda atoa ushauri kuipanga Dodoma

INATOKA UK. 4

mji huo.

"Tangu mji (wa Dodoma) umejengwa ni zaidi ya miaka 40, kwa hiyo hatuwezi kwenda na mpango uleule, mpango huo utatoa taswira ya Dodoma katika miaka 20 ijayo.

"Waziri Mkuu mstaafu yuko sahihi na sisi tunalifanyia kazi na tunaamini miaka kadhaa ijayo litakuwa jiji la mfano kwa sababu linajengwa katika karne ya 21 na teknolijia mpya,"alisema.

Balozi wa China nchini, Wange Ke, alisema kama ambavyo wamekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania, watahakikisha wanawaunga mkono katika ujenzi wa jiji hilo hususani kwa kuwapekeka wataalamu kwenda kujifunza nchini mwao.

"TTB (Bodi ya Utalii Tanzania) kwa sasa inafanya kazi kubwa ya kutangaza utalii Tanzania na kwa sasa inapata watalii wengi wakiwamo wanaotoka China.

# EAC yafunguka madai ya ukata kuikwamisha

**Novatus Makunga,** ARUSHA

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC) imeeleza kuwa haijateteleka kutokana na ukata unaodaiwa kuchangiwa na nchi wanachama kushindwa kutoa michango yao na hivyo kusababisha watumishi wa kada mbalimbali kurejea katika nchi wanazotoka.

Ufafanuzi huo ulitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa EAC, anayeshughulikia mipango, miundombinu, fedha na utawala, Mhandisi Steven Mlote, na alisema watumishi wote wa jumuia hiyo walelipwa mishahara yako iliyopita kwa wakati ukiondoa wabunge ambao alisema kwa utaratibu wao walilipwa katika wiki ya kwanza ya mwezi huu.

Mlote alisema kuwa watumishi wa jumuiya 14 wapo likizo akiwamo Katibu Mkuu wa jumuiya hiyo, Balozi Liberat Mfumukeko.

Aidha, alisema watumishi wengine 11 wapo katika majukumu ya kikazi nje ya makao makuu ya jumuiya akiwamo naibu katibu mkuu anayeshughulikia uzalishaji na sekta za kijamii, Christopher Bazimo na mtumishi mmoja yupo katika likizo ya uzazi.

Makao makuu ya jumuiya hiyo, yanawahusisha watumishi wa vyombo vinne ambavyo ni Sekretariati, Mahakama ya Afrika ya Mashariki (EACJ) na Bunge la Afrika ya Mashariki (EALA).

Aidha, jumuiya hiyo ambayo ina watumishi zaidi ya 400, pia ina taasisi shiriki nyingine nane zilizosambaa katika nchi wanachama.

Akizungumzia nchi wanachama kushindwa kutoka michango yake, Mlote alisema ni mapema kuanza kuzihukumu nchi hizo kwani mwaka wa fedha ulianza mwezi uliopita, huku nchi zikipewa hadi Desemba 31 kuwasilisha michango yake.

Kwa mujibu wa taarifa za ndani ya jumuiya hiyo, nchi ya Sudan Kusini haijawahi kutoa michango kwa muda mrefu, huku Burundi nayo ikisuasua katika uwasilishaji wa michango yake.

Naibu katibu huyo wa EAC hakuwa tayari kufafanua kuhusiana na Sudan Kusini kwa kushindwa kutoa michango, huku akieleza ni vyema kuisaidia nchi hiyo katika kipindi hiki iweze kurudisha hali yake ya amani wa ndani ya nchi.

Hata hivyo Mhandisi Mlote alisema Uganda tayari imeshawasilisha sehemu ya mchango wake wa mwaka huu wa fedha wa 2019/2020. Nchi wanachama kila moja katika mwaka wa fedha unatakiwa kuchangia dola za Marekani 8,378.

Kwa mujibu wa mkataba wa uanzishwaji wa EAC, kila nchi inapaswa kutoa mchango wake uliowekewa ukomo kila ifikapo Desemba 31 ya kila mwaka kabla ya mwaka wa fedha unaoanza Julai Mosi na kuishia Juni 30.

Katika hatua nyingine, Mlote alisema kuwa Rais Yoweri Museveni wa Uganda atazindua kamati ya kutengeneza Katiba ya Shirikisho la kisiasa la Afrika Jumatatu ijayo jijini Kampala.

Alisema kamati hiyo ambayo imepewa miezi sita na ilishaanza kazi ikiwa na jumla ya wataalamu 18, ambapo kila nchi itatoa watu watatu na inatakiwa kukamilisha kazi yake Novemba mwaka huu.

Mlate alisema kuwa kamati itapita katika nchi zote wanachama kukusanya maoni na baadaye yatawasilishwa katika mkutano wa wakuu wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo Novemba 30, mwaka huu.




Meneja Masoko wa Huduma za Kifedha wa Vodacom Tanzania, Noel Mazoya, akizungumza na vijana 22 kutoka nchi 16 duniani waliotembelea ofisi za makao makuu ya kampuni hiyo, chini ya Shirika la Young Global Pioneers, jijini Dar es Salaam jana. Vijana hao walijifunza kuhusu masoko ya ndani na kimataifa na pia huduma ya malipo kwa kutumia simu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni zaomba kutafutiwa soko la pamba

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

KAMPUNI zinazomiliki viwanda vya kuchambua pamba na ununuzi wa zao hilo katika Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, zimeiomba serikali kuwasaidia kutafuta masoko.

Meneja uzalishaji wa kampuni ya Kahama Oil Mills LTD inayomiliki kiwanda cha kuchambua pamba na kusindika mafuta ya kula cha mjini Kahama, Braithon Edward, ndiye aliyetoa ombi hilo juzi baada ya kutembelewa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, kwa lengo la kujionea shughuli za uchambuaji wa pamba.

Edward aliliambia gazeti hili kuwa kampuni yake inaendelea na ununuzi wa pamba kwa wakulima, huku akijiapiza kununua pamba nyingi na kuongeza kuwa wanashirikiana na kampuni nyingine zenye viwanda vya kuchambua pamba ili kuhakikisha pamba yote iliyopo kwa wakulima inanunuliwa. "Kampuni yangu inatekeleza vyema agizo la serikali kuhakikisha kuwa pamba yote iliyopo kwa wakulima inanunuliwa na kuisha kabisa ila ombi letu serikali iangalie uwezekano wa kutusaidia kutafuta masoko ambayo yamekuwa changamoto kubwa," alisema na kuongeza:

"Kwanza hali hii imefanya idadi kubwa ya wananchi wanajipatia ujira kwa kufanya vibarua kiwandani hapa nina vibarua zaidi ya 400."

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliliambia gazeti hili kuwa lengo la ziara yake katika viwanda vya kuchambua pamba wilayani humo ni kujionea shughuli ya uchambuaji na kuyahimiza makampuni hayo yaongeze bidii kununua pamba kwa wingi ili kuhakikisha mkulima ananufaika na rasilimali hiyo licha ya bei ya pamba duniani kuteteleka.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau kama benki, bei ya dunia tumeweka pembeni na kuanza kununua pamba kwa wakulima na hadi sasa jumla ya kilo milioni 2.5, lengo la serikali ya wilaya ni kuhakikisha inanunua pamba milioni 4.7," alisema Macha.

# Kampuni ya TCCIA yapata faida mil.366/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya TCCIA Investment imesema imepata faida ya Sh. milioni 366.57 katika mwaka 2018 ikilinganishwa na Sh. milioni 246.57 za mwaka 2017 na Sh. milioni 154.17 za mwaka 2016.

"Kampuni yetu inaendelea vizuri," alisema Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni hiyo, Fortunatus Magambo, wakati wa mkutano mkuu wa mwaka.

Aliuambia mkutano huo kwamba katika mwaka ulioisha Desemba 2018, faida ya kampuni kabla ya kodi ilishuka kwa asilimia 44 hadi Sh. milioni 195.78 ikilinganishwa na faida ya 2017 na kutaja sababu za kushuka huko kuwa ni pamoja na kupanda kwa gharama katika manunuzi.

Aliwaeleza wajumbe kwa kusema kwamba faida baada ya kodi ilipanda kwa asilimia 49 kufikia Sh. milioni 366.57 kutokana na bidii iliyofanywa kuchanganua na kusimamia mapato yatokanayo uwekezaji katika hati fungani za serikali na pia gawio kutoka kwa kampuni ambako TCCIA Investment imewekeza.

Mkutano uliidhinisha malipo ya gawio la shilingi 2.54 kwa kila hisa kama ilivyokuwa mwaka 2017.

Aidha, kampuni hiyo, imewekeza kwenye mashirika na taasisi mbalimbali za fedha ikiwamo NMB, CRDB, Dar es Salaam Commercial Bank (DCB), Viwanda vya Saruji vya TWIGA, SIMBA, Tanzania Breweries (TBL), Swiss Port, na Kiwanda cha Sigara (TCC).

Tangu kuanzishwa kwa kampuni hii mwaka 2005, imeweza kufanya vizuri katika uendeshaji wake kiasi cha kuweza kujenga imani kubwa kwa wanahisa wake nchini.

Kampuni ya wanahisa ya TCCIA Investment ni moja ya kampuni za wanahisa inayofanya vizuri na kuchangia harakati za kuondokana na umaskini katika jamii.

# Mradi wa maji kuwakomboa watu 64,000

**Elizabeth Faustine na Neema Emmanuel,** MWANZA

JUMLA ya wakazi 64,000 wa wilaya Misungwi mkoani Mwanza wapo mbioni kunufaika na huduma ya maji kufuatia hatua ya majaribio ya kufungua maji katika mradi wa Nyahiti kuanza.

Mradi huo uliogharimu fedha kutoka serikali ya Tanzania shilingi bilioni 12 na kujengwa ndani ya miezi 24 unatarajiwa kukamilika mwezi huu Agosti 30, mwaka 2019.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijiji Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga, alisema hayo wakati walipofanya ziara na waandishi wa habari wa mkoa huo katika kituo cha tiba ya maji Capripoint na mradi wa maji Nyahiti.(Nyahiti Water Pumping Misungwi)

Mhandisi Sanga alisema lengo la mradi huo ni kuwahudumia wakazi wote wa Misungwi hivyo mwanzoni mwa mwezi Septemba wakazi hao watakuwa wamepata huduma ya maji.

"Tumefanya majaribio leo Agosti 9 kwa mara ya kwanza, kuwasha mtambo huu wa Nyahiti kwa kusukuma maji mpaka kwenye haya matenki mawili kama mlivyoshuhudia, mabomba ambayo ni mapya huku moja likiwa na ujazo lita 300,000 na jingine lita 600,000 na baada ya hapo yatasambazwa kwa wakazi wa Misungwi ili waweze kupata maji safi na salama," alisema Mhandisi Sanga.

Aidha, alisema, katika mradi huo wameshaunganisha wateja 1,400 ambapo zoezi linaendelea na kuanzia wiki hii watawafungia mita, lakini kabla watasafisha kwanza mabomba kwa ajili ya kuondoa uchafu na baada ya hapo wanatarajia kuwaunganisha wateja wengine zaidi ya 2,500.

"Lengo ni kuwahudumia wakazi wa Misungwi, hivyo tunatarajia mwanzoni mwa mwezi septemba wakazi hao watakuwa wamepata maji hayo, kwani tunapo 'dizaini' miradi ya maji hatuangalii mahitaji ya sasa bali ya miaka 10 hadi 20 ijayo," alisema Sanga.

Naye Mtaalamu wa Maabara ya MWAUWASA kutoka kituo cha tiba ya maji Capripoint, Yusuph Bunzali, aliwaeleza waandishi kuwa, wanayatibu maji kwa kwa mujibu wa sheria kwa kudhibiti aina yeyote ya uchafu usipite na kuhaikisha kuwa wanaweka dawa bila kuizidisha wala kupunguza ili kulinda afya ya mtumiaji.

Bunzali alisema, maabara hiyo inauwezo wa kutibu maji lita milioni 4.2 kwa saa moja, hivyo kila sekunde dawa inaingia katika matenki ya maji.



Mtaalamu wa maabara ya Mwauwasa kutoka katika kituo cha tiba ya maji Capripoint, Yusuph Bunzali, akionyesha muundo wa namna maji yanavyoanza kuingia kwenye matangi na kufanyiwa tiba kwa kuwekewa dawa mpaka kumfikia mtumiaji yakiwa safi na salama kwa matumizi. **PICHA NA ELIZABETH FAUSTIN**E

# Dawa watumishi wanaotusi wagonjwa sasa yapatikana

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, limemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, kufunga kamera(CCTV) kwenye wodi zote na ofisi za madaktari ili kuwadhibiti watumishi ambao wamekuwa wakitoa lugha chafu kwa wagonjwa.

Madiwani waliyabainisha hayo jana kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo walisema malalamiko ya wagonjwa kutolewa lugha chafu na baadhi ya wauguzi yamekithiri na kufungwa kwa kamera hizo kutasaidia kupunguza malalamiko hayo.

Walisema kuwa endapo mkurugenzi atafanikiwa kufunga kamera kwenye wodi na ofisi za madaktari, pia itasaidia kuwabaini watumishi au madaktari ambao wamekuwa na tabia ya kuiba dawa na kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo kuwafukuza kazi.

Shedrack Nkwambi, Diwani wa Nyihogo alisema wamekuwa wakipokea malalamiko mengi kutoka kwa wagonjwa juu ya kurushiwa maneno machafu na baadhi ya watumishi ambao sio wadilifu, na wamekuwa wakikosa ushahidi wa kuwachukulia hatua za kisheria.

"Mkurugenzi utakapofunga CCTV kwenye wodi itasaidia kupunguza unyanyaji kwa wagonjwa hasa wanawake unaofanywa na baadhi ya watumishi ambao sio waadilifu. Hata wagonjwa akinababa huwa wanafanyiwa vitendo hivyo lakini wanashindwa kutoa taarifa," alisema Nkwambi.

Diwani Viti Maalumu Kata ya Malunga, Berenadeta Mbagale, alisema asilimia kubwa ya wagonjwa ambao wamekuwa wakirushiwa maneno machafu na waguzi ni kinamama ukilinganisha na kinababa.

Aidha, alisema wamekuwa wakipata malalamiko mengi kutoka kwa wagonjwa kuhusiana na kufanyiwa vitendo hivyo, lakini wamekuwa wakikosa ushahidi wa kuwachukulia hatua kutokana na ushahidi wa maneno badala wa video au sauti.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, Anderson Msumba, alisema kwa sasa Halmashauri inajenga jengo la kupumzikia wagonjwa wa nje (OPD) na kila wodi na ofisi za madaktari zitafungwa CCTV ili kukabiliana na changamoto ambazo zimekuwa kiripotiwa na wagonjwa.

# Hati yenye shaka ya CAG yaiweka h/shauri matatani

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MENEJIMENTI ya Halmashauri ya Wilaya ya Tabora (Uyui) imepewa mwezi mmoja kuhakikisha imejibu na kumaliza kujibu hoja 72 za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zilizosalia ili ziweze kufungwa na kuondoa dosari zilizojitokeza kwenye ukaguzi uliopita. Hoja hizo zinahusu miradi na manunuzi mbalimbali iliyotumia zaidi ya Sh. milioni 515.4 ambayo hayana uthibitisho.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati wa kikao maalumu cha Baraza la Madiwani kupitia hoja mbalimbali kutoka ofisi ya CAG kwa mwaka 2017/18.

Alisema hoja hizo ndio zimesababisha halmashauri hiyo kuwa kati ya halmashauri saba nchini zilizopata hati yenye shaka, hivyo ni lazima zijibiwe kwa kuwasilisha vielelezo vitakavyothibitisha matumizi ya fedha hizo kama yalifuata taratibu.

Awali akiwasilisha taarifa Mkaguzi Mkuu wa Nje, Anicet Mushumbusi, alizitaja sababu zilizopelekea kupata hati yenye shaka ni pamoja na kutokuwapo kwa uthibitisho wa fedha za amana kiasi cha Sh. milioni 30.4, malipo yenye shaka kwa kazi hewa ya shilingi milioni 95.2.

Sababu nyingine ni manunuzi ya shajala kwa ajili ya vikao mbalimbali yenye thamani ya Sh. milioni 116.5 ambayo hayana mchanganuo na malipo yenye nyaraka pungufu kiasi cha Sh. milioni 20.4.

Mushumbusi aliongeza sababu nyingine ni upungufu kwa vidadisi bei zilizowasalishwa na watoa huduma kabla ya manunuzi ya vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 200.5 na manunuzi yaliyofanyika bila ushindanishi ya Sh. milioni 52.2.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, alisema watawachukulia hatua watumishi wote ambao wameisababishia halmashauri hiyo kuzalisha hoja za kiukaguzi na kupata hati yenye shaka.

Alisema watumishi ni vema wakajitahidi kuzuia hoja na sio kutoa maamuzi ambayo yanasababisha kuendelea kuzalisha hoja kila mwaka.

Aliitaka menejimenti ya halmashauri hiyo kuunda timu ya kushughulikia hoja hizo ili ndani ya mwezi mmoja wawe wamejibu na kufutwa.

Makungu aliwaomba madiwani kuhakikisha wanafuatia katika kata zao ili miradi mbalimbali ya wananchi inakuwa na ubora unaotakiwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Said Ntahondi, alisema wameunda timu ya madiwani na wataalamu watakaochunguza watendaji waliosababisha wapate hati yenye shaka ili waweze kuchukuliwa hatua.

# Masoko yalivyowaunganisha wajasiriamali Arusha, K'njaro

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

ZAIDI ya wajasiriamali 10,000 kutoka vikundi 450 katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, wamenufaika na elimu ya ujasiriamali na kuunganishwa na masoko ya kuwakwamua kiuchumi.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa tawi la Arusha kutoka shirika linalojihusisha na elimu ya ujasiriamali la Hand in Hand Eastern Afrika Tanzania, Jane Sabuni, wakati akizungumza na wajasiriamali wanaosaidiwa na shirika hilo.

Alisema wajasiriamali hao wamekuwa wakifanya shughuli mbalimbali, baada ya kuwezeshwa na shirika hilo kupitia mafunzo ya aina tofauti, yakiwamo namna ya kutunza fedha zao na kuweka akiba.

Alisema ni lengo la kuwawezesha wajasiriamali ili kuondokana na kupunguza umaskini kupitia uanzishwaji wa biashara ndogondogo na kutengeneza fursa za ajira kwa watu wengine.

"Tumejiwekea malengo ya kufikia zaidi ya wajasiriamali 10,000 kwa kila mwaka katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, ambapo tumevuka lengo tayari hivyo hadi kufikia Desemba mwaka huu tutakuwa tumewafikia wajasiriamali wengi zaidi," alisema.

Aliongeza zaidi kuwa, wamekuwa wakiwafundisha wajasiriamali namna ya kuongezea thamani ya bidhaa zao ili kushindana na soko la ajira.

Alifafanua wamewafundisha wajasiriamali hao teknolojia mpya ya kutengeneza mkaa kwa kutumia migomba na kinyesi ambapo teknolojia hiyo inatunza mazingira kwa kiwango kikubwa.

Selestina Wilson, mkazi wa Sakina anayejishughulisha na utengenezaji wa sabuni za maji, alisema shirika hilo limemsaidia kwa kiasi kikubwa kujikwamua kiuchumi, kwa kuanzisha biashara hiyo ambayo alikuwa hana ujuzi nao. Aidha, alisema changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu wa vifungashio, kwani vilivyopo ni vichache, hivyo wakipatiwa elimu namna ya kutengeneza vifungashio hivyo, wataweza kupata kwa haraka na kwa wingi pia.

Martha Jeremia Mkazi wa Kijiji cha Sasi Kata ya Bangata, mjasiriamali anayetengeneza taulo za kike za asili, alisema shirika hilo limeweza kumpa elimu namna ya kutengeneza taulo hizo kwa kutumia mashine ya cherehani, ambayo ni ya bei nafuu na kila mmoja ana uwezo wa kumudu gharama.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, akipokea maelezo ya utafiti kwa mwanafunzi wa elimu ya juu kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha nchi ya Korea (Seoul), Frank Manongi, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa kimataifa wa nishati endelevu na teknolojia ya maji. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Ndalichako aagiza watafiti kutengeneza teknolojia rahisi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ameviagiza vituo na taasisi za utafiti kutengeneza teknolojia rahisi, itakayorahisisha na kuchochea maendeleo kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa tatu wa kimataifa wa nishati endelevu na technolojia ya maji katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela(NM-AIST), Ndalichako alisema ni wakati kwa vituo vya utafiti na taasisi zinazojihusisha na tafiti, kubuni teknolojia rahisi itakayochangia kuchochea maendeleo kwa kasi katika jamii.

Alisema kuwa sayansi na teknolojia ni nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo ya kiuchumi, endepo kutatumika teknolojia rahisi ambayo itawawezesha wananchi wengi hususan maeneo ya vijijini kupata maendeleo kwa wakati.

Hata hivyo, alisema serikali imejenga mifumo na miundombinu pamoja na kutenga bajeti kubwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wananchi, kufahamu umuhimu wa utafiti unaofanywa na watafiti nchini. Alisema sera ya serikali ya mwaka 2015/2025, ni kufikia uchumi wa viwanda na sera hiyo, inaendana na sera ya kimataifa ya maendeleo endelevu.

"Mwaka 2017, nilikuja hapa Nelson Mandela, kuzindua vituo vinne vya umahiri vya sayansi na teknolojia vya elimu ya juu, ambavyo vilianzishwa na serikali kupitia mkopo nafuu kutoka benki ya dunia kwa lengo la kuboresha utafiti ambao utaleta matokeo chanya kwa wananchi," alisema Ndalichako na kuongeza:

"Furaha yangu baada ya miaka miwili kupita vituo vinne nilivyovizindua vimeanza kazi ya kuboresha utafiti na kuleta matunda ya nchi."

Alisema lengo la serikali kufikia uchumi wa viwanda, hivyo watatoa elimu na kuendeleza ujuzi kwa wananchi, ili wawe na uwezo wa kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha kwa kutumia teknolojia rahisi na ya kisasa.

Dk. Yusufu Jande, Kiongozi Msaidizi kutoka Kituo cha Umahiri cha Miundombinu ya Maji na Nishati Endelevu cha Wise- Future, alisema nchi 11, zimeshiriki katika mkutano huo wa kimataifa ni Korea Kusini, Nigeria, Namibia, Indonesia, Ufaransa, Uingereza, Tanzania, Kenya na Uganda.

Alisema lengo la kuwakutanisha watafiti kutoka nchi hizo ni kujadiliana namna ya kuvumbua mambo kupitia kazi za utafiti wanaofanya.

Aidha, alisema kuwa kupitia utafiti wanaofanya wamegundua teknolojia rahisi ya kuondoa madini ya floride, vijidudu na chumvi chumvi katika maji.

Alieleza kuwa kwa mujibu wa utafiti uliofanyika awali, kiasi cha chumvi katika maji kinatakiwa kuwa miligramu 500, kwa lita moja ya maji.

Mkuu wa Chuo cha Nelson Mandela, Prof. Emmanuel Luoga, alisema chuo hicho, kimejikita zaidi katika utafiti wa nishati endelevu ya jua na maji kwa kushirikiana na nchi washiriki wa mkutano pamoja na vituo vya utafiti vya iTEC.

# Wapewa mwezi kuzitumia EFD

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MANYARA

WAFANYABIASHARA wa Mkoa wa Manyara, wenye biashara ghafi kuanzia Sh. milioni 14 na zaidi ambao hawajafunga mashine za kielektroniki za kutoa risiti (EFD), wamepewa mwezi mmoja ili kuwa nazo au watafikishwa mahakamani na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Meneja wa TRA wa Mkoa wa Manyara, John Mwigura, akizungumza juzi na wadau wa maendeleo wa mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, alisema watawafikisha mahakamani wafanyabiashara hao wasiokuwa na EFD.

Mwigura alisema wafanyabiashara wote watakaokiuka agizo hilo, watafikishwa mahakamani kwani ndicho chombo cha kutoa haki, hivyo hayupo tayari kuona watu wanavunja sheria bila kuchukuliwa hatua. Alisema mfanyabiashara mwenye mauzo ghafi ya Sh. milioni 14 siyo mtaji yaani biashara inayoingiza faida Sh. 38,000 kwa siku anapaswa kuwa na mashine hizo.

Alisema wametoa elimu kwa wafanyabiashara hao juu ya kufunga mashine ya EFD, lakini wapo baadhi yao hawakutekeleza hilo zaidi ya kufikishwa mahakamani kwani watakuwa wameshindwa kutekeleza wajibu wao.

"Kuna baadhi ya wafanyabiashara wana mashine mbili za kutoa risiti, wakikuona umevaa suti hawakufahamu wanatoa risiti ya EFD, lakini kama hawajakutilia shaka wanatoa risiti zilizoandikwa kwa mkono hawa tukiwabaini tutawapeleka mahakamani," alisema Mwigura.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema wafanyabiashara wanapaswa kufanya shughuli zao kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni ili waweze kufanikiwa.

"Serikali imekuwa ikiwaasa kila wakati wafanyabiashara juu ya risiti," alisema Chaula.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alisema kuna baadhi ya risiti ambazo zinatambuliwa kuwa hazipo katika mfumo wa EFD, hivyo wafanyabiashara wasitumie kigezo hicho kwa kutoweka mashine za EFD.

Mmoja kati ya wafanyabiashara hao Magdalena John alisema elimu inapaswa kuendelea kutolewa kwa wafanyabiashara hao ili kujua umuhimu wa kulipia mashine za EFD.

## Karoti yaleta neema Siha

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MAKULI wanaofanya shughuli za kupakia, kushusha na kuosha karoti katika Wilaya ya Siha, sasa watapata ulaji baada ya Baraza la Maendeleo ya Kata ya Indumeti (BMK), kupitisha uamuzi wa kuanzishwa mradi wa kusafisha zao hilo, kabla ya kusafirishwa kwenda kwenye masoko ya Dar es Salaam na Zanzibar.

Akizungumza na wakazi wa Kata ya Indumeti jana, Diwani wa Kata hiyo, Jackson Rabo, alisema katika kupambana na tatizo la ajira, wameamua kuanzisha mradi huo utakaoajiri zaidi ya vijana 400.

"Karoti zote zinazozalishwa katika Wilaya ya Siha na hasa ukanda wa juu wa West Kilimanjaro, zote hazioshewi hapa zinapelekwa kuoshwa Dar es Salaam na halmashauri yetu haifaidiki na kodi inayotokana na kazi hiyo, lakini pia watu wetu wanakosa ajira. Tumesema hapana, zitaoshwa Siha, ndio ziende sokoni Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza na Nairobi," alisema.

Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro zilizobuni miradi ya uoshaji wa karoti kama chanzo cha mapato ya ndani, kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya mkoa ni eneo la maili sita katika Wilaya ya Hai, Bonite iliyopo Manispaa ya Moshi na TPC katika eneo la Moshi Vijijini.

Makuli katika eneo la Bonite, Kata ya Shirimatunda Manispaa ya Moshi ambao hupokea karoti kutoka mashamba ya West Kilimanjaro, hutoza gharama za uoshaji wa karoti kwa gunia moja Sh. 4,000. Wakati malori ya mizigo aina ya Fusso ambayo hukodiwa na wafanyabiashara kwa ajili ya kubeba karoti kupeleka sokoni yakitokea Wilaya ya Siha, kwa siku moja ni zaidi 80.

Faida ya kula karoti ni kusaidia kuondoa sumu na taka mwilini, lakini pia inaondoa mafuta yasiyotakiwa katika ini (cholesterol) na kuliwezesha lifanye kazi vizuri na kusafisha njia ya haja kubwa na kusaidia kupata choo vizuri.

Pia kusaidia kuzuia ugonjwa wa kiharusi, kutibu tatizo la kupoteza kumbukumbu kwa wazee, kusaidia kuimarisha macho kuona vizuri mfano tatizo la kutoona vizuri usiku, kuondoa matatizo ya mzio (allergy) kwenye macho, mfano macho kuwasha sababu ya vumbi.

Inaelezwa na wataalamu wa afya kwamba ulaji wa karoti sita kwa wiki husaidia kutopata kiharusi.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, Juma Jani, alisema ubunifu utaisaidia halmashauri kuongeza mapato yake na kwamba wazo la kuanzishwa mradi huo lilishafikishwa kwenye baraza hilo, na ikaagizwa wataalamu kwenda eneo hilo na kufanya tathmini kuhusu gharama ya ujenzi wa miundombinu ya mradi huo. lakini hawajapata mrejesho wake.

# Wataalamu wa lishe watoa angalizo watoto kutumia vilevi

**Na Godfrey Mushi**, HAI

WATAALAMU wa lishe, wametoa tahadhari kuhusu matumizi mabaya ya vilevi kama pombe kwa watoto wadogo, kuwa yanaweza kusababisha mtoto kutoona mbali na hata kupatwa na matatizo ya akili.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Silvania Ignace, alisema jamii inapaswa kuachana na hulka hiyo ya kuwaonjesha pombe watoto wadogo, lakini pia kufahamu pombe inaweza kuleta madhara makubwa kwa mtoto, bila mzazi kuyaona madhara yake kwa haraka. "Yako mambo yanatisha huko vijijini na hasa katika Wilaya ya Hai, mtu anampa mtoto pombe na bado anaona ni sawa. Yako madhara ya kiafya yanayoweza kumpata mtoto kama kupata uoni hafifu au matatizo ya akili baadaye, tunatoa rai kwa wazazi kuacha kufanya hivyo," alionya ofisa huyo.

Kutokana na hulka inayojengwa na baadhi ya wananchi vijijini, ofisa lishe huyo ameziomba serikali za vijiji na mitaa, kutunga sheria ndogo zitakazozuia ulevi kwa watoto na kwa kila mwananchi atayebainika kunywa pombe kupita kiasi na kumnywesha mwanawe ambaye ana umri mdogo chini ya miaka 18.

Katika maeneo ya vijijini wilayani Hai, kumekuwapo na tatizo la baadhi ya wazazi na walezi kunywa pombe kupitiliza na wengine kuwashirikisha watoto wenye umri chini ya miaka 18.

"Hali kama hiyo, ndiyo ambayo husababisha watu kushindwa kutunza familia zao vizuri na kuchangia katika umaskini kwenye jamii. Tabia hiyo inachangiwa na mila zilizopo wilayani hapa, ambapo watu kunywa pombe na kulewa kupita kiasi ni suala la kawaida," alieleza.

Kuhusu matunzo kwa wanawake wanaonyonyesha, ofisa lishe huyo, alisema kuwa ushiriki wa kinababa kwenye malezi na lishe ya mtoto ni kuhakikisha kuwa kina mama wanapata chakula bora kwa ajili ya kutengeneza maziwa ya mama kunyonyesha.

Alieleza kuwa, pia mama anayenyonyesha anatakiwa kupunguziwa majukumu pamoja na maudhi kwenye jamii ili aweze kuwa na muda wa kumhudumia mtoto. Badala yake, ameshauri wanawake kuwanyonyesha watoto maziwa ya mama pekee bila kuwapa maji, wala chakula kwa kipindi cha miezi 6 kwani kwa kufanya hivyo kunawasaidia watoto kuwa na afya njema.



Msindikaji wa Bidhaa za Lishe, Dorice Assenga, akifafanua juu ya virutubisho na viini lishe vinavyopatikana katika unga wa lishe kwa Mratibu wa Shirika lisilokuwa la Kiserikali la INFOY, Laurent Sabuni, katika maonyesho ya bidhaa za lishe jijini Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Hamasa kubwa kwa wakulima kuchangamkia fursa yaingia Hai

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

HAMASA kubwa ya wakulima kuchangamkia fursa ya uzalishaji wa malighafi za viwandani hasa mazao ambayo hayastawishwi kwa wingi nchini kama 'fiwi' imehamia katika Wilaya ya Mwanga.

Fiwi ni aina fulani ya maharage jamii ya kunde, ambayo hulimwa katika maeneo yenye ukame, kwa sababu zao hilo hustahimili sana ukame kwa muda mrefu.

Akizungumzia juhudi zinazofanyika hivi sasa kuhamasisha kilimo hicho kutokana na sehemu kubwa ya eneo la tambarare kukabiliwa na ukame, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Zefrin Lubuva, ameeleza kuwa zao la fiwi, utafiti wake umeonyesha linastahimili ukame na lina gharama ndogo za uzalishaji, ikilinganishwa na mazao mengine.

"Zao hili lina mafanikio makubwa kiuchumi na soko kubwa liko nchi za Kenya na India ambako wananchi wake wengi hupenda kutumia kama chakula, lakini pia Kenya hupenda kutengenezea biskuti," alisema na kuongeza:

"Ndio maana mazao makuu yanayolimwa wilayani Mwanga ni fiwi ikifuatiwa na mahindi, mpunga, ndizi, kahawa, matunda na mboga."

Kwa mujibu wa Lubuva, halmashauri hiyo mpaka sasa imetenga hekta 750 za ardhi ambayo inatoa fursa ya uwekezaji wa shughuli za kilimo.

Aidha, alisema ardhi hiyo imetengwa katika kata za Kirya, Kileo na Kivulini. Katika Kata ya Kirya peke yake kuna jumla ya hekta 900 za umwagiliaji ambapo hadi sasa hekta 150 tu ndizo ambazo zinatumika.

"Wawekezaji wanakaribishwa kuja kuendeleza hekta zilizobaki ambazo zina rutuba nzuri na hali ya hewa nzuri inayoruhusu kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo hili. Eneo lingine ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni Kijiji cha Kileo chenye jumla ya hekta 2,400 ambazo zinafaa kulimwa kwa kipindi chote cha mwaka," alisisitiza mkurugenzi huyo.

Kijiji cha Kivulini chenyewe, kina jumla ya hekta 1,050 ambapo hekta zinazotumika kwa kilimo ni 400 tu.

Wakati katika Tarafa ya Jipe Ndea, nayo imetengwa kama maeneo yenye ardhi ya kutosha inayofaa kwa kilimo. Mazao yanayostawi ni alizeti, mtama, uwele, miwa, mahindi, maharage, ngwara, korosho, mboga, matunda na mpunga.

# ama

ALHAMISI AGOSTI 15, 2019

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 18

**Wizara yaanzisha operesheni TB kwa magereza 15 nchini**



Ukurasa 15

Ukeketaji kutoka zama za wasichana, hadi kufichwa



Ukurasa 14

**Ijue tiba ya kidonda kwa kompyuta**



**ULINGO WA SADC**

# Tanzania imekwezwa kisiwa cha utalii wa maajabu ya matibabu

Ukurasa 16

# Ijue tiba ya kidonda kwa kompyuta

**LONDON,** Uingereza

MAENDELEO duniani yamepiga hatua mpya, watafiti wa Chuo Kikuu cha Heriot-Watt, nchini hapa wamebuni kifaa cha kutibu kidonda bila ya ukaguzi wa macho na kugusa kwa mkono uliozoeleka.

Kiongozi wa Utafiti, Profesa Michael Crichton, anasema " Tunaweka kifaa cha kuhisi juu ya mishipa ya mwili jirani na jeraha. Tunaweza kupata kipimo (cha kompyuta) na kujua hasa nini kinachotokea.

"Kama tunaweza kufanya kila baada ya muda fulani, ina maana inatuambia kinachoendelea kwa namna moja au nyingine. Lakini jeraha la mwili likoje? Kabla hawajajua, ni budi watafiti wachunguze tabia ya ngozi inavyokuwa pindi inakatwa."

Anaeleza kuwa tabia ya ngozi ya binadamu, hata iliyokomaa ya mtu mzima inakuwa na tabia ya kuathirika kwa namna fulani, hata ikiguswa kidogo, kuna baadhi ya madhara watu hufikia kukatwa mguu, pale tiba inaposhindikana.

Ni sehemu ya mradi wa miaka miwili kufanya uvumbuzi unaohusu afya ya jamii, ukimjumuisha mtaalamu bingwa wa masuala ya hisia za ngozi, Dk. Jenna Cash, kutoka Chuo Kikuu cha Edinburgh, Uingereza.



Mtaalamu tiba akifanyia kazi taarifa ya kidonda zinazoonekana katika kompyuta. **PICHA: MTANDAO.**

MAZINGIRA

# Hatimaye dawa mpya inatibu ebola



Kambi ya matibabu ya ebola nchini DRC. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

NCHINI Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambako ni waathirika wakuu hadi sasa wa maradhi ya ebola wameshawapoteza wenzao, jumla yao 1,800. Imekuwa janga la dunia.

Sasa kuna taarifa mpya kwamba, majaribio ya watafiti yanaonyesha kuwapo dawa mpya zinazoonyesha kutibika kwa maradhi hayo, baada ya dawa za aina mbili kujaribiwa kwa wagonjwa wanne.

Wanasayansi kupitia utafiti wao, wanasema uwezo wake wa tiba ni sawa na kiwango cha asilimia 90 tena kwa wale walioathirika zaidi.

Maofisa afya wanaofanya kazi ya kutibu, walitamka Jumanne iliyopita kuwa wagonjwa wawili waliondolewa katika kituo cha tiba cha mjini Goma, kwenda kujiunga na familia yao.

Taasisi ya Marekani inayohusika na Magonjwa ya Aleji na Maambukizi (NIAID), iliyokuwa inadhamini majaribio hayo ya kitafiti imeyapokea kwa mikono miwili kwamba, 'ni habari njema.'

Tayari dawa hizo zimepewa majina ya awali ambazoi ni 'REGN-EB3' na 'mAb114' ikiwa na kazi mwilini ya kuvunja virusi vinavyoshambulia mwili na kulainisha uwezo wa madhara yake dhidi ya chembe hai za mwanadamu mgonjwa.

> **Hatuifuti ebola, lakini ni lazima tuweze kudhibiti milipuko na kuiweka katika ngazi ya mataifa na mikoa.**



Huduma ya chanjo dhidi ya ebola ikiendelea nchini DRC.

Mkurugenzi wa NIAID, Dk. Anthony Fauci, anaieleza kuwa ni dawa ya kwanza inayoonyesha majibu ya uhakika katika tiba hiyo ya ebola, mzizi wake wamejifunza kutoka vimelea vya aliyepona maradhi hayo.

Kuna dawa zingine mbili zilizobuniwa ambazo baada ya majaribio zimewekwa kando, kutokana na kuonyesha matokeo hasi katika majaribio ya kitafiti.

Ni majaribio yaliyofanywa chini ya uratibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Novemba mwaka jana. Kati ya kipindi hicho na sasa, kunaelezwa kuwapo majaribio wastani wa wagonjwa 700, kati yake 499 majibu yake yameshapatikana.

Msisitizo wa mtafiti wa maradhi hayo, Sabue Mulangu, ni kwamba iwapo kundi la wanajamii waliopatwa na maradhi hayo wakatibiwa mapema, basi wana nafasi ya kupona kwa kiwango anachokitaja kuwa 'asilimia 90.'

Mkurugenzi wa asasi ya kijamii ya Welcome Trust Global Health Charity Hailing, Jeremy Farrar, anaeleza furaha yake ya dalili za dunia kunusuriwa, akitanguliza imani kwamba 'ebola inazuilika.'

"Hatuifuti ebola, lakini ni lazima tuweze kudhibiti milipuko na kuiweka katika katika ngazi ya mataifa na mikoa," anasema Farrar.

Dk. Fauci naye anafafanua: "Yale matarajio kwamba dawa bora zinatoka Marekani, inawafanya wagonjwa wajisikie vizuri."

Ushauri wake ni kwamba ngazi bora ya mafanikio kiafya ni kuwa na chanjo inayofaa, kuwajengea wananchi kinga sahihi na kuifanya sawa maradhi yanakingika.

WHO ilishasema kwamba kinga ambazo zinatumika hivi sasa, hata kabla ya kupewa leseni rasmi zimeshaonyesha ubora mkubwa

Msukosuko wa ugonjwa nchini DRC iliopo sasa, ulianza mwezi Agosti mwaka jana na inaelezwa kuwa mkubwa zaidi, kati ya milipuko 10 iliyotokea tangu mwaka 1976.

Mnamo mwezi uliopita, WHO ilitangaza ebola kuwa janga la kimataifa kiafya, huku kukishuhudiwa ugumu mkubwa katika ufanikishaji udhibiti wake.

Hata hivyo, katika mazingira ya DRC Taifa linalobakiwa na majanga ya kiusalama, baadhi ya madaktari raia wa DRC waliwekwa mikononi mwa sheria kwa kuhusishwa na vifo vya madaktari waajiriwa wa WHO.

Pia, kuna tukio la kuwapo miundombinu takriban 200 ya kutibu maradhi hayo yalishambuliwa, hali iliyovuruga matibabu na kinga dhidi yake. Katika tukio mojawapo, wanafamilia waliokuwa wanashuhudia mazishi ya ndugu yao aliyekufa kwa ebola, waliamua kuuvamia.

Shida nyingine katika kukabili ebola nchini DRC ni mwaka jana iliripoitiwa katika jarida la afya kwamba, kumekuwapo upotoshaji kuhusiana na maradhi hayo.

AFYA

# Ukeketaji kutoka zama za wasichana, hadi kufichwa kwa watoto wachanga

• Dk. Ngululile aapa 'kufa'na wahalifu

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya Serikali kubaini kuwapo mbinu mbalimbali zinazotumiwa na madaktari wasio na maadili, pia wakunga, sasa kuna agizo la kuwakagua watoto wachanga kubaini kama wamekeketa au, ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, anasema kama watoto wamefanyiwa ukatili huo, wahusika wanapaswa kuchukuliwa hatua.

Ni msimamo aliyoutoa Dk. Ndugulile mwaka jana, alipozungumza katika mdahalo wa wahariri wa vyombo vya habari uliofanyika jijini Dar es Salaam, kuhusiana masuala ya ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni, kipindi kuelekea kilele cha Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike

Mdahalo huo ulijikita katika namna bora ya kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto wa kike, ambao wanakumbana na madhila hayo kufikia ngazi ya watoto wachanga.

"Jamii baada ya kubadili mwenendo wa ukeketaji, Serikali imebaini mbinu hizo na inawataka madaktari wote nchini kufanya uchunguzi kwa watoto wote wachanga, ili kubaini kama watoto hao wamefanyiwa ukatili kwa kukeketwa, ili wahusika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria," anasema Dk. Ndugulile.

Kimsingi, ukeketaji ni tendo linalopingwa duniani kote, kiafya, kisheria na kijamiii na ndio maana imetengewa siku maalum ya maadhimisho, ikiwa na kaulimbu mbalimbali zenye lengo la kutokomeza ukatili huo dhidi ya watoto, wasichana na wanawake.

Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji kwa mwaka huu, ambayo huadhimishwa kila Februari 6 na mwaka huu, ilikuwa na kaulimbiu: 'Acha mila zenye madhara; Tokomeza ukeketaji'. Februari ya kila mwaka, Tanzania huungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hiyo, baada ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kuidhinisha rasmi upingaji wa ukeketaji duniani na kuitenga rasmi tarehe hiyo, mwaka 2003.

Inaelezwa kuwa, tatizo la ukeketaji limeendelea kuwapo kwa takribani karne 21. Kwanini hivyo? Kuna sababu nyingi zinazotajwa kuchangia kutokea kwake, mojawapo ni jamii kutawaliwa na mfumo dume na mila kandamizi kwa wanawake.

Jamii kumvusha mtoto wa kike rika kutoka kuwa usichana na kuwa mwanamke kamili kupitia kumwozesha, ni sababu nyingine ya ongezeko la ndoa za utotoni, huku wasichana wakikosa haki zao za msingi kama vile elimu.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akiwa na wasichana waliookolewa kutoka vitendo vya ukeketaji, sasa wanapatiwa mafunzo ya ujasiliamali na Kituo cha Mtandao wa Kupambana na Ukeketaji Orkesumet Simanjiro mkoani Manyara. **PICHA: KITENGO MAWASILIANO WAMJW**

> **Shirika la Afya Duniani (WHO), iliainisha madhara ya muda mfupi na mrefu yatokanayo na ukeketaji. Hapo kuna wahusika wanapoteza damu nyingi na wanaofariki dunia.**




Wasichana wakishiriki kampeni za kupinga ukeketaji kitaifa.

Umaskini unaotajwa kuchangia jamii nyingi kubaki kwenye kitanzi cha mila ya ukeketaji kwa vile wazazi wa mtoto husika hutegemea kupata kipato kwa kuwaozesha mabinti baada ya kuwakeketa.

**SUMU YAKE**

Shirika la Afya Duniani (WHO), iliainisha madhara ya muda mfupi na mrefu yatokanayo na ukeketaji. Hapo kuna wahusika wanapoteza damu nyingi na wanaofariki dunia.

Mengine yanatajwa kuwa mhusika kukabiliwa na maumivu makali ya mwili, mshituko, maambukizi ya magonjwa kutokana na kutumika vifaa mtu zaidi ya mmoja, pia si safi na salama.

Vilevile WHO inaeleza, ukeketaji unadaiwa kusababisha maambukizi ya magonjwa katika njia ya haja ndogo; homa ya manjano (Hepatitis B); matatizo wakati wa kujifungua; kutofurahia tendo la ndoa; na maumivu ya kisaikolojia.

Shirika hilo linataja madhara ya muda mrefu kuwa ni tabu ya kisaikolojia isiyoisha, kovu la kudumu sehemu za siri, fistula, kupata shida wakati wa kujifungua na chanzo cha ugumba kwa baadhi ya kinamama.

Hata hivyo, nchini Serikali imeendelea kuboresha sheria na sera mbalimbali kuweka wigo mkubwa zaidi wa kuadhibu wale wote wanaofanya vitendo vya ukeketaji.

Serikali inasema, mabadiliko ya Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, yamelenga kupanua adhabu na kutengeneza mnyororo mpana wa washiriki, huku kukiwapo maboresho ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu (2002), inayopanua uwanda wa adhabu unaobaini kipimo cha ushiriki wa mtuhumiwa katika ukeketaji.

**NCHINI KULIVYO**

Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu mwaka (LHRC) 2017, inaeleza kwamba, bado kuna mikoa kadhaa nchini inaendelea kuendekeza ukatili huo dhidi ya mtoto wa kike.

Vilevile ripoti ya Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey (TDHS) ya mwaka 2015 hadi 2016 inataja mikoa hiyo, Manyara ikiwa kileleni, ikifuatiwa na Dodoma; Arusha; Mara na mwisho Singida.

Mangariba wanatajwa kuwa wahusika wakuu na robo ya wasichana wote wanakeketwa katika umri kabla ya mwaka na wengine ni chini ya miaka 13 na zaidi.

Aidha, ripoti hiyo inasema wasichana wanaozaliwa au kulelewa na mama aliyekeketwa, kunaonekana uhusiano nao hukeketwa, ikihisiwa ni mwenendo wa jamii yake.

Pia, kuna sura ya pili binafsi, asilimia 95 ya wanawake waliokeketwa, daima hawavitaki vitendo hivyo.

AFYA

ULINGO WA SADC

# Tanzania imekwezwa kisiwa cha utalii wa maajabu ya matibabu

## • MOI, Taasisi Moyo, Muhimbili… • Viwanda 80 vya dawa viko njiani



Siku ulipofanyika uzinduzi wa kampasi ya taaluma ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), iitwayo Mloganzila, jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Beatrice Moses**

UHAKIKA wa huduma ya matibabu ni jambo linalotia moyo katika jamii yoyote, japo kunaweza kuwapo changamoto za kumudu gharama, hasa inapomlazimu kwenda kutibiwa nje ya nchi.

Kwa miaka kadhaa, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi ambazo zimekuwa zikipeleka wagonjwa wanaobainika kuwa matibabu yao hayapatikani nchini.

Mwezi Oktoba wa mwaka 2017, serikali ilitangaza kwamba haitatoa tena vibali vya wagonjwa kwenda nje ya nchi kutibiwa. Ni hatua iliyofuata baada ya kuboreshwa kiwango kikubwa huduma za afya nchini.

Ni kauli kutoka kwa aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Mpoki Ulisubisya, baada ya kupokea timu ya wataalamu,wakiwamo madaktari bingwa wa fani mbalimbali kutoka nchini Cuba.

Wiki iliyopita, serikali ilieleza kuwa inatarajiwa kuongeza kupokea idadi ya wagonjwa watakaoletwa kutibiwa nchini kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

### UMMY AANIKA KULIKOFIKIWA

Ni kauli ya Waziri wa Afya,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Ummy Mwalimu, alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dare es Saalam, kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.

Waziri Ummy anasema, kupitia maonyesho hayo sekta ya afya imepata fursa kuonyesha kuwa Tanzania sasa inakuwa nchi ya utalii wa kimatibabu, inatokana na huduma za kisasa zinazotolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

> **“Tunashukuru kwamba tumepata zabuni hii wakati Rais John Magufuli anakabidhiwa uenyekiti wa SADC, hivyo tunaamini kwamba atatusaidia kutuongoza vizuri hatimaye tutafanikisha kazi tuliyopewa.**



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisikia ufafanuzi kutoka kwa daktari bingwa wa MOI, William Mugisha, kwenye Viwanja vya Maonyesho SADC, jijini Dar es Salaam.

Anasema, ni hatua inayotokana na serikali kufanikiwa kuboresha na kuanzisha huduma za kisasa, ikiwamo upandikizaji figo na vifaa vya kusikia kwa watoto na kutibu kwa kutumia kifaa cha radiolojia' unaofanywa kwenye Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

Waziri Ummy, anasema huduma hizo awali hazikupatikana nchini hata ndani ya wanachama wa SADC, isipokuwa nchi ya Afrika Kusini pekee inayotoa huduma za upandikizaji figo, jambo linaloisogeza Tanzania katika frusa kupokea wagonjwa kutoka wanachama wa SADC.



Wataalamu kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, wakitoa maelezo kuhusu huduma zao,katika Viwanja vya Maonyesho SADC, jijini Dar es Salaam.

Anaieleza kuwa ni hatua inayowajengea mazingira wanajumuiya wa SADC, kuandaa mbadala wa wagonjwa wao kutibiwa ndani ya SADC ambako ni Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH)

Ummy anaeleza imani yake kwamba, mkutano wa SADC utaongeza idadi ya wagonjwa wanaopokelewa kutoka jumuiya hiyo, ambayo ilikuwa ni wagonjwa 24 kila mwezi, kutoka nchi za SADC, hususan Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Comoro na Malawi.

Waziri Ummy anasema, kupitia Mkutano wa SADC unaoendelea nchini, kuna mengi yanayohusu afya Tanzania itanufaika nayo.

Wakati wa maonyesho ya Viwanda ya SADC wiki iliyopita, Waziri Ummy alitembelea mabanda ya sekta ya afya, ikiwamo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, ambazo aliungana nazo mkono kuwa na huduma za tiba ya kisasa zinazotolewa katika taasisi hizo.

“Katika maeneo haya ya maonyesho, tumejipanga vizuri kutoa huduma ya tiba ya dharura. Kuna 'ambulance (magari ya wagonjwa) 22, pamoja na vyumba maalum vilivyotengwa kwa huduma hizo kwa mtu atakayepata matatizo ya kiafya katika mkutano huu,” anasema.

Pia anataja eneo la tatu, ni utoaji wa zabuni na kufafanua Tanzania itanufaika na ununuzi wa pamoja wa dawa na vifaa tiba kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ambao inasaidia kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa kwa nchi hizo.

### MSD NA SADC

Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD), Laurean Bwanakunu, anasema kuna Watanzania kadhaa wameonyesha nia ya kujenga viwanda vya dawa nchini, MSD ikiamini kwamba mwakani vinaweza kukamilika na kuanza kufanya kazi.

“Tulitangaza zabuni kimataifa, tumepokea maombi ya viwanda vya dawa 80. Shughuli inayofanyika sasa ni kuchambua zabuni hizo, ikiwamo kuangalia bei na kujiridhisha na uwezo wao,” anasema

Anafafanua kuwa, waombaji hao wanatoka katika nchi 30, India ndiyo inaongoza kwa kuwa na viwanda vingi vilivyoomba kuuza dawa na vifaa tiba, ikilinganishwa na nchi nyingine.

Mkurugenzi huyo anasema, baada ya kumalizika kwa mkutano wa wakuu wa nchi SADC, wanatarajia kutuma taarifa za matokeo ya zabuni kwa nchi wananchama, ili zijipange katika namna ya kushughulikia usajili.

Anasema, malengo ya kufanya uamuzi huo wa pamoja, ni kuongeza uwezo wa nchi za SADC kuwa na viwanda, kwani hata kunakokuwapo nchi zinazoonekana kuwa ni ndogo, nazo zinaweza kualika wawekezaji kupitia mgongo wa jumuiya hiyo.

Pia, SADC inalenga kuhakikisha kuwa bei ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba inapungua kwa nchi zote wanachama zinapofanya ununuzi wa mahitaji pamoja.

“Mnapovuta mahitaji yetu kwa pamoja kama nchi 16 inanufaisha hata nchi ndogo ndogo, unapoleta mahitaji ya pamoja gharama zinapungua. Kuna jumla ya nchi kama 30 kama Tanzania tuna mkataba na viwanda 151 kutoka katika nchi 41,

“Tunashukuru kwamba tumepata zabuni hii wakati Rais John Magufuli anakabidhiwa uenyekiti wa SADC, hivyo tunaamini kwamba atatusaidia kutuongoza vizuri hatimaye tutafanikisha kazi tuliyopewa,” anaeleza Bwanakunu.

### MOI WALIVYONENA

Meneja Ustawi wa Jamii na Uhusiano, wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu (MOI), Almas Jumaa, anasema wamejitokeza kwenye maonyesho ya viwanda SADC ili kutangaza matitabu ya kisasa yanayotolewa nchini kupitia taasisi anakotumikia.

Jumaa anasema, wameiona fursa hiyo na kuamua kujitangaza kwa kuwa wanatambua kuna matibabu ambayo yanatolewa MOI hayapatikani kwenye nchi nyingine za SADC.

“Lengo la kuja hapa ni kuwafahamisha kuwa tuna upasuaji wa aina hiyo, ili walete wagonjwa kutoka kwenye nchi zao kutibiwa,” anasema.

Daktari wa MOI, William Mugisha, anabainisha kuwa kuna nchi sita tu ndiyo zinafanya upasuaji wa kikombe cha nyonga, ambazo kwa Afrika Mashariki ni mbili; Kenya na Tanzania.

Anasema ni miongoni mwa upasuaji mkubwa, ambao nchini kuna madaktari bingwa wanne, wataalam wa tiba hiyo.

Dk Mugisha anasema, pia kuna upasuaji wa nyonga bandia na magoti, ambao kwa upande wa magoti upasuaji unahusisha teknolojia ya kisasa ya kutolifumua badala yake kunatobolewa matundu matatu.

“Matundu siyo vidonda vikubwa, mgonjwa anapasuliwa matundu matatu; moja la kuingiza kifaa cha upasuaji; lingine kwa ajili ya kupitisha maji; la tatu la kamera iliyounganishwa kwenye kompyuta ambayo huwezesha daktari na mgonjwa kuona kila kinachofanyika ndani ya goti husika,” Dk Mugisha anasema

> **Shughuli inayofanyika sasa ni kuchambua zabuni hizo, ikiwamo kuangalia bei na kujiridhisha na uwezo wao.**

Anataja upasuaji wa kuziba mishipa ya damu inayovilia, upasuaji wa marudio wa magoti na nyonga bandia na upasuaji mpya wa ubongo kwa njia ya teknolojia ya kisasa, bila ya kufungua fuvu.

“Upasuaji huu hufanywa kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa upasuaji wa pua, ukihusisha kutoa vivimbe vilivyo sehemu ya mbele ya ubongo karibu na pua, vivimbe vinapitishwa sehemu ya pua na matibabu yanakuwa yamekamilika,” anasema

“Tangu tuanze upasuaji huo ni miaka miwili iliyopita, huu unahitaji ubobezi wa hali ya juu zaidi unaotegemea teknolojia mpya katika matibabu haya, ni tofauti na upasuaji wa ubongo ambao umefanyika MOI zaidi ya miaka 15 iliyopita,” Dk Mugisha anasema

---

# Wamcharukia Trump kubomoa sheria mazingira



Kipepeo; mmoja wa viumbe wanaolindwa na sheria ya mazingira. **PICHA: MTANDAO.**


**WASHINGTON DC,** Marekani

RAIS Donald Trump, amewaibukia wana-mazingira na harakati zake, akiwa na jipya kwamba ana mpango wa kuisuka upya sheria inayosimamia viumbe vilivyo hatarini, kwa kupunguza mlolongo wa kanuni zake.

Ni dhamira inayoelezwa kuwagusa wadau wengi wanaoitetea, wakiamini ni mabadiliko yaliyokuwa na miongozo mingi ya kusimamia sheria tajwa na kutoa ulinzi wa hali ya juu wa mazingira nchini humo.

Sheria hiyo iliyotungwa mwaka 1973, inatajwa kuwa na vipengele lukuki vinavyotetea mazingira kitaifa, ambayo Rais Trump, sasa hayahitaji

Katika mpango unaolengwa, unaelezwa vipengele vingi vya kimazingira vimekuwa vikwazo kwa mikakati ya kiuchumi katika nchi hiyo. Hata hivyo, wanamazingira wanamcharukia.



Donal Trump

Ni mpango uliotangazwa na timu ya maofisa wa sheria 10 wa serikali, wakiainisha Serikali inachonuia katika mageuzi hayo ya kisheria inayogusa na kulinda viumbe na mimea 1,600

Kwa mujibu wa mpango wa kisheria unaoundwa, unalenga kufanyika ndani ya siku 30 zijazo, maofisa wa serikali ya Rais Trump wakijivunia ni mara ya kwanza vigezo vya kiuchumi kujumuishwa katika mpango wa mageuzi ya kisheria wa namna hiyo

Waziri wa Mambo ya Ndani, David Bernhardt, anatetea mabadiliko kuwa na anachokidai kunufaisha 'kule kunakopaswa kuwapo zaidi.'

Mkurugenzi Msaaidizi wa taasisi ya US Fish and Wildlife Service, Gary Frazer, anajaribu kuhami akisema hakuna mabadiliko makubwa kama inavyojadiliwa au kufikiriwa na baadhi au hata jamii kwa jumla

Hata hivyo, wanaharakati wanalalamika kwamba, kupitia mageuzi hayo yanayotarajiwa kutoka serikalini, umma utarajie kutoweka kwa kasi viumbe vingi vya namna tofauti.

Noah Greenwald, ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Viumbe Vilivyo Hatarini, katika taarifa yake anayataja kuwa ni mabadiliko yanayotokomeza viumbe vilivyo hatarini, huku akiorodhesha baadhi yao.

Mwanaharakati mwingine, Drew Caputo, aliienda mbali kutishia kwenda mahakamani kuweka pingamizi. Anasema:

“Hizi juhudi za utawala huu kudhibiti utetezi wa viumbe wa vilivyo hatarini, una sura kuu mbili, moja (utawala) ni zawadi ya sekta ya viwanda, pili si halali.”

Sehemu kubwa ya wanaopinga wamekuwa wakitumia vipengele vya Ripoti ya Umoja wa Mataifa, vinavyotahadharisha kuwapo mamilioni ya mimea na wanyama, walio hatarini kutokana na nyendo za kibinadamu na mabadiliko ya hali ya hewa.

Seneta wa jimbo la New Mexico anayepeperusha bendera ya chama cha Democrat, Tom Udall, aliye mbali kufuata haki ya ukweli kisheria, kupitia sheria zao kongwe za mazingira anazozisifu kuwa na tija.

**Kwa mujibu wa mtandao.**

AFYA

# Wizara yaanzisha operesheni TB kwa magereza 15 nchini



Baadhi ya washiriki katika ufunguzi wa mafunzo ya kutathimini ugonjwa wa kifua kikuu magereza, mafunzo yaliyofanyika katika ukumbi wa Bwalo la Magereza, Ukonga, jijini Dar es Salaam.

**Na Yasmine Protace**

KIFUA Kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza, unaosababishwa na aina mbalimbali za bacteria, wanaojulikana kama 'Mycobacterium tuberculosis.'

Madaktari wanasema kifua kikuu cha kawaida kina asili ya kuathiri mapafu na hata sehemu zingine za mwili, usambazaji wake ukiwa ni kupitia hewa wakati mtu ama anapokohoa, kupiga chafya au mate yake yakiwa hewani.

Pia, kuna maambukizi mengine yanayotajwa hayana madhara kwa wakati husika, lakini baadaye pindi yanapokomaa, yanakuwa maambukizi kamili. Ni ugonjwa hatari ulio katika nafasi ya kuua wengi.

Katika kupambana nayo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ikitumia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma, imeanza kuchukua hatua ya kulikabili hilo magerezani, kupata picha kamili ya hali ya maambukizi, ili kutoa mbinu za kukabiliana nayo.

Kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza nchini, wizara inaanza kuchukua hatua ya kufuatilia na kutathimini hali ya huduma za kutokomeza kifua kikuu katika baadhi ya magereza yaliyoteuliwa kitaifa.

**KAMISHNA NGALAMA**

Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Jeshi la Magereza (CP) nchihi, Owesu Ngalama, akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo kwa maofisa wa jeshi hilo yanayofanyika kwenye Bwalo la Magereza, Ukonga jijini Dar es Salaam, Kamishna Ngalama, anasema hatua hiyo itaisaidia Jeshi la Magereza uhalisia ya kifua kikuu miongoni mwa wahusika wanaoshikiliwa.

> Mkakati wa kudhibiti kifua kikuu upo kwa wananchi wote, hivyo wanaendelea kutoa elimu kwa umma wa Watanzania, kila wanapoona dalili waende kwenye vituo vya afya kupata huduma.



Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Jeshi la Magereza, Owesu Ngalama (katikati), akiwa na Mganga Mkuu wa Magereza (kulia), SACP Dk. Hassan Mkwiche na kushoto ni Meneja Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu, Dk. Beatrice Mutayoba, kwenye mafunzo ya tathimini ya ugonjwa wa TB magerezani.

"Ugonjwa huu unaambukizwa kwa hewa, hivyo kwa tathimini hii, itasaidia kuleta utaalamu mkubwa kwa wataalamu wetu wa tiba walipo kwenye jeshi, kwani hali ya TB sio kubwa kwenye Magereza, ila lengo ni kuhakikisha hakuna maambukizi makubwa kwani wafungwa wanaingia na kutoka," anasema.

Anaishukuru wizara inayobeba dhamana ya kutetea afya ya umma, kwa kuendelea kushirikiana nao kwa muda mrefu, hususan kwenye huduma za afya, ikiwamo utoaji dawa, vifaa tiba na visivyo vya tiba, pamoja na masuala ya lishe kwenye vituo vya afya magerezani.

**MPANGO TB**

Meneja Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) kutoka Wizara ya Afya, Dk. Beatrice Mutayoba, anasema ugonjwa wa kifua kikuu, bado ina upana kwani kuna takribani watu 100,000 na 58,000 wanakadiriwa kuugua maradhi hayo kila mwaka. Pia, kunakadiriwa kuwapo vifo 27, 000 kila mwaka nchini.

Dk. Beatrice anasema, kifua kikuu kinaweza kumpata mtu yeyote, kwani maambukizi yake ni ya njia ya hewa, hivyo yapo makundi hatarishi zaidi katika mjumuiko, ikiwamo ya magerezani, hivyo Serikali inaendelea kuweka jitihada kuyafikia makundi hayo ili kutokomeza kifua kikuu, lengo kuu ni mwaka 2030.

"Kama nchi tumepiga hatua kubwa sana kutokomeza ugonjwa huu, hivyo tunaongeza juhudi zaidi kwenye makundi hatarishi, ikiwamo magereza, migodini, wavuvi ili kuwafikia kwa karibu na kuhakikisha tunapunguza maambukizi ndani ya magereza na maeneo haya," anasema.

Dk. Beatrice anasema, mkakati wa kudhibiti kifua kikuu upo kwa wananchi wote, hivyo wanaendelea kutoa elimu kwa umma wa Watanzania, kila wanapooona dalili waende kwenye vituo vya afya kupata huduma.

Anasistiza kwamba, huduma hizo zinapatikana katika sehemu hizo, kwani wizara husika inatoa dawa, vipimo na huduma za kifua kikuu bila ya malipo kwenye vituo vilivyoteuliwa kutoa huduma za afya.

Anasema, kwa upande wa magerezani unawekwa utaratibu wa kuwachunguza wanaoingia, pindi wakikutwa na kifua kikuu, waanaza matibabu kwani maradhi hayo yana kawaida mgonjwa anapoanza tiba ndani ya wiki mbili, hawezi kuwaambukiza wengine.

Dk. Beatrice anataja mikoa 15 itakayoanza wa ,mradi huo kuwa ni: Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

MAZINGIRA

# Maelfu Rorya walivyohamishwa kutoka adha maji hadi neema

- Wanafunzi na wanandoa...kabla alfajiri wasaka
- Viongozi kijiji wakiri kupumua na lundo la kesi
- Wanakijiji kutunza vyanzo, DC awanya wafugaji

**Na Anthony Gervas,** Rorya

JUMLA ya wakazi 9,407 wa vijiji vya Bitiryo na Baraki wilyani Rorya Mkoa wa Mara, sasa hawako tena katika utaratibu wa kujihimu usiku wa manane, kwenda kuvizia maji porini. Ni adha inayoangukia kwenye historia sasa.

Wahisani wameligeuza hilo kwenye uhuru mpya, sasa wasichana wanawahi shuleni, kinamama wameanza kufanya shughuli mbalimbali za kizalishaji, badala ya kutekwa na hofu ya upatikanaji maji, sasa wamejawa na furaha tele.

Ni matunda ya kazi iliyokamilika mwezi uliopita, iliyofanywa na asasi isiyo ya kiserikali ya Grain to Grow Foundation (GGF), jukumu ikigharimu fedha kiasi cha Sh. milioni 39.

Maji safi na salama katika kijiji cha Bitiryo, yanaelezwa yatasaidia kuchimba kisima kirefu chenye uwezo wa kuzalisha lita 1,582 kwa saa,wakati kijiji cha Baraki kimepata kisima chenye uwezo wa kuzalisha lita 3,270 kwa saa.



Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la GGF, Amillen Saria, akisukuma maji baada ya kuzindua mradi wa maji katika Kata ya Baraki. **ICHA ZOTE: ATHONY GERVAS.**

**KIJIJINI BARAKI.**

Baraki, ni miongoni mwa vijiji vitatu vilivyoko katika Kata ya Baraki wilayani Rorya, chenye jumla ya vitongoji sita. Ni kijiji chenye jumla ya vyanzo vitano vya mapato, ambavyo ni Ziwa Victoria, visima vya asili vinne, bwawa moja la maji, lambo na kisima kimoja kirefu cha kusukuma maji, walichosaidiwa na GGF.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Baraki, Emmanuel Nyamaraga, anasema mradi huo umewaondolea mateso kinamama kuamka usiku kwenda kuteka maji katika visima vya asili porini.

"Mradi huo wa majisafi na salama, umekuwa ni mkombozi wetu wanakijiji wa Baraki, kwani tuliteseka kwa miaka mingi isiyokuwa na simulizi halisi. Pengine shida hiyo ya maji imesababisha hata kuvunjika kwa ndoa nyingi, kuwepo migogoro na mifarakano ya familia,"| anasema Nyamaraga.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Baraki, Anipha Misana, anarejea historia kwamba kiliwahi kuwa na mradi wa maji bomba katika Kijiji cha Kyamweme, ambao kwa sasa haufanyi kazi, kwa sababu ya miundombinu duni.

Kijiji cha Kyamwame, kiliwahi kuwa na mradi wa maji bomba, lakini kwa sasa haufanyi kazi, kutokana na miundombinu kuwa mibovu," anasema Anipha Misana.

Mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Waningo, kijiji cha Bitiryo, Veronica Mwita, akiwa mwathirika, anaelekeza pongezi kwa shirika la GGF akiuleza mradi huo wa maji ya visima, ni mkombozi kwake, kwani kabla ya hapo alilazimika kufuata maji katika visima vya asili ambako ni umbali wa zaidi ya kilomita nne.

> **"Mradi huo wa majisafi na salama, umekuwa ni mkombozi wetu wanakijiji wa Baraki, kwani tuliteseka kwa miaka mingi isiyokuwa na simulizi halisi.**

Kwa mujibu wa binti huyo, ni safari iliyomkwaza kitaaluma, ashindwe kupata muda wa kujisomea, tofauti na sasa anaongeza:

"Nilikuwa nalazimika kutembea kwa miguu kufuata maji kwenye visima vya asili, umbali mrefu zaidi ya kilomita nne nikitumia zaidi ya saa moja na nusu kutembea kwa miguu na baiskeli ni takribani saa moja"

**HALMASHAURI RORYA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Charles Chacha, anasema wameupokea mradi huo kwa mikono miwili, ikiwa ni tendo la ukombozi kwa wananchi hao.

"Mradi huu wa halmashauri ya wilaya yetu nimeupokea kwa mikono miwili, kwa furaha kubwa. Umekuwa mkombozi wa wananchi wa Bitiryo na Baraki, ambao shirika la GGF limetusaidia serikali kupunguza tatizo la maji kwa wananchi wa vijiji hivi viwili, pamoja na ule wa kijiji cha Komuge wa kisima kirefu ambao nao wametusaidia GGF," anasema Mkurugenzi Mtedaji.

Huku akirejea kaulimbiu ya serikali 'maji ni uhai' anahimiza: "Mradi huu utunzeni na kuulinda, asitokee mtu akauhujumu kwa kuiba hata vifaa, pampu ya maji, Rorya maji safi na salama ni asilimia 52. Tunategemea miradi mingine kukamilika ya maji ili tufikie asilimia 67. GGF imetukwamua shida ya maji katika vijiji hivyo."




Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la GGF, Amillen Saria, akimtwisha ndoo mkazi wa Bitiryo, baada ya kuzindua mradi wa maji safi na salama.

**MKUU WA WILAYA**

Kaimu Mkuu wa Wialya ya Rorya, Mrunde Daudi, ambaye pia ni Katibu Tawala, anaelekeza agizo kwa viongozi wa serikali ya kijiji na kamati zilizoundwa vijijini, kuusimamia mradi, kuhakikisha wanautunza na kuulinda.

"Nawaagiza Kamati ya Usimamizi wa Mradi, pamoja na serikali ya kijiji kwa pamoja, mhakikishe

INAENDELEA UK.20

MAZINGIRA

# Maelfu Rorya walivyohamishwa kutoka adha maji hadi neema

INATOKA UK.19

mnautunza na kuulinda mradi huu, halafu ni marufuku mifugo kuchungiwa katika maeneo ya visima hivyo, ili kuepuka uharibifu wa mazingira, "anasema Daud.

Anasema mradi huo ukilindwa, ni bayana utakuwa endelevu na kusaidia vizazi vya baadaye. Msisitizo ni vyanzo mbalimbali vya maji vilindwe na visivamiwe na wananchi ili kuweka matumizi bora, huku akiweka angalizo kwamba atakayepuuza agizo hilo atachukuliwa hatua za kisheria.

### CGF NI NINI?

Ni shirika lililosajiliwa mwaka 2014, likiwa na makao makuu yake mjni Musoma, shabaha yake ni kusimamia utoaji huduma sawa za kijamii, zinazolenga ushirikishwaji na kuzingatia haki kwenye manufaa ya matumizi ya rasilimali zilizopo nchini, mtazamo mkuu ni kujenga kuboresha kiwango cha maisha ya jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Amillen Saria anabainisha malengo makuu ya kuanzishwa kwa shirika hilo kuwa ni shirika bora lisilo la kiserikali (Ngo)lenye kuheshimu na kujali misingi ya utu, lisilojihusisha na siasa, dini, ukabila na jinsi kwa kuhimiza ushiriki wa kila mmoja kuanzia katika familia, jamii yenyewe na taifa kwa ujumla katika kujiletea maendeleo endelevu.

"Malengo makuu ya shirika la GGF ni kuwa shirika bora lisilo la kiserikali, lenye kuheshimu misingi ya utu, lisilojihusisha na siasa, dini, kabila na jinsia kwa kuhimiza ushiriki wa kila mmoja kuanzia katika familia, jamii yenyewe na taifa kwa ujumla, katika kujiletea maendeleo endelevu," anabainisha Saria.

Anasema, wanashirikiana na wadau wengine wa nje na ndani wenye mtizamo wa kupunguza umasikini uliokithiri katika jamii, ikiwamo asasi ya Lion's Club International.

Saria anasema, kuwa pia shirika hilo lilianza shughuli zake rasmi mwaka 2016 katika kata sita za majaribio, mbili wilayani Rorya, ambazo ni Komuge na Kyang'ombe.

Aidha, anataja wilayani Butiama, ambako kuna vijiji vya Nyamimange, Bwiregi na Kyanyari.

Mkurugenzi huyo wa CGF, anasema mwaka huu ndio wamekubaliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kuendesha mipango waliokusudia kwa kuongeza kata moja ya Baraki, hali iliyofanya mpango wao kuwa ni wa kata tatu wilayani.

"Wilaya ya Rorya ina kata 26, lakini lengo letu ni kuzifikia kata zote, ili ziweze kupata fursa hiyo muhimu katika mabadiliko ya maendeleo ya jamii, kuwapunguzia umasikini uliokithiri na kuwainua kiuchumi wananchi.



Mradi wa kisima cha maji Kata ya Komuge, Rorya. **PICHA ZOTE: ATHONY GERVAS.**

> **Shabaha yetu ni kusimamia utoaji huduma sawa za kijamii, zinazolenga ushirikishwaji jamii na wenye kuzingatia haki katika kunufaika na rasilimali zilizopo nchini.**



Mwanafunzi wa kidato cha pili, Veronica Mwita, akisukuma maji baada ya kupata mradi huo.

"Shabaha yetu ni kusimamia utoaji huduma sawa za kijamii, zinazolenga ushirikishwaji jamii na wenye kuzingatia haki katika kunufaika na rasilimali zilizopo nchini," anasema Saria.

### DIRA YA MRADI

Mkuu huyo wa CGF, anasema matarajio ya mradi wanaotekeleza sasa, pia yanagusa kuongeza kipato kutoka kwenye shughuli za kilimo na ujasiriamali; kuimarisha vikundi vya kijamii na kiuchumi; upatikanaji wa maji safi na salama katika jamii; kuendelezwa kilimo mseto, kama njia mbadala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Saria anataja matarajio mengine, ni pamoja kuhakikisha kupungua madhara yatokanayo na uendelezwaji wa mila potofu kwenye jamii kama vile ukeketaji, ukandamizaji wa kijinsia na kudhibiti maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) yanapungua.

Baada ya kuzinduliwa mradi huo wa maji safi na salama katika vijiji hivyo, hakuficha furaha yao kupitia kauli ya shukrani, wakiunda kamati za usimamizi wa visima kwa ajili ya kuvitunza na kuviendeleza viwe endelevu.

"Tayari zimeshaundwa kamati za usimamizi wa visima katika vijiji vyote vyenye mradi huu, ambazo tayari zimeshapewa mafunzo ya usimamizi wa visima kwa ajili ya kuvitunza na kuviendeleza viwe endelevu.


"Visima hivyo vikiharibika, sisi shirika hatutahusika tena na matengenezo ya pampu au marekebisho ya aina yeyote, bali watahusika wenyewe....una muda wa matazamio ya kuishi pampu zake miaka miwili," anasema Saria.

Anaeleza kuwa, jamii kupitia maamuzi ya Mkutano wa Wananchi wa vijiji vya Bitiryo na Baraki, wameamua utaratibu kila kaya kuchangia gharama ya Sh.1000 kwa mwezi kugharamia huduma ya maji, ili kuanzisha mfuko wa kuhuduma mradi wa maji wa vijiji hivyo.

Saria anasema, kamati hizo zimepewa majukumu ya kufungua akaunti za visima benki, kusimamia matumizi sahihi, ulinzi wa visima, usafi wa maeneo, uwasilishaji wa taarifa za mapato na matumizi ya fedha za visima kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji, kwa wananchi wa Bitiryo na Baraki.

Wananchi wa vijiji hivyo wamelishukuru shirika la GGF kwa msaada huo wa maji safi na salama ya visima, huku, Emmanuel Nyamaraga, Mwenyekiti wa Kijiji cha Baraki, anakir adha nyingi za kijamii, zitokanazo na safari za kufuata maji, akitaja zinazohusu ndoa, kwani kinamama waliamka alfajiri, hasa kipindi cha kiangazi.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa simu: (+255) 0682869244 na barua pepe: anthonygervas@yahoo.comPICHA***





Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tabora, Said Ntahondi, akifungua kikao maalumu cha Baraza la Madiwani cha kupitia hoja mbalimbali kutoka Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2017/18 jana. **PICHA: DAUDI TIGANYA**

# RC atangaza kuwapiga viboko wapinzani Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametangaza kuwa atawatandika viboko hadharani baadhi ya wanasiasa wanaopinga shughuli za maendeleo katika mkoa wake.

Chalamila alitoa kauli hiyo jana, wakati wa kukabidhi zaidi ya hati za kimila 800 kwa wakazi wa Kijiji cha Hatwelo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya chini ya mradi wa Tanzania Land Tenure Assistance (LTA) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (Usaid). Alisema wako baadhi ya wanasiasa ambao wanakwamisha shughuli za maendeleo kutokana na kupinga kila kitu kinachotekelezwa na serikali.

"Kuna wenzetu kila mradi unavyokuja wanapinga kila kitu kinachoonekana na hapa kijijini wakati mradi unaanza, kuna watu walipinga walikuwa wanasema mnatapeliwa. Hata ujenzi wa barabara ndani ya mitaa na kata wanapinga. Ukweli mimi nimetangaza kiama, nikisikia mtu anapinga jambo ambalo lina ukweli nitamkamata," alisema Chalamila. Alisema baadhi ya watu wanajitoa ufahamu wakidai hakuna maendeleo yoyote yaliyofanywa na kwamba amedhamiria kuwatandika bakora hadharani.

Ofisa Uhusiano na Uenezi wa LTA, Jacqueline Mhengi, alisema mradi huo umekusudia kuwezesha wilaya za mikoa ya Iringa na Mbeya na kwamba katika Kata ya Ijombe, una lengo la kuweka mfumo mzuri wa uwekezaji endelevu katika kilimo Ukanda wa Kilimo wa Nyanda za Juu kusini SAGCOT.

Alisema mradi huo ni shirikishi kati ya halmashauri za wilaya, vijiji na wanavijiji kumilikishwa ardhi zao kwa kufuata taratibu na kanuni kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

Alisema mradi huo utatekelezwa kwenye vijiji 41 ambapo kati ya hivyo, 36 ni vya Iringa na Mbeya vitano. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, alisema hati hizo zitakuwa chachu ya mabadiliko katika kuboresha utawala na usimamizi wa ardhi nchini kama nyenzo ya kuongeza thamani ya ardhi.

# Wataka JPM avunje Bodi ya Kahawa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WADAU na wakulima wa kahawa mkoani Songwe, wamemwomba Rais John Magufuli kuivunja Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) kwa madai kuwa inashirikiana na madalali kuvuruga bei ya zao hilo ambayo imeshuka kwa zaidi ya asilimia 30.

Waliyasema hayo jana kwenye mkutano uliohusisha wakulima, wadau, bodi na viongozi wa serikali mkoani hapa.

Kwa mujibu wa wadau hao, bei ya kahawa kwa soko la dunia ni dola 145 kwa gunia moja, lakini wakulima wamelazimishwa kuuza kwa bei ya dola 90 hadi 40 kwa gunia moja, ambayo ni chini ya bei elekezi ya dola 120 na kwamba kwenye mnada wa Agosti 8, mwaka huu, hakuna mnunuzi aliyejitokeza.

Kutokana na hali hiyo, wadau na wakulima walimwomba Rais Magufuli aivunje TCB kwa madai ni chanzo cha kuvuruga bei ya kahawa na kusababisha kushuka kupitia mnada.

Mmoja wa wadau hao, Charles Chenza, alisema madalali wakishanunua kahawa kwa wakulima, huuza kwa bei nono ambayo iko nje ya utaratibu wa mnada.

"Tunamwomba Rais Magufuli amulike Bodi ya Kahawa ili kuibua madudu yaliyopo na ikiwezekana kuundwa upya ili wakulima na wadau tunufaike na zao hili ambalo ni tegemeo katika kuendesha maisha yetu," alisema Chenza.

Samson Simkoko aliwahimiza wakulima wenzake kuwa wamoja na kutokubali kurubuniwa na madalali ambao wana lengo la kuwalangua ili wajinufaishe kupitia jasho lao.

Aliwashauri wakulima waendelee kuuza kahawa yao kwenye minada ambayo imewekwa na vyama vya ushirika.

Meneja wa TCB Nyanda za Juu Kusini, Gerald Mlay, alisema hawezi kuyasemea madai hayo kwa kuwa msemaji wake ni Mkurugenzi Mkuu aliyeko Dar es Salaam.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, David Kafulila, alikiri kuwapo kwa changamoto kwenye Bodi ya Kahawa na kusema ni lazima iwajibishwe kwa mujibu wa sheria.

# Mashauri 30 kuamuliwa Mahakama Rufani Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Rufani ya Tanzania inatarajia kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri 30 ya makosa ya kijinai na madai katika mkoa wa Mbeya ambayo yalishindikana kutatuliwa katika Mahakama Kuu na kukatiwa rufani.

Naibu Msajili wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Bernard Mpepo, alisema hayo jana, mjini hapa na kwamba yataanza kusikiliza makosa ya jinai na baadaye madai kupitia jopo la majaji watatu.

Mpepo alisema kesi hizo zitaendeshwa kwa wiki tatu katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya na jopo la majaji hao litaongozwa na Jaji Stella Mugasha.

"Katika mashauri haya kuna rufani sita za makosa ya mauaji, mashauri mawili ya uhujumu uchumi, mashauri mawili ya ubakaji na yaliyobaki ni ya unyang'anyi wa kutumia silaha," alisema Mpepo.

Kaimu Mkuu wa Mashtaka wa Mbeya na Songwe, Baslius Namkambe, alisema kwa mujibu wa sheria za nchi Mahakama ya Rufani ndiyo mahakama ya mwisho katika kutoa uamuzi wa makosa mbalimbali yaliyoshindakana.

Baadhi ya wananchi wa Jiji la Mbeya walifurahia uamuzi wa mahakama hiyo kuanza kusikiliza mashauri na kwamba itasaidia kutoa uamuzi mapema.

Mmoja wa wananchi hao, Zella Mwambeta, alisema jopo hilo la majaji litasaidia kushughulikia madai hayo kwa wakati, huku akishauri kutenda haki.

Katika mashauri hayo 30, 26 ni kutoka rufani za Mbeya na manne ni kutoka Rufani za Rukwa, huku makosa ya jinai yakiwa 27 na madai yakiwa ni matatu.





# Takukuru yawaonya makandarasi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), Mkoa wa Dodoma imewataka makandarasi na wasimamizi wa miradi katika halmashauri kuhakikisha wanatekeleza miradi hiyo kwa ufanisi kulingana na taratibu za mikataba waliyoingia.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Taasisi hiyo mkoani hapo, Sosthenes Kibwengo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ufuatiliaji wa rushwa katika miradi mbalimbali ya maji na mingine inayotekelezwa katika halmashauri.

Alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya makandarasi kutekeleza kinyume na taratibu mikataba waliyoingia hali inayosababisha miradi kujengwa chini ya kiwango.

Alitaka kila mmoja kutambua wajibu wake katika kazi anayofanya kitendo ambacho kitamfanya awe salama katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwamo kukwepa mkono wa sheria inayokataza kutoa na kupokea rushwa.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na wao wanapaswa kutoa ushirikiano kuitekeleza kulingana na thamani ya fedha ambayo wamekabidhiwa.

Pia alisema kinachotakiwa ni kuhakikisha wanaifanya miradi kwa weledi ili iweze kuleta tija kwa wananchi wa eneo husika.

Alisema Takukuru hawatakuwa na msamaha wowote kwa yeyote ambaye atakutwa na makosa ya kupokea rushwa kutoka kwa jamii. "Naomba makandarasi na wasimamizi wa miradi hiyo kuweni makini na kazi mlioaminiwa kwa sababu mkiharibu mnawakwamisha wananchi na serikali kwa ujumla," alisema Kibwengo.

Kibwengo alisema miradi hiyo ni muhimu, hakuna sababu ya wao kwenda kinyume na taratibu zilizowekwa katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Alifafanua kuwa wao kama Takukuru wanazidi kuwasisitiza watu kutoa ushirikiano katika utoaji wa taarifa pale wanapoona kuna viashiria vya rushwa katika maeneo mbalimbali ambayo yanamanufaa kwa jamii.

Alisema lengo lao ni kuona kila mmoja anatambua umuhimu wake katika sekta ambayo anaitumikia kwa mujibu wa sheria jambo ambalo litaleta manufaa kwa taifa.

Aliwataka wananchi kutoficha maovu wanayoona katika miradi ambayo inatekelezwa ili iwe rahisi kwa taasisi hiyo kuwabaini wanaofanya vitendo viovu vya upokeaji rushwa.

Alisema udhibiti wa rushwa ni wa kila mtu na kuongeza kuwa kila mmoja anapaswa kuwajibika kulingana na nafasi aliyokuwa nayo katika kupambana na rushwa.

Katika hatua nyingine, Kibwengo alisema Takukuru itaendelea kutoa elimu ya kupambana na rushwa katika maeneo mbalimbali jijini Dodoma ili kuhakikisha wananchi wote wanapata uwelewa katika elimu hiyo.

Alisema lengo lao ni kuona kila mmoja anapata uelewa na kuwa balozi wa kupiga vita suala la rushwa katika eneo analotoka.



Mdau wa elimu hapa nchini, Dk. Ombeni Msuya, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ntyuka ya jijini Dodoma jana, walipokwenda kukabidhi msaada wa vifaa vya elimu shuleni hapo. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana watakiwa kutumia fursa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA nchini wametakiwa kutambua fursa katika jamii zao ili kujitengeneza ajira na kuacha kulalamika vijiweni.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Vijana kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ester Riwa, wakati alipokuwa akizungumza katika mkutano wa vijana kujadili maazimio ya kuwa na Baraza la Taifa la Vijana.

Riwa alisema vijana wanatakiwa kuwa wabunifu katika kutambua fursa zilizopo katika jamii ili kujitengenezea ajira na kuondokana na malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa kila siku.

Alisema pamoja na vijana kuhitaji kuwa na baraza lao, lakini bado ipo changamoto kwao ya kutambua fursa zilizopo ili waweze kujitengenezea ajira.

"Vijana wanatakiwa kuanza na kitu kwanza, Baraza la Vijana likianza liwakute wakiwa tayari wana kitu cha kufanya ili sisi kama serikali tuwawezeshe mitaji itakayowawezesha kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo," alisema.

Vilevile, aliwataka vijana kuacha tabia za kujadili mambo bila kuchukua hatua za kuyatekeleza.

"Vijana lazima tuwe na uthubutu, wengi wenu mmekuwa wazungumzaji sana lakini hakuna anayefanya kwa vitendo lazima muwe na uthubutu katika kufanya mambo mbalimbali nyinyi ndiyo tunao wategemea kama taifa," alisema.

Pia aliwataka vijana kuwa na tabia ya kutafuta taarifa mbalimbali zinazobainisha fursa zilizopo serikalini pamoja na maeneo mengine ili waweze kuzitumia katika kujitafutia ajira.

Alisema vijana wengi hivi sasa wamekuwa bize muda mwingi kutafuta taarifa ambazo hazina tija kwao na kuacha zile ambazo zingeweza kuwasaidia katika maisha yao.

Godfrey Chacha kutoka Idara ya Vijana Ofisi ya Waziri Mkuu, alisema mchakato wa kuwa na Baraza la Vijana upo katika hatua za mwisho kukamilika.

Alisema tayari sheria pamoja na kanuni ya kuwa na baraza hilo vimeshaundwa kinachosubiriwa ni kuanza kutumika kwa kuwa na muundo wa uongozi wa baraza hilo, kuanzia ngazi ya taifa hadi ngazi za chini.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Vijana Assembly, Mbayani Tayai, ambao ndio waandaaji wa mkutano huo, alisema lengo la kikao hicho ni kuangalia na kuandaa maazimio ya vijana na kuyawasilisha kwa serikali mapendekezo kuhusu baraza la vijana la taifa.

Alisema kuanzishwa kwa baraza hilo kutawasaidia vijana kuwa na chombo cha kujadili mambo yao na kuyafikisha katika ngazi mbalimbali za serikali bila kujali itikadi zao za dini au vyama vya siasa.

## Mpwapwa yajenga wodi ya utapiamlo

**Na Mwandishi Wetu,** MPWAPWA

KATIKA kukabiliana na tatizo la utapiamlo na udumavu, Wilaya ya Mpwapwa ipo mbioni kukamilisha ujenzi wa wodi kwa ajili hiyo katika Hospitali ya Wilaya.

Wodi hiyo inajengwa kufuatia utafiti uliofanywa mwaka 2017/2018 wa hali ya lishe nchini na utoaji wa vitamini A kwenye wilaya hiyo kuonyesha kuwa kati ya watoto 70,117 waliopimwa, asilimia 37 kati yao wana udumavu, asilimia 12 wana uzito pungufu na asilimia moja wana unyafuzi.

Ujenzi wa wodi hiyo uliwekewa jiwe la msingi juzi na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2019 kitaifa, Mzee Mkongea Ally, baada ya kuridhishwa na ujenzi wake. Akitoa maelezo kuhusu ujenzi huo, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Arcard Rwezaula, alifafanua kuwa lengo la kujengwa wodi hiyo ni kutoa matibabu kwa watoto wenye utapiamlo mkali chini ya miaka mitano.

"Mwaka 2017/2018 wakati wa utoaji wa matone ya vitamini A, minyoo na upimaji wa hali ya lishe chini ya miaka mitano ulionyesha uwapo wa tatizo la utapiamlo mkali hivyo baada ya kuona hali ilivyo duni kwa kushirikiana na wadau hao wakaona wajenge jengo hilo la kutoa matibabu ya utapiamlo mkali katika wilaya yetu," alisema.

Aliwaomba wananchi baada ya wodi hiyo kukamilika waende kupata matibabu, huduma na elimu ya namna ya kuboresha lishe ili kuondokana na tatizo hilo.

Akielezea hatua walizochukua mpaka sasa za kuhakikisha wanakabiliana na tatizo hilo, Dk. Rwezaula alisema vituo vyote 62 vya kutolea huduma katika halmashauri hiyo wahudumu wake wamefundishwa namna ya kutambua na kuwapatia huduma watoto wenye utapiamlo.

Akizungumza baada ya kukagua wodi hiyo inayojengwa kwa ufadhili wa Shirika la Action Against Hunger (AAH), kiongozi huyo alisema ameridhishwa na ujenzi na kutoa maelekezo ya kuhakikisha maji yanakuwapo saa 24. "Watu wanaweza wakajiuliza kwanini tunatumia muda mrefu kukagua wakati fedha ni za wafadhili, ndugu zetu hawa wametoa kodi za wananchi wao ili kusaidia nchi yetu, hivyo ni lazima tuwe na uchungu ili kuwapa shauku ya kuendelea kusaidia miradi hii," alisema.

Akizungumza baada ya maelekezo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema maelekezo yaliyotolewa wameyapokea na watayafanyia kazi.

"Maelekezo uliyoyatoa tumeyapokea na tutayatekeleza, kuhusu maji tayari tulishaanza kufanyia kazi na hapa kuna tangi moja la maji tutajitahidi kuhakikisha huduma hii inapatikana kwa saa 24," alisema Shekimweri.





# Ataka ushirikiano kuendeleza elimu

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, ameitaka Taasisi ya Kimaendeleo kutoka nchini Nadhalend (NHHL), kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuendeleza sekta ya elimu nchini.

Akizungumza na mkurugenzi wa taasisi hiyo alipofika ofisini kwake, waziri huyo alisema ushirikiano huo utasaidia katika kuimarisha udugu wa nchi mbili hizo.

Alisema bado Zanzibar inakabiliwa na upungufu wa madarasa hasa katika ngazi ya shule za maandalizi na msingi, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watoto wapya wanaoandikishwa shule kila mwaka.

Waziri Pembe alisema bado serikali na wafadhili mbalimbali wanaendeleza jitihada za kusaidia kujenga madarasa mapya ili kusaidia kupunguza tatizo hilo.

Aidha, aliishukuru taasisi hiyo kwa uamuzi waliochukua kuamua kujenga shule ya maandalizi na msingi Zanzibar na kuahidi kuwa serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wa elimu ili kuleta maendeleo nchini.

Naye Mkurugenzi wa NHHL, Ayhan Arslantas, alisema amefarajika kufika Zanzibar kutokana na ushirikiano mzuri alioupata na kuahidi kuendelea kujenga shule katika sehemu zingine ili kuendeleza elimu Zanzibar.

Taasisi hiyo tayari imeshajenga shule ya maandalizi na msingi inayojulikana VIVID Dreams na kufunguliwa na Waziri Pembe katika eneo la Mbuzini Wilaya ya Magharibi A, Unguja.




Wakazi wa Wilaya ya Nachingwea, Mkoa wa Lindi, wakitafuta wanunuzi wa mianzi ambayo ni maarufu kwa ajili ya kujengea uzio. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Neema wananchi kushuka bei za mafuta

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imetangaza bei mpya ya mafuta ambayo ilianza kutumika rasmi jana.

Kwa mujibu wa taarifa ya mamlaka hiyo, bei hiyo imeshuka ikilinganishwa na mwezi uliopita.

Akitangaza bei hizo mbele ya waandishi wa habari katika ofisi za mamlaka hiyo zilizoko Maisara, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliaano cha Zura, Khuzaimat Bakari Kheri, alisema sababu ya kushuka kwa bei za mafuta ni kutokana na kushuka kwa bidhaa hizo katika soko la dunia.

Kutokana na kushuka huko, alisema bei ya mafuta ya petroli kwa mwezi huu ni Sh. 2,181 wakati Julai ilikuwa Sh. 2,338.

"Mafuta ya dizeli yameshuka kwa asilimia 4.23, bei ya Julai ilikuwa Sh. 2,319 na bei ya mwezi huu itakuwa Sh. 2,221," alisema.

Mkuu huyo wa mawasiliano alisema mafuta ya taa kwa mwezi huu yatauzwa kwa Sh. 1,675 kwa lita wakati mwezi uliopita bei ilikuwa Sh. 1,753.

Pia alisema bei ya mafuta ya meli (banka) itakuwa Sh. 2,047 na kwamba imeshuka kulinganisha na mwezi uliopita kwa kuwa ilikuwa ikiuzwa kwa Sh. 2,145.

"Zura inapenda kuwajulisha wananchi kuwa bei zilizotangazwa ndizo bei halali zitakazoanza kutumika kuanzia siku ya Jumatano ya Agosti 14 mwaka huu," alisema.

# Akemea abiria kutozwa nauli kubwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mohammed Ahmada Salum, amesema ni uonevu unaofanywa na baadhi ya madereva na utingo wa daladala kuwatoza wananchi nauli kubwa tofauti na iliyotangazwa na serikali.

Salum alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na abiria na baadhi ya madereva na utingo wa daladala mjini Zanzibar wanaodaiwa kuwatoza wananchi nauli kubwa kinyume cha iliyopangwa na serikali ambayo ni Sh. 400.

Alisema serikali imeamua kuweka nauli hizo ili kuwasaidia wananchi na wafanyabiashara wa usafiri huo, hivyo kama kuna mtu anafanya kinyume cha matakwa ya serikali, anapaswa kuchukuliwa hatua.

Naibu Waziri alisema hali hiyo haikubaliki na wananchi wasikubali kudhulumiwa haki yao, hivyo ni vyema kushirikiana na kuwa na msimamo wa pamoja kwa kutoa taarifa pale wanapotozwa nauli kubwa.

"Wamiliki wa magari yote ya abiria wahakikishe wanaweka taarifa za bei ya nauli pembeni mwa magari yao pamoja na namba za gari na namba za simu zangu, kamanda wa usalama barabarani pamoja na katibu wa bodi ya usafiri, ili kuwasaidia wananchi kutoa taarifa," alisema.

Alisema serikali italifuatilia suala hilo katika maeneo yote ambao madereva watabainika wanakwenda kinyume cha agizo la serikali.

Naye Katibu wa Bodi ya Usafiri Zanzibar, Mohammed Simba Hassan, alisema wameamua kufanya ziara hiyo kutokana na malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na wananchi juu ya wamiliki wa daladala katika maeneo hayo kutoza nauli kubwa tofauti na ile iliyotangazwa na serikali.

Aliwatahadharisha wamiliki wa daladala kwamba hilo ni onyo la mwisho na yeyote atakayekwenda kinyume, atachukuliwa hatua za kisheria.

Baadhi ya wananchi walisema wanashangazwa na baadhi ya makondakta wa daladala kuwatoza nauli kubwa ambayo haijatangazwa na serikali.

Kwa upande wao, madereva na utingo wa daladala zinazofanya safari katika maeneo hayo, waliishukuru serikali kwa kuwaelimisha na kuwaomba kuendelea kuzungumza nao.

# Singida kicheko kukamilika ujenzi wa hospitali ya wilaya

**Na Elisante John,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Singida imetumia zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya, iliyojengwa kwenye Tarafa ya Ilongero, katika kijiji cha Sekou Toure.

Fedha hizo zilitolewa na serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya kutekeleza mradi huo pamoja na wilaya zingine ambazo hazina hospitali kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma za afya.

Mbunge wa Singida Kaskazini, Justine Monko, alisema kwa asilimia kubwa tayari majengo takribani saba yamekamilika, hivyo kufufua matumaini na ndoto ya muda mrefu ya wananchi wa wilaya hiyo kupata hospitali yao itakayowarahisishia tiba.

"Nipende tu kuishukuru serikali ya awamu ya tano inayowajali wanyonge. Kupitia Rais John Magufuli anayewajali wanyonge, ametupatia fedha za mradi huu, hivyo kuwezesha wananchi kunufaika na huduma za tiba karibu zaidi," alisema.

Alisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli katika kuwaletea wananchi maendeleo na kupongeza juhudi za Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, kufanya ziara kwa wilaya hiyo na kuagiza ujenzi huo kukamilika haraka, hali ambayo sasa ndoto hiyo imetimia.

Monko alisema licha ya ujenzi wa hospitali hiyo, serikali pia iliipatia halmashauri hiyo zaidi ya Sh. bilioni moja, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vipya vya afya katika kata za Msange na Mgori, ambavyo ujenzi wake ni wa kiwango cha juu.

Alibainisha kuwa sasa wananchi wa maeneo husika na yale ya jirani, watanufaika na huduma za afya kwa ufanisi, kitu ambacho ndicho lengo la serikali kuhakikisha jamii inaondokana na adha ya kufuata huduma za afya mbali na maeneo yao.

Aidha, Monko alitumia fursa hiyo kuwashukuru wananchi wa halmashauri ya wilaya hiyo wanavyojitolea katika kushirikiana na serikali kwenye miradi ya maendeleo, ikiwamo ya afya, elimu, maji na barabara.

Mbunge huyo aliwaomba wananchi wa jimbo hilo kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na kero mbalimbali zilizodumu kwa miaka mingi ili kuwezesha shughuli za uzalishaji mali kuendelea vyema ndani ya jamii. Katika hatua nyingine, Monko aliwataka watumishi wa umma wa halmashauri hiyo kuendelea kuwa karibu na wananchi katika kuwatumikia na kuendeleza mshikamano baina yao, ili kumaliza kero zinazowakabili kwa kushirikiana na serikali.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Rashidi Mandoa, alisema kukamilika kwa ujenzi huo, kutafungua fursa kwa wananchi wa wilaya hiyo kunufaika na huduma za tiba, kupitia hospitali hiyo mpya ya serikali.

Alisema kwa sasa serikali inajipanga vyema kukabiliana na changamoto zilizobaki zikiwamo vifaa tiba na watumishi ambazo zitawezesha kuendesha hospitali hiyo kwa ufanisi.



Meneja Masoko na Mahusiano ya jamii wa Benki ya Exim, Abdulrahman Nkondo (alievaa kofia nyeupe), akiwagawia vinywaji baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam waliojitokeza kwenye viunga vya Stendi ya mabasi ya Mbagala kuchangia damu kwa ajili ya majeruhi wa ajali ya moto iliyosababishwa na lori la mafuta eneo la Msamvu mkoani Morogoro ambapo watu zaidi ya 70 walifariki dunia na wengine kujeruhiwa. Zoezi hilo la siku tatu limeratibiwa na benki hiyo kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS)na linatarajiwa kukamilika Agosti 16. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Waziri akemea ucheleweshaji hati

**Na Munir Shemweta,** TABORA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekemea ucheleweshaji wa utoaji hati za ardhi katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Amesema kitendo hicho kinachangia kuikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi ya ardhi.

Dk. Mabula alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ziara yake ya kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi na kukagua mifumo ya kodi kwa njia ya kielektroniki na masijala ya ardhi katika mkoa wa Tabora.

Alisema hayo baada ya kubaini uwapo wa hati 92 za ardhi katika manispaa hiyo, ambazo hazijafanyiwa kazi kwa muda mrefu kwa madai kuwa baadhi ya majalada ya hati yalikuwa na upungufu na wahusika wake hawapatikani.

Naibu Waziri alishangazwa na hali hiyo kwa kuwa baadhi ya maombi ya hati yana zaidi ya miaka miwili katika ofisi ya Ofisa Ardhi Mteule wa Manispaa ya Tabora bila kufanyiwa kazi, jambo alilolieleza kuwa linawakatisha tamaa wananchi wanaoomba hati.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mabula alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Bosco Ndunguru, kumwandikia barua ya onyo Ofisa Ardhi Mteule wa Ardhi, Daudi Msengi, kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, kwa sasa wizara yake haitamvumilia mtumishi yeyote wa ardhi atakayeshindwa kutekeleza majukumu yake na kusisitiza kuwa upandishwaji vyeo kwa watumushi utazingatia utendaji kazi na kuwataka kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Pia alizitaka halmashauri nchini kupanga malengo ya uandaaji hati za ardhi kwa watendaji wake ili kuelewa kwa siku moja zinaandaliwa hati ngapi na kwamba hiyo itazisaidia halmashauri kufikia malengo ya utoaji hati.

Dk. Mabula alitolea mfano wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza kuwa imejiwekea malengo ya kuandaa hati tano kwa siku moja, jambo lililoiwezesha kuandaa hati nyingi, hivyo kuwa moja ya halmashauri zinazofanya vizuri kwa utoaji wa hati za ardhi.

Alisema Manispaa ya Tabora imeshindwa hata kutimiza malengo yake ya kutoa hati katika mwaka wa fedha 2018/19. Manispaa hiyo ilijiwekea lengo la kutoa hati 2,000 lakini ilitoa 1,200 tu.

# Neema yaja kwa wanaovaa miwani kwa uoni hafifu

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA ambao wanalazimika kuvaa miwani kutokana na uoni hafifu hii ni habari njema kwao, baada ya huduma ya kisasa ya kurekebisha uono wa macho imeingia nchini ambapo mhusika anapopata huduma hii anakuwa hategemei tena kuvaa miwani ili kuona vizuri.

Kwa mujibu wa Meneja wa Hospitali ya Kimataifa ya macho ( International Eye Hospital) inakotolewa huduma hiyo, Adam Mwatima, hospitali hiyo ndiyo ya kwanza kutoa huduma hiyo ambayo ni nadra kupatikana hapa nchini na katika nchi nyingi za Afrika.

Alisema huduma hiyo ilianza kutolewa hospitalini hapo mwezi Mei mwaka huu na waliofanyiwa marekebisho hayo (upasuaji mdogo) wameonyesha matokea mazuri kwani hawahitaji kuvaa miwani tena ili kuona mbali au karibu.

"Tuliamua kuanza kutoa huduma hii baada ya kuona uhitaji mkubwa kwa Tanzania na ili kupunguza gharama kwa watu ambao walikuwa wakilazimika kwenda mataifa ya Ulaya na Marekani kutafuta huduma hii. Sasa huduma hii inapatikana hapa nchini Tanzania," alisema.

"Tunafanya hivi kuunga mkono sera ya serikali kuhakikisha matibabu kama haya ya magonjwa yasiyo ya kuambukizwa yapatikane hapa nchini. Tunalenga pia kukuza utalii wa kimatibabu (Medical Tourism) ili watu wa nchi za Afrika Mashariki kama Uganda, Rwanda, Burundi na nchi nyingi za Afrika waje kupata huduma hii hapa nchini," alisema.

Alisema hospitali hiyo imeanza kutoa huduma hizo za kibingwa kwa punguzo la asilimia 50 ili kuhakikisha Watanzania wengi wenye kuhitaji huduma hiyo wanamudu kuipata kwa gharama za nafuu tofauti na ambapo wangeenda nje ya nchi. Alisema huduma hiyo hufanywa na madaktari bingwa wa hospitali hiyo wenye uzoefu wa miaka mingi kwenye kazi hiyo.

Daktari bingwa wa macho wa International Eye Hospital, Dk. Aydin Yildirim, alisema daktari anaweza kurekebisha macho ya mgonjwa kwa kutumia njia ambayo kwa kitaalamu inajulikana kama Laser assisted in Situ Keratomileusis (LASIK) au njia ya Photorefractive Keratoctomy (PRK) kulingana na hali ya macho ya mhusika

"Daktari baada ya kumwangalia mhusika na kumfanyia vipimo ataamua atumie njia gani kati ya hizo mbili kumhudumia lakini cha muhimu ni kwamba mtu akishafanyiwa marekebisho hayo hahitaji tena kuvaa miwani maisha yake yote," alisema

## HABARI KIMATAIFA

# Polisi wafukua maiti, waivua nguo

**NAIROBI,** Kenya

MAOFISA kutoka Magharibi mwa Kenya wamelazimika kuufukua mwili wa Martin Shikuku Alukoye aliyezikwa na sare.

Marehemu Alukoye alizikwa akiwa na sare zake za huduma ya vijana wa Kaunti ya Kakamega baada ya kufa maji mwezi huu.

Imeelezwa kuwa baada ya mwili wa marehemu kuzikwa baadaye maofisa wa kaunti hiyo, waliufukua mwili wake ili kumvua nguo hizo kulingana na ripoti.

**Mjomba wa marehemu, Francis Mutamba alieleza kuwa maofisa hao walikiuka sheria za nchi na tamaduni.**

Mjomba wa marehemu, Francis Mutamba alieleza kuwa maofisa hao walikiuka sheria za nchi na tamaduni.

Alisema; "Tuliishirikisha serikali ya kaunti katika mipango ya mazishi na hawakupinga pendekezo letu kumzika akiwa na sare za kazini," alisema Mutamba.

Familia hiyo inasema kwamba ilipinga ombi kutoka kwa maofisa kuchukua nguo hizo kufuatia kuzikwa kwa kijana wao mwenye umri wa miaka 31, kwamba maofisa waliamua kuufukua mwili huo bila idhini yao au agizo la mahakama.

Naibu Chifu wa eneo la Ituti, Daniel Namayi alishutumu maofisa hao kwa kitendo cha kufukua mwili wa marehemu na kuonya kuchukua hatua za kisheria dhidi ya maofisa hao.

"Mara tu mwili unapozikwa, utahitaji agizo la mahakama kwa mtu yeyote mwenye malalamishi kuufukua. Wasimamizi wa kaunti wameenda kinyume na sheria kwa kuufukua mwili suala ambalo ni kinyume na utamaduni," alisema Namayi na kuongeza:

"Tuliamua kumzika mtoto wetu usiku kuambatana na tamaduni ambazo zinasema kwamba mtu aliyekufa maji hapaswi kuzikwa wakati kuna mwanga wa jua. Lakini maofisa wa kaunti wametushangaza wakati walipoamua kuufukua mwili ili kuchukua sare alizozikiwa nazo," alisema Mutamba.

Hata hivyo, mwili wa marehemu ulivishwa nguo mpya na kuzikwa tena mapema baada ya wazee kufanya matambiko ya kuitakasa familia hiyo. **BBC**



Polisi wakilinda ukumbi wa kuondoka abiria wa Uwanja wa Ndege wa Hong Kong baada ya kupambana na waandamanaji juzi. **PICHA: REU-**

# Wananchi waendelea kuisubiri serikali mpya

**KINSHASA,** Congo

WANANCHI wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) wamekaa 'mkao wa kula' wakisubiri kusikia nani na nani kaingia na kutoka kwenye serikali mpya ya Rais, Felix Tshisekedi.

Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Sylvestre Ilunga anatarajia kuwasilisha kwa Rais Tshisekedi majina ya watu waliopendekezwa kuhudumu kwenye nafasi za mawaziri kwenye serikali hiyo mpya.

Uteuzi wa mawaziri hao unatarajiwa kutangazwa muda wowote kuanzia sasa. Viongozi wa makundi 21 na chama cha siasa vinavyojumuika kwenye muungano FCC wamekutana na Seneta Joseph Kabila, ambaye ni nguzo ya muungano huo kwa kuzungumza kuhusu mgawanyo wa majukumu katika serikali mpya ijayo.

Kulingana na vyanzo vya karibu na muungano wa FCC, nafasi za mawaziri zilitolewa kulingana na idadi ya wabunge ambao kila chama kinao katika Bunge la Kitaifa.

Pamoja na wabunge 118 katika ngazi ya taifa, chama cha PPRD kitachukuwa nafasi za mawaziri 11 na manaibu mawaziri watatu.

Muungano wa AAB unaojumuisha vyama kadhaa vya siasa katika muungano wa FCC, utaweza kupata mawaziri watatu na naibu waziri, vyama vingine vinaweza kuwa na waziri mmoja au wawili au naibu waziri, kulingana na chanzo hicho.

Makundi matatu ambayo hayana wawakilishi bungeni hayataweza kuwakilishwa katika serikali hiyo mpya.

Kwa upande mwingine, wafuasi wa chama cha AFDC ambao wameendelea kushirikiana na Joseph Kabila wanaweza kuwakilishwa serikalini.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema Rais mstaafu Joseph Kabila atanufaika na kiwango cha asilimia 10 kwenye nafasi 42 zilizohifadhiwa kwa washirika wake wa kisiasa. **RFI**

# Safari za ndege zarejea baada ya maandamano

**HONG KONG,** China

SAFARI za ndege zimeanza kurejea mjini Hong Kong baada ya kusitishwa kwa siku mbili.

Jaji Mkuu wa mahakama mjini humo ndiye aliyetoa amri ya muda kudhibiti maandamano ya kupinga serikali yaliyo sababisha shughuli za usafiri kusitishwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, Hong Kong.

Shughuli kwenye uwanja wa ndege wa Hong Kong ambao ni miongoni mwa viwanja vinavyohudumia wasafiri wengi zaidi duniani, zimeanza tena taratibu asubuhi ya jana.

Lakini mamlaka ya uwanja huo imeonya kuwa baadhi ya safari zinaweza kuendelea kutatizwa.

Tangazo la kurejesha safari za ndege liliwekwa kwenye huduma ya simu za mkononi, au app ya uwanja huo mnamo saa 12 asubuhi kwa saa ya Hong Kong.

Uwanja huo ulikuwa umeahirisha safari zote za ndege tangu Jumatatu, baada ya maelfu ya waandamanaji kukusanyika katika ukumbi wanakofikia wasafiri.

Wengi wa waandamanaji hao wameondoka usiku wa kuamkia jana, wakibaki wapatao 50 tu.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ya Hong Kong jana ilieleza kuwa Jaji Mkuu ametoa amri ya muda wa kudhibiti maandamano ya kuipinga serikali, katika moja ya uwanja wa ndege mkubwa duniani, ambapo kwa siku mbili waandamanaji walikuwa wameleta ghasia kwa kupambana na polisi.

Amri hiyo inawataka waandamanaji kuwapo katika maeneo maalumu, ikiwa ni juhudi za kuzuia msongamano ambao ulisababisha wafanyakazi wa serikali na mashirika ya ndege kurudishwa majumbani ikiwa pamoja na kusitisha safari zote za ndege za kutoka na kuingia katika himaya hiyo ya China.

Hatua hiyo ilisababisha wasafiri wa ndege kutojua la kufanya na kutokuwa na uhakika wa lini wataendelea na safari zao, huku wakishindwa kununua chakula na kukosa mahala pa kulala. **VOA**

HABARI KITAIFA

# Watumishi 137 wapewa siku 7 kulipa 'ultra sound'

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga (pichani), ametoa siku saba kwa watumishi wote wa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi (Somanda), kuhakikisha wananunua mashine ya kupima magonjwa ya ndani na kutambua taarifa za mwili wa binadamu (ultra sound) ambayo iliibwa hospitalini hapo katika mazingira ya kutatanisha.

Alitoa agizo hilo jana katika kikao chake na watumishi wote wa hospitali hiyo, ambapo alitoa siku saba kwa watumishi wote kuchanga kulingana na kiwango cha mshahara kwa kila mtumishi ili kuhakikisha wananunua mashine hiyo.

Kiswaga alimtaka Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Mike Mabimbi na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Merkzedeck Humbe, kuhakikisha siku hizo zikipita wanamletea mashine hiyo ofisini kwake.

"Kwa kuwa mashine hii iliibwa mchana na ikaibwa na vifaa vyake vyote, inaonyesha kuwa waliohusika ni wataalamu na kwa maana hiyo watumishi wote 137 wa hospitali hii mnahusika na wizi huu, hivyo nyie ni watuhumiwa wa kwanza wa wizi huu," alisema Kiswaga.



"Kila mmoja kuanzia kwa mganga mkuu wa halmashauri mtachangia kulingana na kila mtu na mshahara wake, nataka ndani ya siku saba nikabidhiwe hiyo mashine, ambaye atagoma kuchangia huyo itakuwa halali yangu," aliongeza Kiswaga.

Mbali na uamuzi huo, Mkuu huyo wa Wilaya alisema watumishi 17 ambao walikamatwa na polisi kwa ajili ya uchunguzi, na kuwa kesi yao itaendelea kufanyiwa kazi, huku akimtaka Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) kukamilisha uchunguzi haraka dhidi yao na hatua zaidi ziweze kuchukuliwa.

Aidha, Kiswaga alimtaka Ofisa Utumishi wa halmashauri hiyo kuorodhesha majina yote ya watumishi hao kwenye karatasi kisha kumpatia kwa ajili ya kuangalia nani atakaidi kuchanga ili mashine hiyo inunuliwe.

Aidha, alisema kuwa tabia ya wizi katika hospitali hiyo imekuwa sugu ambapo wahusika wakuu wamekuwa watumishi wake, hali ambayo alieleza hawezi kuivumilia kama kiongozi wa wilaya.

Kiswaga alisema kuwa yuko tayari kufukuzwa kazi kwa hatua yoyote ambayo atachukua kwa watumishi hao ikiwa watashindwa kuhakikisha wanarudisha mashine hiyo kupitia michango yao ndani ya muda ambao ametoa.

Mkurugenzi wa Halmashuari, Merkzedeck Humbe, alisema kitendo hicho ni fedheha kwa halmashuari na serikali pia, hivyo alisema hatua kali zitachukuliwa kwa wahusika.

Mabimbi alisema mashine hiyo iliibwa Agosti 5, 2019 mchana ikiwa kwenye wodi ya wajawazito hospitalini hapo.

Mabimbi alisema kuwa baada ya kupata taarifa za wizi huo walitoa taarifa polisi ambapo watumishi 17 walikamatwa na wamehojiwa, na uchunguzi dhidi yao unaendelea.

## Shahidi akana mawasiliano na Zitto

INATOKA UK. 5

hivyo wananchi waliwapa elimu kutoka katika eneo la hifadhi.

Alidai kuwa baada ya kupatikana eneo, operesheni ya kuwahamisha ilianza kwa kuwatumia askari wa wilaya, mgambo na wananchi na Oktoba 15, 2018 alipata taarifa kuna vurugu ilitokea.

Alidai kuwa alikwenda kuonana na diwani; "lakini hatukuweza kuzuia tukabakia tumekaa hadi Oktoba 18, 2018 nilipopigiwa simu na Mkuu wa Wilaya niende, nilipofika niliwakuta Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa, wakasema walishindana na wananchi wanaomba msaada tuende porini kutafuta miili ya marehemu."

"Mheshimiwa hakimu tulikwenda porini Oktoba 19, 2018 tukafanikiwa kupata miili ya marehemu wawili askari na baadaye ilifahamika kuna raia wengine wawili walifariki katika operesheni hiyo na kufanya idadi ya waliokufa kufikia wanne," alidai shahidi huyo.

Aliwataja waliokufa kuwa ni Mkuu wa Kituo cha Polisi na polisi anayeitwa Muddy na kwa upande wa raia walikufa wawili.

Shahidi alidai, jina la Zitto analisikia, lakini hajawahi kuwasiliana naye kuhusu idadi ya waliokufa katika operesheni hiyo.

Katika kesi ya msingi, Zitto anakabiliwa na mashtaka matatu ya uchochezi. Anadaiwa kutenda makosa hayo, Oktoba 28, 2018 katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi za makao makuu ya chama cha ACT-Wazalendo.




## Daktari feki anaswa akitibu wagonjwa

INATOKA UK. 5

alipofika kutoka Visiga, amekuwa akijitambulisha kuwa yeye ni daktari anayetibu watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali.

Pia alisema mtu huyo katika kufanya hivyo, taarifa zinaeleza kuwa alipatiwa Sh. milioni 1.2 na mtu aliyefika kutaka huduma ya tiba na mwingine alitoa Sh. 60,000 kwa tiba aliyofanyiwa.

Katika hatua nyingine, watu wengine wawili, Adinikas Kyuvu (45) raia wa Kenya na Deo Mapunda (32) mkazi wa kijiji cha Mbinga Mhalule Wilaya ya Songea, wamekamatwa kwa tuhuma za kufanya utapeli.

Kamanda Maigwa alisema Agosti 8, mwaka huu, majira ya saa 10 alasiri katika nyumba ya kulala wageni ya Gosaki, Bombambili Manispaa ya Songea, polisi wakiwa kwenye doria, walimkamata Kyuvu anayedaiwa kuwa mchungaji kutoka Nairobi, Kenya akiwa na vipande vya chupa, shanga, kwato ya ng`ombe, chupa tano za ubani na kifuu cha nazi.

Alisema mchungaji huyo alikuwa anatumia vifaa hivyo kutapeli watu wakati wa maombezi ili kuwaaminisha kuwa anatenda miujiza na kwamba vipande hivyo vya chupa vinatoka kwenye vinywa vya binadamu jambo ambalo limeonekana si la kweli.

Mtuhumiwa huyo pamoja na kukamatwa, alisema amepelekwa ofisi za Idara ya Uhamiaji kwa upelelezi zaidi na kwamba polisi wanaendelea na upelelezi wa kina na utakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Pia alisema Agosti 11, majira ya saa 2:00 usiku katika kijiji cha Mbinga Mhalule, wilayani Songea, polisi walimkamata Deo Mapunda (32) kwa tuhuma za kujifanya mganga wa kienyeji anayeweza kufufua watu waliokufa.

Kamanda Maigwa alisema chanzo cha taarifa hizo kilieleza kuwa mtu huyo aliyejifanya mganga wa kienyeji, alifika kijijini hapo na wenzake wawili wakiwa wamebeba jeneza ambalo alidai anatibu na kufufua watu waliokufa, jambo ambalo lilisababisha watu wengi waliowahi kufiwa na ndugu zao kufika ili kusaidiwa ndugu zao kufufuka.

Alisema Mapunda na wenzake waliendelea kutoa huduma hiyo na siku ya tukio wakati wakiendelea kutoa huduma ndani ya jeneza, alikuwamo mwenzake aliyetambulika kwa jina moja la Abdul kwa lengo la kuwaaminisha watu walifika ili wasaidiwe kuwa aliyepo ndani ya jeneza ni marehemu na ana uwezo wa kumfufua na baada ya kufanya mambo ya udanganyifu aliamka na kusimama japokuwa alikuwa hawezi kuzungumza.

Maigwa alisema kitendo hicho kiliashiria kuwa mtu huyo alikuwa amefufuka na alipelekwa nyuma ya nyumba akiwahakikishia kuwa ifikapo saa 6:00 usiku ataanza kuzungumza.

Alisema kuwa baada ya kitendo hicho kufanyika, wananchi walikwenda nyuma ya nyumba hiyo na kubaini kuwa mtu huyo aliyekuwa ndani ya jeneza na baadaye kusimama ametoweka katika mazingira ya kutatanisha, ndipo wakagundua kuwa wamedanganywa.

Kutokana na kitendo hicho, alisema wananchi walimkamata na kwa hasira waliamua kuchoma moto jeneza kisha kutoa taarifa ya tukio hilo katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Songea Mjini.

Alisema katika mahojiano ya awali mtuhumiwa Mapunda alikiri kuwa yeye si mganga anayeweza kufufua watu bali njia aliyoitumia wenzake ilikuwa na nia kutaka ya kujipatia fedha.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA / MASHAMBA**

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**

Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:155....2018**

**Mdai: HAMAD ALLY ISLAM**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: ONESMO LYANZILE**

**Kwa:**
**ONESMO LYANZILE**
**KILOSA**
**MOROGORO**

**Ombi la Mdai:**
**HAMAD ALLY ISLAM**

**Madai ya: PESA SHILINGI 2,241,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 04 mwezi 09 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 08 mwaka 2019.

215374202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA MTIBWA WILAYA YA MOROGORO.**
**MADAI NAMBA..33..2019**
**Mdai: MOSSES JOSEPH SHIO**
**ANAMDAI**
**Mdaiwa: JOYCE JOHN**
**Kwa:**
**JOYCE JOHN.**
**AJULIKANI ALIPO**

Kwa kuwa mdai/wadai Ameleta /wameleta madai Yake/yao kwamba/eleza hapa habari ya madai;
TARAKA
MGAWANYO WA MALI
MATUNZO YA MTOTO

Kwa hiyo unaitajiwa /Mnaitajiwa kuhudhuria binafsi ktk mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 26-08-2019 SAA 2:00 Asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na kwakuwa siku hiyo no siku ya kukatwa shauri hilo,ni lazima kuleta Mashahidi wako/Wenu na hati zote zonazohisu shauri hilo kwa ajiri ya kujitetea ktk shauri hilo.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 08 mwaka 2019.

215375002

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI.

**MASANJA SALUM MBUGUZI** MKAZI WA TINDE HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI T,193 AZG AMBAYO ILIPOTEA MWAKA JANA MAENEO YA TINDE HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA MASANJA SALUMU MBUGUZI KWA SIMU NAMBA 0756295243

**RB NAMBA SHY/RB/ TR/495/ 2019**

215372402

### KUPOTEA KWA VYETI



**Emmanuel Rwachuma Ruhinda** anatangaza kuptelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0118-0010** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1998 katika shule ya Sekondari Seminary Katoke, cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0126-0513** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2001 katika Shule ya Sekondari Magamba. Yeyote atakaeiona atoe taaifa kituo chochote ch Polisi.

**Polisi Taarifa: BI/RB/4133/2011**

115372502

### KUPOTEA KWA CHETI



**Pamela Joseph Towilo** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4479-0010 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari St. Ann's.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi taarifa: DAR/CEN/RB/207303/2019**

115373202

### KUPOTEA KWA CHETI



**Mercy Zephania** anatangaza kupotelewana cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0308-0061** kilichotolewa ba Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari Enaboishu.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo

chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: ARU/ARU/RB/171313/2019**

115372902

### KUPOTEA KWA CHETI




**Biime Hamad Khamis** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Taaluma ya Ualimu Grade A chenye **index namba E0616-0012** kilichotolewa na Chuo cha ualimu Ununio Dar es Salaam mwaka 2013.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: MBW/RB/8474/2019**

115372602

### KUPOTEA KWA CHETI



**Christopher Leonard Machange** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2626-0051** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Charlotte.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .**

**Polisi taarifa: MOR/RB/180124/2019**

115373302

### MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **UCHUMI COMMERCIAL BANK, SISI JIKUZE BUSINESS SOLUTION** tutauza kwa mnada wa hadhara Kiwanja cha mdaiwa sugu mali ya **Ndugu Wiliam Nyello chenye No. 352,Kitalu D** kilichopo eneo la MSARANGA NG'AMBO-MOSHI -. Lengo ni kufidia / kupunguza deni la mkopo anaodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe **24/08/2019 kuanzia saa nne asubuhi,** mahali dhamana ilipo.

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:-**
**0757433333/0652113262/0717616227**

215374602

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EDMONTON TRAVEL &TOURS.** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA yenye namba za usajili T 663 AUT.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/199884/2019**

215374902

### KUPOTELEWA NA KADI YA TANKER LA MAFUTA

**EDMONTON TRAVEL &TOURS.** anatangaza kupotelewa na kadi ya tanker la mafuta rangi ya blue yenye namba za usajili **T 765 ACJ .**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/199878/2019**

215374902


## NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

## KWA BEI NAFUU SANA

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BRESCIA WAJITOSA KUMSAJILI BALOTELLI



**MILAN,** Italia

KLABU ya Brescia imejitosa ofa ya mwisho ya kutaka kumsajili 'mtukutu' Mario Balotelli.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa sasa hana klabu yoyote baada ya kuachwa na Marseille kipindi cha majira ya joto.

Maofisa wa Klabu ya Flamengo walisafiri kwenda Ulaya Jumanne kukutana na wakala wa Balotelli, Mino Raiola, kufanya mazungumzo kwa ajili ya kumsajili wiki hii.

Lakini klabu ya mji wa nyumbani kwa Balotelli, Brescia imeamua kujitosa kutaka kumsajili mchezaji huyo. Kwa mujibu wa gazeti la CalcioMercato klabu hiyo iliyopanda kucheza Ligi Kuu ya Serie A, imempa ofa Balotelli ya pauni milioni moja kwa mwaka pamoja na bonasi ambayo itamfanya achukue pauni milioni 2.5.

Inaeleweka kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia anaziaangalia ofa zote mbili kwa makini kabla ya kufanya maamuzi yake, kwa sababu Flamengo nao wametoa ofa nzuri. Klabu hiyo ya nchini Brazil imeripotiwa kwamba imefanya mazungumzo na Balotelli na wapo tayari kumlipa pauni milioni 13.8 kwa mkataba wa miaka miwili na nusu.

West Ham pia ilitoa ofa ya kutaka kumsajili Balotelli mwezi uliopita baada ya kumkosa Maxi Gomez nyota wa Bournemouth, Callum Wilson.

# PSG waikataa tena ofa ya Barca kwa Neymar

**BARCEONA,** Hispania

MAOFISA wa Barcelona walifanya safari Jumanne ya kwenda jijini Paris kwa ajili ya kutoa ofa ya kuwazidi wapinzani wao Real Madrid ili kumsajili Neymar, lakini mpango huo unaonekana kukwama baada ya ofa yao ya pauni milioni 74 na kumtoa Philippe Coutinho kukataliwa.

Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu sasa amepanga kukutana na tajiri wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi leo Alhamisi jijini Liverpool wakati wa mkutano wa chama cha klabu za Ulaya.

Lakini baada ya ofa yao ya wiki iliyopita kukataliwa, wakala wa Neymar, Pini Zahavi alifanya mazungumzo ya kuhusu uwezekano wa kutua kule Real Madrid, na miamba hao wa Katalunya wakaamua kuongeza kasi ya mazungumzo na PSG.

Bartomeu aliwatuma Mkurugenzi wa Michezo wa Barcelona, Eric Abidal na wasaidizi wake, Javier Bordas na Andre Cury, kukutana na mkurugenzi wa michezo wa PSG, Leonardo na msaidizi wake, Angelo Castellazzi.

Lakini katikati ya wiki, Barcelona walipanga kutoa fedha taslimu pamoja na Coutinho, lakini PSG waliikataa.

Barcelona pia ilitoa wazo la kuongeza mchezaji mwingine ambaye ni kiungo, Ivan Rakitic.







# Roma yapanga kumchukua Lovren wa Liverpool

**ROME,** Italia

KLABU ya AS Roma ipo kwenye mazungumzo na Liverpool kwa ajili ya kumsajili beki wake wa kati, Dejan Lovren kwa pauni milioni 15 na inaweza kumaliza kipindi chake cha miaka mitano ya kukaa pale Anfield.

Lovren amejikuta hana nafasi ya kucheza tangu aliporudi kutoka kwenye kipindi cha maandalizi ya msimu mpya, kwani kocha, Jurgen Klopp anaonekana kupendelea zaidi kumtumia Virgil van Dijk na Joe Gomez pamoja na Joel Matip.

Roma imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Lovren mara kadhaa, lakini ilishindwa na sasa wana nafasi ya kumchukua mchezaji huyo kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la uhamisho mwezi Septemba 2.

Lovren aliachwa nyumbani kwenye mchezo wa jana Jumatato wa Super Cup dhidi ya Chelsea, huku Liverpool ikisema sababu ya kumuacha ni mgonjwa.

Pamoja na Van Dijk, Gomez na Matip, Liverpool imemsajili kinda wa Uholanzi, Sepp van der Berg kutoka FC Zwolle Juni pamoja na Fabinho.

Lovren kwa sasa amebakiwa na miaka miwili katika mkataba wake na hivyo ana nafasi ya kuondoka kwenye Ligi Kuu ya England.

Alijiunga na Liverpool akitokea Southampton Julai mwaka 2014 kwa pauni milioni 25 ambao kwa wakati huo ilikuwa rekodi kwa klabu hiyo.

HABARI MICHEZO

# Jovic akosa nafasi Real kutolewa kwa mkopo

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI Luka Jovic ambaye alisajiliwa Real Madrid kwa pauni milioni 62 anatarajiwa kutolewa kwa mkopo kwenda kucheza katika klabu nyingine, gazeti la Marca limeandika.

Gazeti hilo limeripoti kwamba Jovic ameshindwa kumshawishi kocha Zinedine Zidane wakati wa kipindi cha maandalizi ya msimu wa ligi na sasa anajiandaa kumtoa kwa mkopo.

Jovic alikuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa na Zidane kipindi cha majira ya joto, akisaini mkataba wa miaka sita ya kukaa hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu baadaya kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati akicheza kule Eintracht Frankfurt msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 hakuwa kwenye kiwango kizuziri wakati Real Madrid wakichezea kichapo cha mabao 7-3 kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid mapema Julai kwenye mchezo wa kujipima nguvu.

Lakini Zidane ameripotiwa kwamba hajahamasika na kiwango alichokiona kutoka kwa mshambuliaji huyo wakati wakielekea kuanza msimu mpya wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Jumamosi dhidi ya Celta Vigo.






# WILSHERE AKODI MTAALAMU WAKE WA VIUNGO

**LONDON,** England

JACK Wilshere amemkodi mtaalamu wa viungo, Declan Lynch kutoka nchini Ireland ambaye atakuwa akimfanyisha mazoezi ya peke yake mara mbili kwa wiki ili kujiweka fiti zaidi.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27 ambaye amaichezea mara 34 timu ya taifa ya England, amekuwa akikumbwa na majeruhi ya mara kwa mara katika miaka ya hivi karibuni.

Katika msimu wake wa kwanza pale West Ham alicheza mechi nane tu za Ligi Kuu baada ya kuondoka akiwa mchezaji huru kutoka Arsenal.

Akiwa Arsenal ndio alikutana na mtaalam huyo wa viungo Lynch, ambaye alichaguliwa na mkuu wake, Colin Lewin mwaka 2012.

Wilshere anamlipa yeye mwenyewe Lynch, na kwa ajili ya kufanyiwa mazoezi hayo ambayo amaanini kuwa yatamuweka fiti.

Na kocha wake, Manuel Pellegrini hana tatizo na mpango huo wa Wilshere kwa sababu hata yeye anataka mchezaji huyo awe fiti kwa ajili ya kumtumia kwenye kikosi chake.

Lynch aliondoka Arsenal na kwenda kufanya kazi pale Bath katika klabu ya mchezo wa rugby.

# *Solskjaer kumweka akiba Sanchez*

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer yupo tayari kumpeleka Alexis Sanchez kujifua na timu ya akiba kama hatakubali kuondoka klabuni hapo, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Manchester United ipo kwenye harakati za kutaka kumuuza Sanchez, ambaye analipwa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki, kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Ulaya Septemba 2 mwaka huu.


Roma kwa sasa ndio klabu pekee iliyoonesha nia ya kutaka kumsajili Sanchez, lakini mshahara wake ndio unaonekana kuwa kikwazo cha kukamilika kwa mazungumzo.

United imeripotiwa kwamba, ipo tayari kugawana na timu nyingine kubeba mzigo wa mshahara wa Sanchez kama klabu nyingine itamchukua kwa mkopo na yenyewe italipa asilimia kubwa.

Solskjaer haoni majaliwa ya baadae ya Sanchez hapo Old Trafford na anataka mchezaji huyo auzwe kwani hayupo kwenye mipango yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ameichezea mechi 16 tu kwenye mashindano United chini ya Solskjaer, akifunga bao moja pekee.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile amekuwa akifanya mazoezi kivyake nje ya kambi ya United ya Carrington wakati akiendelea kujiuguza maumivu yake ya misuli ya nyama za paja aliyoumia mwanzoni mwa Julai.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK: SIRI KUZIDI KUWIKA LIVERPOOL

Suala la kununuliwa dau kubwa halinisumbui, unachoweza kufanya ni kuinamisha kichwa chini na...

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Virgil van Dijk amesisitiza uhamisho wake wa pauni milioni 75 kamwe suala hilo halijawa kuwa tatizo kwake baada ya kuwa beki ghali zaidi duniani, rekodi ambayo ilivunjwa mapema mwezi huu.

**Van Dijk alijiunga na Liverpool akitokea Southampton Januari mwaka jana, uhamisho ambao ulitupiwa jicho na wengi kutokana na dau kubwa lililotumika kumnunua.**

Lakini nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi, aliisaidia miamba hiyo ya Ligi Kuu England kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na ameibuka kuwa miongoni mwa wanaowania tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ('Ballon d'Or').

Hata hivyo, rekodi hiyo ya dunia kwa upande wa beki, imevunjwa baada ya Manchester United kukubali kuilipa Leicester City pauni milioni 80 mapema mwezi huu ilipoipata saini ya beki wa kati wa England, Harry Maguire.

Van Dijk, ambaye jana waliivaa Chelsea kwenye fainali ya UEFA Super Cup iliyopigwa Istanbul, Uturuki, alipinga umuhimu wa dau hilo kwake.

"Si suala kubwa kwangu. Ni kitu ambacho huna ushawishi nacho," aliuambia mkutano wa wanahabari.

"Kinatokea sokoni, ni soko na kitu pekee unachoweza kufanya ni kuinamisha kichwa chako chini na kuanza kucheza, kujitoa kwa kila kitu kwa timu.

"Hicho ndicho ninachokifanya na kinafanya kazi hadi sasa, nitajaribu kuendelea kufanya hivyo, endelea kufanya na kuwa mchezaji bora."

Mabingwa hao wa Ulaya, Liverpool waliivaa Chelsea wakitoka kushinda 4-1 kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Norwich City wakati kikosi cha Frank Lampard 'The Blues' chenyewe kikitoka kuangukia pua ya mabao 4-0 kutoka kwa Man United.

Van Dijk anatamani upande wa Jurgen Klopp kushinda Kombe na Liverpool kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2005.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR BADO HAKIELEWEKI

PARIS St-Germain na Barcelona zimekutana rasmi kwa mara ya kwanza kujadili uhamisho wa mshambuliaji Mbrazil Neymar, lakini hakuna makubaliano yaliyofikiwa baada ya majadiliano ya saa tatu. ***(Le Parisien - in French)***

### COUTINHO, RAKITIC SASA CHAMBO

BARCELONA inajiandaa kuipa ofa PSG ya pauni milioni 93 pamoja na kiungo mshambuliaji Mbrazil Philippe Coutinho, 27, na kiungo Mcroatia Ivan Rakitic, 31, ili kubadilishana na Neymar. ***(ESPN)***

### UNITED YAFUNGUKA KWA POGBA

MANCHESTER United haitakuwa tayari kusikiliza ofa yoyote kwa kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, kabla ya dirisha la usajili la Ulaya kufungwa. ***(Telegraph)***

### SANCHEZ KUPELEKWA ROMA

MANCHESTER United inaweza kukubali kulipa sehemu ya mshahara wa Alexis Sanchez kama mshambuliaji huyu wa kimataifa wa Chile, atakubali kujiunga na Roma. ***(Sun)***

### TOBY KUMALIZANA NA SPURS

BEKI Mbelgiji Toby Alderweireld, 30, yupo tayari kumaliza mkataba wake wa mwaka mmoja na Tottenham ili aondoke akiwa huru majira ya joto yajayo. ***(Mirror)***

### SABABU CITY KUTOFUNGIWA FIFA

MANCHESTER City imeepuka kifungo cha kusajili kama cha Chelsea kwa sababu klabu hiyo "ilikubali jukumu hilo" kuhusu kuvunja kanuni za usajili wa wachezaji kinda, kwa mujibu wa msemaji wa Fifa. ***(Mirror)***

### PSG YAMTAKA SEMEDO

PSG imeiambia Barcelona ipo tayari kumwachia Neymar kurudi Camp Nou endapo itawapa pauni milioni 93, Philippe Coutinho, Ivan Rakitic na beki wa kulia Mreno Nelson Semedo, 25. ***(Mail)***

### BAKAYOKO ANUKIA MONACO

KIUNGO wa Chelsea, Mfaransa Tiemoue Bakayoko, 24, anajiandaa kurudi Monaco baada ya miamba hiyo ya Ligue 1 kufungua meza ya mazungumzo ya kumsajili kwa mkopo. ***(Mail)***

### NEWCASTLE, LONGSTAFF WATETA

NEWCASTLE United ipo katika mazungumzo na kiungo Sean Longstaff, baada ya kuivutia Man United. ***(Times)***

### WAMFUATA BALOTELLI

VIONGOZI wa Flamengo wamepanda ndege kuelekea Ulaya kufanya mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Marseille, Mtaliano Mario Balotelli, 29, kwa mkataba wa miaka miwili. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### AZIAMSHA NAPOLI, ROMA

LAZIO imejiunga na Napoli, Roma na Fiorentina katika mbio ya kuinasa saini ya straika wa Tottenham, Fernando Llorente, 34, kwa uhamisho huru. ***(Mail)***

### WILSHERE AFUATA DAKTARI

KIUNGO wa West Ham, Jack Wilshere, 27, anapanga kukwea pipa kwenda Ireland kwa kikao binafsi na daktari wake. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## KMC waanzia Gym wakisaka ya kirafiki

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kulazimisha sare tasa ugenini nchini Rwanda dhidi ya AS Kigali, timu ya KMC FC inatarajia kutafuta mechi moja ya kirafiki Jumamosi ili kusahihisha makosa yao kabla ya kurudiana na Wanyarwanda hao mwishoni mwa wiki ijayo kwenye mechi yao ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Anuari Binde alisema wanatarajia kucheza na timu ya Daraja la Kwanza au yoyote inayoshiriki Ligi Kuu.

"Mwalimu amesema anahitaji mechi moja ya kirafiki kabla ya mchezo wetu wa marudiano tukipata timu tutawafahamisha mashabiki wetu," alisema Anuari.

Aidha, alisema kwa sasa timu yao inaendelea na mazoezi ya Gym kwa muda wa siku tatu, na baadaye watahamia uwanjani.

"Juzi asubuhi tulianza mazoezi ya Gym jioni tukaenda uwanjani, tutafanya kwa siku tatu mfululizo," alisema msemaji huyo.

Alisema timu yao inaendelea vizuri na kudai kila mchezaji ameahidi kufanya vizuri katika mchezo huo, ambao watacheza nyumbani wakihitaji ushindi wowote ili kusonga mbele.

## Ruvu Shooting dimbani Uhuru

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Ruvu Shooting inatarajia kuendelea kuitafutia kasi Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza Agosti 23, mwaka huu, kwa kucheza mchezo wa kirafiki na timu ya Polisi Combine, Jumamosi ya wiki hii katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Masau Bwire, alisema baada ya mchezo huo watajipima nguvu tena na Namungo FC Agosti 20, mechi ambayo itakuwa ya mwisho kwao kabla ya msimu wa 2018/19 Ligi Kuu Bara kuanza siku tatu zijazo.

"Tupo kwenye maandalizi ya mwisho mwisho kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu ambao unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa," alisema Masau Bwire.

Aidha, aliongeza kuwa kikosi chao kipo vizuri isipokuwa wachezaji wao wawili ambao ni majeruhi, huku akifafanua kuwa msimu ujao wataingia na mabadiliko makubwa kutokana na mazoezi magumu wanayoyafanya wachezaji wao kila siku.

Katika Ligi Kuu Bara inayoshirikisha timu 20, msimu uliopita Ruvu Shooting ilimaliza nafasi ya tatu kutoka mkiani baada ya kujikusanyia pointi 45 zilizotokana na jumla ya mechi 38.

# BARIDI YAAHIRISHA MAZOEZI YANGA SC

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kikosi cha Yanga kikitarajia kupanda pipa kuelekea nchini Botswana Jumanne ijayo, kuifuata Township Rollers tayari kwa mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayopigwa Jumamosi Agosti 24, mwaka huu, jana asubuhi wachezaji wa kikosi hicho walishindwa kuhimili baridi ya mjini Moshi, hivyo kulazimika kusubiri hadi jioni ili kuweza kufanya mazoezi, imeelezwa.

**Yanga itaifuata Township Rollers ikiwa ni siku mbili baada ya kuivaa AFC Leopards ya Kenya kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha katika mchezo wa kirafiki.**

Kesho Yanga itajipima ubavu na Polisi Tanzania katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi kabla ya Jumapili kuvaana na AFC Leopards jijini Arusha.

Akizungumza na Nipashe jana, moja kwa moja kutoka mkoani Kilimanjaro, Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema baada ya kumaliza michezo yao ya kirafiki, kikosi hicho hakitarudi jijini Dar es Salaam, na badala yake kitaanzia safari ya kuwafuata Township Rollers katika Uwanja wa Ndege wa KIA.

"Tunatarajia kuondoka Agosti 20, safari yetu itaanzia KIA, kikubwa tunakwenda kupambana," alisema Hafidh.

Aidha, aliongeza kuwa jana wachezaji wao hawakufanya mazoezi ya asubuhi kutokana na baridi kali iliyopo mkoani Kilimanjaro.

"Leo (jana) hatujafanya mazoezi asubuhi mpaka jioni hali ya huku ni baridi kama kulivyo Botswana," alisema mratibu huyo.

Hata hivyo, alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri, isipokuwa Paulo Godfrey ambaye hajaweza kuungana na wenzake kutokana na kuwa majeruhi.

"Wachezaji wote tumekuja nao isipokuwa Paulo Godfrey amebaki Dar es Salaam endapo atapona tutaenda naye Botswana," alisema.

Yanga ambayo imeweka kambi mkoani Kilimanjaro ili kuzoea hali ya baridi inayoelezwa kufanana na ile ya Botswana kwa sasa, inahitaji ushindi ama sare ya kuanzia mabao mawili ili kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kufuatia mechi ya awali katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kumalizika kwa sare ya bao 1-1.



Wachezaji wa timu ya Lipuli FC ya mkoani Iringa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Chuo cha Ualimu Mkwawa (MUCE) wiki iliyopita, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kuanza Agosti 23, mwaka huu. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# *Yosso wa Tanzania kutua leo Asmara*

**Na Somoe Ng'itu,** ERITREA

KIKOSI cha timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 15 cha Tanzania (U-15), kinatarajiwa kutua jijini Asmara, Eritrea leo kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yanayotarajiwa kufanyika nchini hapa, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jijini Asmara jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), Nicholas Musonye, alisema yosso hao wa Tanzania wanatarajia kuwasili nchini hapa leo asubuhi tayari kuanza safari yake ya kuwania kombe la michuano hii.

Musonye alisema kuwa timu nyingine zinazotarajiwa kuwasili leo ni pamoja na yosso kutoka Rwanda, Uganda na Ethiopia.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuwaeleza kuwa tayari timu nne zimeshafika hapa, nazo ni Kenya, Somalia, Sudan na wenyeji Eritrea, maandalizi yako katika hatua za mwisho, tunatarajia kuwa na mashindano mazuri na yenye mafanikio kwa maendeleo ya soka kwenye ukanda wetu," alisema Musonye.

Aliitaja timu ya Djibouti imejitoa katika mashindano hayo ambayo yamepangwa kuchezwa kwenye mji mmoja wa Asmara na yakilenga kutoa nafasi kwa wachezaji chipukizi kujifunza.

Aliongeza kuwa baada ya kujitoa kwa Djibouti, ratiba ya mashindano hayo ambayo awali ilikuwa katika makundi matatu itabadilika, na leo jioni timu zote zitajulishwa kuhusu ratiba mpya pamoja na kanuni za michuano hii.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Cecafa, Doris Petra, aliwashukuru viongozi wa baraza hilo ambalo wameandaa timu zao kuja kushiriki katika michuano hii.

Petra aliwataka viongozi wa timu zote zilizofika nchini hapa kuhakikisha wanashirikiana ili kufanikisha mashindano haya yanafanikisha malengo yake.

"Tunahitaji kuona wachezaji wetu wanafurahia mpira, wanahitaji kujifunza na kupata wakati mzuri wa kupata uzoefu," aliongeza kiongozi huyo.

# Michezo

Alhamisi Agosti 15, 2019

Nipashe




Van Dijk: Siri kuzidi kuwika Liverpool UKURASA 30




Meneja Mradi wa Sprite BBall Kings 2019, Bhoke Egina, akizungumza na vyombo vya habari jana kuhusu usajili na uzinduzi wa mashindano hayo utakaofanyika Jumamosi.
**PICHA: SABATO KASIKA**

# Aussems: Simba hii si yakupigwa tena bao 5

## ●●● Asema gharika ya mabao ugenini haitatokea, achungulia ubingwa wa kwanza Ngao Jamii na kuahidi...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikishushiwa gharika ya mabao katika mechi za kimataifa hususan kilipocheza ugenini kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema aibu hiyo haiwezi kujirudia tena msimu huu.

**Msimu uliopita Simba ilipoteza mechi zake zote za ugenini kwenye hatua ya makundi tena kwa kipigo kitakatifu, kabla ya robo fainali kwenda kutolewa ugenini na TP Mazembe ya DR Congo kwa kuchapwa mabao 4-1 baada ya sare tasa Uwanja wa Taifa .**

Hatua ya makundi licha ya kushinda mechi zake zote nyumbani, ugenini ilianza kwa kukubali kuchapwa mabao 5-0 dhidi ya AS Vita ya DR Congo na kipigo kama hicho ikikipata ilipoifuata Al Ahly nchini Misri na mabao machache ilifungwa ilipocheza nchini Algeria dhidi ya JS Saoura baada ya kukubali kulala 2-0.

Simba ambayo msimu huu pia inaipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, tayari imecheza mechi moja ya raundi ya awali ugenini Msumbiji dhidi ya UD Songo na kufanikiwa kupata sare tasa.

Akizungumzia namna kikosi chake kilivyojipanga kimataifa msimu huu, Aussems alisema kwa usajili walioufanya umempa kikosi kipana zaidi na ana uhakika kipigo cha mabao mengi ugenini hakiwezi kutokea tena.

Alisema kutokana na kuongezeka baadhi ya nyota mfumo watakaoutumia msimu huu utakuwa tofauti na msimu uliopita na kwamba tayari wameanza kufanya hivyo kwenye mechi yao ya raundi ya awali ugenini dhidi ya UD Songo ambayo hawakuruhusu bao.

"Msimu uliopita ushindi pekee ugenini ulikuwa raundi ya awali dhidi ya Mbambane Swallows ya Eswatini (Simba ilishinda 4-0), ambayo haikuwa timu imara ukilinganisha na zingine tulizokutana nazo, hivyo hatutaruhusu tena mabao mengi," alisema.

Simba msimu huu imeongeza nguvu kwa kuwasajili Kiungo Msudan Sharaf Eldin Shiboub, Wabrazili mshambuliji Wilker Henrique da Silva, kiungo Gerson Fraga Vieira, beki Tairone Santos da Silva na winga Mkongomani Deo Kanda, huku kwa wazawa ikiwasajili kipa Beno Kakolanya, beki Gadiel Michael, kiungo Ibrahim Ajibu, beki Haruna Shamte, winga Miraji Athumani na beki Kennedy Juma.

Aidha, akizungumzia kuelekea mechi ya Ngao ya Jamii Jumamosi dhidi ya Azam FC itakayopigwa Uwanja wa Taifa saa moja usiku, alisema kikosi kitakachoshuka uwanjani siku hiyo kitakuwa tofauti na kitakachovaana na UD Songo mwishoni mwa wiki ijayo.

"Kwa sasa mipango yetu ni kupata kombe la kwanza msimu huu kwa kubeba Ngao ya Jamii, baada ya hapo tutaanza kujiandaa na mechi dhidi ya UD Songo, ila mfumo na hata kikosi kitabadilika," alisema Aussems.

# Kumekucha Sprite BBall Kings 2019

**Na Sabato Kasika**

USAJILI wa timu zitakazoshiriki mashindano ya Sprite BBall Kings 2019, unatarajiwa kufanyika Jumamosi jijini Dar es Salaam, ukienda sambamba na uzinduzi wa mashindano hayo.

Meneja Mradi wa Sprite BBall Kings 2019, Bhoke Egina, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi kutoka vyombo mbalimbali vya habari kuhusu ma andalizi ya mashindano hayo.

"Mashindano haya yanatarajia kushirikisha timu zote za mpira wa kikapu kutoka pande mbalimbali hapa Tanzania huku yakifanyika viwanja tofauti ndani ya Jiji la Dar es Salaam," alisema Egina.

Alisema mashindano hayo yanaandaliwa na East Africa Televisheni na East Africa Radio kwa kushirikiana na kinywaji cha Sprite na kwamba wachezaji wanaoruhusiwa ni kuanzia miaka 16 na pia kila timu itakuwa na wachezaji 10.

"Michuano ya Sprite BBall Kings 2019 inajumuisha hatua mbalimbali kuanzia usaili, mtoano, hatua ya 16-bora, robo fainali, kisha nusu fainali na mwisho itafanyika fainali kamili," alisema.

Egina alisema bingwa wa michuano hiyo atajinyakulia Sh. milioni 10 na Kombe la Sprite BBall Kings 2019, huku mshindi wa pili akizawadiwa Sh. milioni tatu wakati mchezaji bora ataibuka na kitita cha Sh. milioni mbili na kikombe.

"Mashindano ya Sprite BBall Kings 2019 yalianzishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2017 na jumla ya timu 52 kutoka pande mbalimbali za Tanzania zilishiriki, lakini safari hii tunatarajia kuwa na timu zaidi ya hizo," alisema.

Egina alifafanua kwamba, East Africa Televisheni na East Africa Radio ni chombo cha habari ambacho kinaziunganisha nchi za Afrika Mashariki kwa kuwalenga zaidi vijana kuanzia miaka 18 hadi 35 kwa lengo la kuwahabarisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha kupitia vipindi mbalimbali.